

# Wadhihirishaji Pacha



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 4

# Wadhihirishaji Pacha

Taasisi ya Ruhi

Vitabu katika Mlolongo:

Hapo chini yapo majina ya vitabu vilivyopo kwa sasa katika mlolongo ulioandaliwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vinakusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika juhudi ya kimpangilio ili kuimarisha uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inakuza seti moja ya kozi zinazochepua kutoka kitabu cha tatu katika mlolongo kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya watoto ya Kibahá'í, na halikadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuinua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hizi, pia, zimeoneshwa katika orodha hapo chini. Inapaswa kukumbukwa kwamba orodha hii inaweza kubadilika kadiri uzoefu uendeleavyo ugani, na majina ya ziada yataongezwa kadiri idadi ya vipengele vya kimtaala vinavyoendelea kukuzwa vifikiapo hatua ambapo vinaweza kusambazwa kwa upana.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinukaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Duara Lipanukalo: Mchepuo wa pili wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Ufundishaji Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja katika Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mjadala ya Umma* |

Hakimiliki © 2001, 2023 ya Udhamini wa Ruhi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.1.PE.PV (tafsiri ya muda) zilizochapishwa Septemba 2023
ISBN 978-628-95545-5-7

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Las Manifestaciones Gemelas*
Hakimiliki © 1987, 1997, 2021 ya Udhamini wa Ruhi, Colombia
ISBN 978-958-53332-2-2

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo


Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi .......... v

Ukuu wa Siku Hii ................................................. 1

Maisha ya Báb ..................................................... 15

Maisha ya Bahá’u’lláh......................................... 69

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Hadi washiriki wafike hapa, kozi ya nne iliyotolewa na Taasisi ya Ruhi, wao kwa uhakika watakuwa wameendelea katika njia ya utumishi iliyofunguliwa na mfuatano mkuu wa kozi. Wowote uwao usuli wao pale walipoingia katika Kitabu cha 1, sasa wao watakuwa wameshajikita katika muono wa mbadiliko wa mtu binafsi na wa jumuiya ulioelezwa katika Maandiko ya Bahá'u'lláh. Kufikia hatma hii, wao watakuwa wameanza kujenga tabia ya kusoma maneno Yake kila siku na watakuwa wanachota chakula cha kiroho, pote pawili katika mikutano ya ibada na katika nyakati za kutafakari kwa ukimya, kutoka kwenye sala na mashauri ambayo Yeye amefunua. Wao watakuwa wanajifunza kufanya maongezi pamoja na marafiki na jamaa juu ya kanuni za kiroho Yeye alizofundisha na watakuwa wanafanya matembezi ya majumbani katika kijiji chao au ujirani kwa ajili ya kujadili juu ya mafundisho Aliyoleta ya kujenga upya ulimwengu. Baadhi watakuwa wanaendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Katika hatua hii ya njia ya huduma, basi, wao watakuwa tayari — wenye shauku haswa — kufahamu kikamilifu zaidi maisha ya Yule ambaye mafundisho Yake yamewaathiri kwa kina sana, na kuthamini zaidi hali za kihistoria zilizoambatana na kuzaliwa na ukunjukaji wa polepole wa Ufunuo Wake. Vitengo vitatu vya Kitabu cha 4 vinakusudia kuwapatia washiriki fursa hii.

Maisha ya Mdhihirishaji wa Mungu, kwa uhakika, kimsingi ni tofauti kutoka yale ya wanadamu wengine, na Ukuu Wake hauwezi kueleweka kwa kusoma tu matukio yanayomzunguka Yeye. Katika miaka ambayo anaishi duniani, uwezo Wake usiokuwa wa kawaida unakuwa juu ya sayari nzima, na kuleta mabadiliko katika uhalisia wa vitu vyote vilivyoumbwa na kuisukuma jamii ya wanadamu kuelekea kwenye hatua mpya ya maendeleo. Ingawa kwa macho ya nje maisha Yake yanaweza kuonekana kuwa yamejaa shida, macho ya kiroho yanaona katika kila tukio dalili za utukufu Wake na ufahari. Kuwaandaa washiriki kwa ajili ya kusoma historia ya maisha ya Báb na Bahá'u'lláh, yaliyojadiliwa katika kitengo cha pili na cha tatu kwa mfuatano, wa kwanza vinawataka wafikiri kuhusu maana ya Siku hii tunamoishi, Siku ambayo imeshuhudia uonekanaji wa Wadhihirishaji wawili wa Mungu.

Kitengo hiki ni kifupi kwa wastani. Kina mafungu kadhaa kutoka maandiko ya Kibahá'í yanayoongelea ukuu wa Siku hii, pamoja na mazoezi machache ya kawaida. Pamoja, haya yatawawezesha washiriki kutafakari siyo tu juu ya asili ya wakati huu katika historia, pale ambapo muungano wa jamii ya wanadamu hatimaye, sasa unawezekana, lakini juu ya majukumu ambayo maarifa haya yanatusukuma juu ya kila mmoja wetu. Wale wanaohudumu kama wakufunzi wa Kitabu cha 4 sharti watambue kuwa kitengo hiki kinaamini kuwa washiriki tayari wanao uelewa wa msingi wa baadhi ya dhana za kimsingi za Imani, walioupata pote pawili, kutoka masomo ya kozi za awali na katika kujishughulisha katika maisha ya jumuiya yao. Ya kwamba vitabu vyote vya dini vya zamani vimeongelea Siku iliyoahidiwa ya Mungu ambapo amani na haki vitasitawishwa juu ya ardhi, ya kwamba Bahá'u'lláh ameinua bendera ya amani ya ulimwengu na ameiita jamii ya wanadamu kukubali umoja wake wa lazima, ya kwamba Yeye amekazia uoni wa jumuiya ya wafuasi wake juu ya lengo la utaratibu mpya wa ulimwengu — hizi ni miongoni ya dhana zilizopo chini ya majadiliano ya kitengo, "Ukuu wa Siku Hii".

Vitengo viwili vinavyofuata vinaandika maelezo ya matukio kufuatana na tarehe ambavyo vimeisogeza Imani mbele kutoka jioni ile ya kukumbukwa katika mwaka 1844, ambapo Báb alitangaza Dhima Yake, hadi kufikia kwenye muda wa masaa ya alfajiri baada ya takriban miaka hamsini baadaye ambapo roho ya Bahá'u'lláh' ilipopaa kutoka sura hii ya dunia ya uwepo. Masimulizi haya ya kikalenda hususan katika kitengo cha tatu juu ya maisha ya Bahá'u'lláh, yanakamilishwa na mafungu kutoka Maandiko ambayo yanaangaza baadhi ya mada za kiroho zinazohusu nafsi ya Mdhihirishaji. Mafungu kadhaa miongoni mwa haya yamefuatwa na mazoezi; mengine yanadai usomaji wa kurudia mara nyingi na tafakari binafsi. Wakati mkufunzi atataka kuhakikisha kuwa washiriki wanapata ujuzi kamili na wa hatua kwa hatua kuhusu maisha ya Báb na Bahá'u'lláh watakapokuwa wanasoma vitengo hivi, ni zile kweli za kina za kiroho zinazoweza kupatikana kutoka matukio yaliyoelezwa ambazo ni zenye umuhimu wa msingi.

Wakati anajiandaa kukipitisha kikundi katika kitengo cha pili na cha tatu, hapo, mkufunzi anapaswa kufikiria kwa uangalifu mada za kiroho zinazoongelewa. Kwa mfano, miongoni mwao zimo mada hizi, kwamba kila Kiongozi mtukufu anadhihirishwa katika ulimwengu wa jamii ya wanadamu siyo kwa hiari Yake, bali kwa Amri ya Mungu, Ambaye humjaalia ujuzi wa kiasili; kwamba wa kwanza kutambua Daraja Lake wanaitwa kufanya vitendo vya ushujaa mkubwa, vitendo vinavyoshuhudia uwezo unaobadili wa Imani Yake; kwamba Yeye anakubali kuvumilia maisha yenye mateso ili aweze kuongoza jamii ya wanadamu kwenye ukweli na kuifahamisha kusudi na Amri ya Mungu kwa muumbo Wake; na kwamba hakuna nguvu duniani, hata ikiwa yenye uwezo mkubwa kiasi gani,inaweza kupunguza athari Yake au kumzuia Yeye kukamilisha Dhima Yake ambayo amekabidhiwa. Kuhusiana na hili, dhana moja muhimu inayoongelewa katika kitengo cha tatu ni ile ya hatari na ushindi. Uelewa wa dhana hii — kwamba kila hatari katika Hoja ya Mungu hutumika kuachilia kipimo kipya cha uwezo wa kiasili — ni lazima kwa ajili ya wale wote wanaotembea njia ya huduma, siyo tu kwamba wathamini historia ya Imani, bali pia kwamba waweze kuchangia kwa ukunjukaji wake thabiti katika ujirani na vijiji vyao, mchakato ambao hauepuki kupitia mifuatano kadhaa ya hatari na ushindi.

Tafakari juu ya mada kama hizi itawasaidia washiriki kuona katika matukio yanayohusu maisha ya Báb na Bahá'u'lláh joto la upendo Wao kwa ajili ya jamii ya wanadamu na tabia iliyotukuka ya Dhima Zao zinazofuatana. Itatumika kuvuta mioyo yao karibu zaidi kwa Mdhihirishaji wa Mungu na kuweka imara hatua zao katika njia ya huduma kwa Hoja Yake. Pia itaendeleza uwezo wao wa kuongea pamoja na watu wengine kuhusu uwepo wa Bahá'u'lláh na Ufunuo Wake, uwezo ambao walikuwa wakiendelea kuukuza, tangu waliposoma masimulizi ya maisha Yake katika Kitabu cha 2. Kwa minajili ya kupata uwezo wa kusimulia historia ya maisha Yake na maisha ya Mtangulizi Wake kwa namna ambayo masimulizi yatagusa mioyo ya wasikilizaji, hutegemea zaidi ya yote, juu ya uelewa wa maana za kiroho ya matukio yaliyosimuliwa. Bila shaka, mazoezi mengi pia yanahitajika, na mkufunzi lazima ahakikishe kuwa washiriki wanapewa fursa za kutosha za kuhusisha tukio moja la lingine kutoka maisha ya Wadhihirishaji Pacha. Baadhi ya washiriki pengine pia wataweza kutambulisha kile wanachojifunza katika maongezi yanayofanyika pamoja na marafiki na majirani kama sehemu ya mfuatano wa matembezi kwa kaya zao. Ili kuweza kuwasaidia katika matembezi haya na mengineyo, kijitabu chenye michoro na maelezo mafupi kimeambatanishwa pamoja na kila kitengo cha historia. Kijitabu hiki kinaweza kufanyiwa nakala, kamma inavyohitajika, au kinaweza kupakuliwa kutoka tovuti ya umma ya Taasisi ya Ruhi.

Ni muhimu kutaja hapa kwamba matukio yanayohusu maisha ya Wadhihirishaji Pacha yamenukuliwa katika vitengo kufuatana na kalenda ya Kigregori ambapo vilitokea. Siku hizi,

maadhimisho ya matukio muhimu husherehekewa mnamo tarehe za Kibahá'í, kufuatana na maelezo ya kalenda ya Badí',na mlingano wake wa tarehe za Kigregori zinaweza kutofautiana mwaka hadi mwaka. Mkufunzi hahitaji kuingia katika mjadala kuhusu suala hili pamoja na wajumbe wa kundi, polepole itakuwa wazi kwao kadiri watakavyo shiriki katika maadhimisho ya Siku Takatifu katika jumuiya zao. Hakika, wakati wa shughuli hizi na nyingine kwa ujumla, matukio kutoka maisha ya Wadhihirishaji na ya siku za mwanzo za Imani aghalabu husimuliwa, na hii itawapatia washiriki umaizi zaidi katika mazingira ya kihistoria yaliyotoa msukumo wa mwanzo kwa michakato wanayoipeleka mbele katika kijiji au ujirani wao leo.



# Ukuu wa Siku Hii

## Kusudi

Kupata umaizi na maana ya Siku hii na matumaini inayobeba kwa ajili ya jamii ya wanadamu

## SEHEMU YA 1

Sisi tumebarikiwa kuishi katika kipindi hiki maalum cha historia ya wanadamu — zama zilizozinduliwa na Wadhihirishaji wawili wa Mungu, Bahá'u'lláh na Mtangulizi Wake, Báb waliokuja kuvifanya upya viumbe vyote. Tunaona, mbele ya macho yetu wenyewe, jinsi nguvu zilizoachiliwa na Wadhihirishaji hawa zinavyobadilisha jamii ya wanadamu, jinsi ulimwengu mkongwe unavyopita na kuondoka na ule mpya unavyosimamishwa badala yake. Ni kweli, kwa uhakika, kuwa kufa kwa utaratibu wa zamani kunaambatana na mateso yasiyoelezeka. Hatuna budi kuathiriwa na kusikitishwa sana na mateso haya makubwa mno. Walakini hatuelemewi, kwa kuwa tunatambua kwamba ulimwengu unasonga mbele kwa uthabiti kuelekea kwenye ustaarabu mtukufu ambao Bahá'u'lláh ameutabiri.

Hii ni Siku ya Mungu. Kuishi katika Siku ya Mungu ni fadhila isiyopimika, lakini fadhila hiyo inamaanisha pia majukumu mazito. Kuthamini vyema ukubwa wa fadhila hii na kutimiza wajibu wetu ipasavyo, sisi lazima tutafakari kila mara juu ya maana na ukuu wa Siku hii, na tuendelee zaidi kutambua kusudi la Mungu kwa ajili ya jamii ya wanadamu. Kusudi la kitengo hiki, ambacho ni kifupi, ni kututambulisha baadhi ya mafungu kutoka katika Maandiko ya Kibahá'í yanayoongelea maana ya zama hizi tunamoishi. Kabla ya kujifunza mafungu haya na kutafakari juu ya maana yao, pengine itakusaidia wewe na wenzako katika kikundi chako kubaini baadhi ya malengo ambayo Mungu amekusudia kwa ajili ya jamii ya wanadamu katika siku huu. Muungano wa watu wote wa ulimwengu kuwa familia moja ya wote, sisi tunajua kuwa ni miongoni ya malengo tunayotakiwa kuyapata katika zama hizi. Ni yapi mengine machache?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## SEHEMU YA 2

Bahá'u'lláh husema:

**"Kwa Ukweli ninasema, hii ndiyo Siku ambamo jamii ya wanadamu inaweza kuuona Uso, na kusikia Sauti ya Mwahidiwa. Wito wa Mungu umepaazwa, na mwanga wa uso Wake umeinuliwa juu ya watu. Imempasa kila mtu kufutilia mbali dalili ya kila neno lisilofaa kutoka ubao wa moyo wake, na kutazama, kwa akili iliyo wazi na isiyopendelea, juu ya alama za Ufunuo Wake, mathibitisho ya Dhima Yake, na dalili za Utukufu Wake"**[1]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Katika Siku hii, sisi tunaweza kuuona _______________, na kusikia ________________, ya Mwahidiwa.

b. ________________________ wa ___________________ umepaazwa, na ____________ wa ____________ Wake umeinuliwa juu yetu.

c. Ni wajibu wetu kufutilia mbali ________________ ya kila ________________ lisilofaa kutoka ubao wa ________________________ , wetu, na kutazama, kwa _____________ iliyo __________________ na ______________ juu ya _______________ za Ufunuo Wake, _______________ wa Dhima Yake, na _______________ za Utukufu.

2. Ni yapi miongoni mwa mawazo yafuatayo yanayowazuia watu wasitambue ukweli wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh?

_____ "Dini ya wazazi wangu inanitosha."

_____ "Jamii ya wanadamu inahitaji majira ya mchipuo ya kiroho."

_____ "Dini ni nzuri kwa wale wanaoihitaji."

_____ "Dini ni chanzo cha ugomvi tu, hivyo sharti iachwe."

_____ "Kadiri nionavyo mimi, dini zote takriban ni sawa, hivyo hakuna tofauti yoyote wewe ni wa dini gani."

_____ "Mungu ameitelekeza jamii ya wanadamu."

_____ "Mambo yote sharti yafanywe upya, ikiwemo dini."

_____ "Sayansi huhakikisha kuwa hakuna Mungu. Matatizo yetu yote yanaweza kutatulika kama tutatumia uwezo wa akili"

_____ "Sitaki kujifungamanisha mwenyewe na dini yoyote."

_____ "Kila mtu binafsi aruhusiwe kumjua Mungu katika njia yake mwenyewe. Kwanini tumuhitaji Mdhihirishaji?"

_____ "Tunayo Maandiko Matakatifu ya dini yetu wenyewe. Hakuna haja ya Mdhihirishaji mpya."

3. Ni zipi kati ya zifuatazo ni miongoni mwa alama za Utukufu wa Bahá'u'lláh?

_____ Ufasaha wa matamshi Yake

_____ Uwezo unaopenyeza wa Maneno Yake

_____ Mabadiliko yanayotokea katika mioyo ya wale wanaokutana na Maandiko Yake

_____ Athari ambayo Mafundisho Yake yanayo juu ya mawazo na vitendo ya watu

_____ Athari ambayo Mafundisho Yake yanayo juu ya mwelekeo wa historia

_____ Ubora wa maono Yake kwa ajili ya mustakabali wa jamii ya wanadamu

_____ Mateso na shida aliyovumilia kwa ajili ya jamii ya wanadamu

_____ Mamlaka Yake, licha ya kuwa chombo cha kuteswa cha nguvu za kidunia

_____ Uwezo wa mafundisho Yake kwa ajili ya kuunganisha watu wa kila dini na usuli

_____ Ukuaji thabiti wa jumuiya ya wafuasi Wake

_____ Uwezo wa Agano Lake la kushinda kila kizuizi na kuhifadhi umoja wa Hoja Yake

_____ Uzuri mkubwa wa Utaratibu Wake wa Utawala

_____ Jinsi ulimwengu unavyosonga mbele kuelekea Maono Yake

## SEHEMU YA 3

Bahá'u'lláh husema:

**"Kwa uhakika Siku hii ni kuu! Vidokezo ambavyo vimetajwa juu yake katika Maandiko Matakatifu yote kama Siku ya Mungu vinashuhudia juu ya ukuu wake. Roho ya kila Mtume wa Mungu, ya kila Mjumbe Mtakatifu, imeitamani sana Siku hii ya ajabu. Jamaa zote mbalimbali za dunia, vilevile, zimetamani sana kuifikia. Walakini, mara Nyota ya Mchana ya Ufunuo Wake ilipojidhihirisha yenyewe katika mbingu ya Mapenzi ya Mungu, wote isipokuwa wale ambao Mwenyezi alipendezwa kuwaongoza, walikutwa wamepatwa na bumbuwazi na wasiojali."**[2]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Kwa uhakika, Siku hii ni ________________________ ! Vidokezo ambavyo vimetajwa juu yake katika ___________________________________ yote kama __________________________ vinashuhudia juu ya _________________ wake .

   b. Roho ya kila _____________________ wa Mungu, ya kila _______________ _________________ , imeitamani sana Siku hii ________________ .

   c. __________________________________________________ za dunia, vilevile, ____________________ sana __________________ .

   d. Mara tu ______________ ya Siku ya Ufunuo Wake ______________________ yenyewe katika mbingu ya Mapenzi ya Mungu, wote isipokuwa wale ambao ________________________________________ , walikutwa _______________ na ____________ na ______________________ .

2. Kutokana na uteuzi uliopo hapo juu, ni dhahiri kwamba hii ni siku ya utimilizo. Mitume wote na Wajumbe wa Mungu wametabiri kuja kwa Siku ambapo amani na upatano vitasimamishwa duniani. Bahá'u'lláh anarejea katika fungu kwa wale ambao, ingawa walisubiri kwa shauku Siku iliyoahidiwa, wao hawakumkubali Yeye pale Yeye alipotangaza ujio wake. Taswira nyingi zinakuja akilini pale mtu anapofikiri juu ya roho inayomtambua Bahá'u'lláh. Jaza katika nafasi maneno yanayofaa: kuwa macho, yakini, utambuzi, kuamini, tumaini.

a. Kusogea kutoka kwenye usingizi hadi kwenye ___________________________

b. Kusogea kutoka kwenye uzembe hadi kwenye ____________________________

c. Kusogea kutoka kwenye unyonge hadi kwenye ___________________________

d. Kusogea kutoka kwenye tuhuma hadi kwenye ____________________________

e. Kusogea kutoka kwenye shaka hadi kwenye ______________________________

3. Unafikiri ni kitu gani kinachoweza kufungua moyo kwa Ufunuo wa Bahá'u'lláh?

## SEHEMU YA 4

Bahá'u'lláh anasema:

**"Hii ndiyo Siku ambamo fadhila bora kabisa za Mungu zimemiminwa juu ya watu, Siku ambamo neema Yake yenye nguvu imeingizwa ndani ya viumbe vyote vilivyoumbwa. Inawapasa watu wote wa ulimwengu kusuluhisha tofauti zao, na, kwa umoja kamili na amani, waishi chini ya kivuli cha Mti wa uangalizi Wake na wema Wake wenye upendo. Inawabidi kushikilia chochote kile ambacho, katika Siku hii, kinapelekea kwenye utukuzaji wa madaraja yao, na uendelezaji wa maslahi yao bora kabisa."[3]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Katika Siku hii, _______________ bora kabisa za Mungu _________________ __________ juu ya watu.

b. Katika Siku hii _____________________ ya Mungu yenye nguvu _______________ ndani ya viumbe vyote.

c. Inawapasa watu wote wa ulimwengu _________________ tofauti zao, na, kwa _______________________ , na, ___________________________ waishi chini ya ________________ , cha ____________________ Wake wa _________________ na _________________ Wake wenye _______________ .

d. Watu wa ulimwengu wanapaswa kushikilia chochote kile ambacho, katika Siku hii, kinapelekea kwenye ____________________ wa ___________________ , yao, na _____________________ wa ______________ yao _________________ kabisa .

2. Ni zipi baadhi ya "fadhila bora kabisa" ambazo Mungu amejaalia juu ya jamii ya wanadamu katika Siku hii? _______________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

3. Maneno “kinapelekea kwenye” yana maana gani? ____________________________

____________________________________________________________

4. Orodhesha mambo yale ambayo unaweza kuendeleza maslahi bora kabisa ya jamii ya wanadamu: __________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Bahá’u’lláh anasema:

**“Hii ndiyo Siku ambamo Bahari kuu ya rehema ya Mungu imedhihirishwa kwa watu, Siku ile ambamo Nyota ya Mchana ya wema Wake wenye upendo imetawanya uangavu wake juu yao, Siku ile ambamo mawingu ya fadhila Yake yenye ukarimu imefunika wanadamu wote. Sasa ni wakati wa kuwachangamsha na kuwaburudisha wanyonge kwa upepo mwanana uhuishao wa upendo na urafiki, na maji ya uzima ya urafiki na hisani.”**[4]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Katika Siku hii, Bahari kuu ya _______________________ ya Mungu ime ___________________ kwa jamii ya wanadamu ___________________.

   b. Katika Siku hii, Nyota ya Siku ya _________________________ Wake ______________ ime _________________________ Wake juu ya jamii ya wanadamu.

c. Katika Siku hii, mawingu ________________________ yame ______________ binadamu wote.

d. ________________________ ni wakati ku ________________ na ______________ ____________________________ wanyonge kwa upepo mwanana uhuishao wa ___________________ na ________________________ , na maji ya uzima ya ____________________ na ___________________ .

2. Yapi kati ya yafuatayo huchangamsha na huburudisha watu?

_____ Kupata njia ya kujipatia elimu

_____ Kuwasaidia kujiongezea uwezo wa kushauriana

_____ Kutazamwa kwa huruma

_____ Kufaidi kutokana na maendeleo ya kisayansi

_____ Kushawishiwa kuunga mkono chama kimoja au kingine cha kisiasa au kundi

_____ Kusoma na kugawana pamoja na wengine Neno la Mungu

_____ Kushawishiwa kununua kwa mkopo vitu ambavyo hawahitaji

_____ Kuwa na utambuzi mkubwa zaidi wa umuhimu wa ibada

_____ Kutiwa moyo katika jitihada zao

_____ Kuwezeshwa kuwasilisha malalamiko kwa ufasaha kwa mamlaka ya serikali kupitia njia za kisheria

_____ Kushiriki katika maandamano ya kupinga

_____ Kunywa pombe kwa ajili ya kusahau matatizo yao

_____ Kupata manufaa ya utaratibu wa matunzo ya afya

_____ Kuwa na kilabu katika ujirani kama mahali pa kujiburudisha

_____ Kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu wa siku hii

_____ Kutegemea juu ya uwezo wa msaada mtakatifu

## SEHEMU YA 6

Bahá'u'lláh anasema:

**"Uzani wa ulimwengu umepinduliwa kupitia nguvu zinazotetema za Utaratibu huu mkuu kabisa na mpya wa Ulimwengu. Maisha ya wanadamu yaliyokuwa yana mpangilio yamepinduliwa kupitia nguvu za kipekee, za Mfumo huu wa ajabu — ambao mfano wake macho ya kiutu hayajapata kushuhudia.**

**"Jizamisheni wenyewe katika bahari kuu ya maneno Yangu, ili muweze kufumbua siri zake, na kugundua lulu zote za hekima ambazo zimefichwa ndani ya vina**

**vyake. Jihadharini msisitesite katika dhamira yenu kukubali ukweli wa Hoja hii – Hoja ambayo kupitia kwake nguvu zilizojificha za uwezo wa Mungu zimefunuliwa, na enzi Yake kusitawishwa."[5]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. ________________ wa ulimwengu ume _________________ kupitia _____________ zinazotetema za ___________________ huu mkuu kabisa, na _______________ .

   b. ________________________ ya wanadamu __________________________ yame ________________ , kupitia nguvu za __________________________ huu ____________________ , huu wa ajabu.

   c. Sharti _________________________ wenyewe katika __________________ ya maneno Yake, ili tuweze _________________________________ zake, na ______________________________ lulu zote za ______________________ ambazo zimefichwa ndani ya vina vyake.

   d. Sharti tusije _____________________________ katika _____________________ yetu ku _____________________ ukweli wa Hoja hii.

   e. Hii ni Hoja ambayo kupitia kwake _____________________ za ______________ wa Mungu ________________ , na _______________ Yake ________________ .

2. Nini maana ya neno "uzani"? _____________________________________________
______________________________________________________________________

3. Nini kimeharibu uzani wa ulimwengu? ______________________________________
______________________________________________________________________

4. Ni zipi baadhi ya ishara zinazoonyesha kwamba ulimwengu umepoteza uzani wake?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

5. Ni zipi baadhi ya ishara zinazoonyesha kwamba maisha ya jamii ya wanadamu yamepinduliwa? _________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

6. Ni nini huu "Mfumo wa ajabu" ambao Bahá'u'lláh anauongelea? ________________

7. Tunajizamishaje wenyewe katika bahari ya maneno ya Bahá'u'lláh? ____________

8. Fikira zetu zinaathiriwaje wakati tujizamishapo wenyewe katika bahari ya maneno Yake? ________________

9. Vitendo vyetu vinaathiriwa namna gani pale tunapojizamisha katika bahari ya maneno Yake? ________________

10. Tunapokea kutoka wapi nguvu zetu za kiroho zinazo hitajika kufanya kazi ya kusitawisha Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh? ________________

11. Nini maana ya neno ku "sitasita"? ________________

12. Nguvu zetu za kiroho huathiriwaje, kama tukisitasita katika kuukubali Ukweli wa Hoja Yake katika utimilifu wake? ________________

## SEHEMU YA 7

'Abdu'l-Bahá anatuhutubia kwa maneno haya:

**"Enyi wapendwa wa Bwana! Siku hii ni siku ya muungano, siku ya mkusanyiko wa wanadamu wote. 'Hakika Mungu huwapenda wale ambao, mithili ya ukuta imara, hupigania Hoja Yake katika safu zilizosimama bega kwa bega!' Angalia kwamba Yeye anasema 'katika safu zilizosimama bega kwa bega' — ikimaanisha kusimama kwa kubanana bila kuacha nafasi, kila mmoja akifungiwa kwa yule aliyemfuata, kila mmoja akimsaidia mwenzake.Kupigana, kama ilivyosemwa katika aya hiyo takatifu,katika kipindi kitakatifu hiki kikuu kuliko vyote, haimaanishi, kwenda mbele pamoja na upanga na mkuki, kwa fumo na mshale unaopenya — bali zaidi kwa silaha ya dhamira safi, kwa nia adilifu, kwa ushauri wenye msaada na unaofaa, kwa sifa za uchaji Mungu,kwa vitendo vimpendezavyo Mwenyezi,kwa sifa za mbinguni.Humaanisha elimu kwa wanadamu wote, uongozi kwa watu wote, uenezaji kila mahali harufu nzuri za roho,utangazaji wa mathibitisho ya Mungu,uelezaji wa hoja zenye kuthibitisha na tukufu, ufanyaji wa vitendo vya hisani."[6]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. 'Abdu'l-Bahá anatuambia kwamba siku hii ni siku ya ____________________ , siku ya ________________________ wa ________________________ wote.

   b. Yeye anaeleza kwamba Mungu ___________________________ wale ambao, mithili ya _______________________ , katika ________________________ hu _____________________ Hoja Yake.

   c. Kuwa "katika safu zilizosimama bega kwa bega", 'Abdu'l-Bahá anaelezea, maana yake ni ku _______________________ kwa __________________ , kila mmoja ________________ mwenzake.

   d. Kupigana katika huduma kwa Hoja katika _______________ hiki kikuu kuliko vyote, ___________________________ , Yeye hutuambia, haimaanishi kwenda mbele kwa _______________ na _______________ , kwa ______________ na _____________________ bali zaidi _________________________________ ya ______________________ , kwa _________________________________ , kwa _______________________ , kwa _______________________________ , kwa _____________________ , kwa _________________ .

   e. Kupigana katika kipindi kitakatifu hiki humaanisha ___________________ kwa wanadamu wote, ________________________________________ kwa watu wote, _____________________ kila mahali ______________________ , wa Mungu, _______________________ , _______________________ wa ______________ , ___________ wa ____________________________ .

2. Hii ndiyo siku ya muungano wa mbari wa wanadamu. Kuthamini jinsi gani kazi hii ilivyo kubwa, fikiria juu ya migawanyiko mbalimbali isiyohesabika ambayo kwayo binadamu wamejitenganisha wenyewe. Orodhesha migawanyiko mingi kadri uwezavyo.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

3. Nguvu gani inaweza kuwaunganisha watu wote hawa waliotengana? ______________

________________________________________

4. Ni ipi asili ya vita tunavyopigana? ______________________________

________________________________________

5. Weka alama mbele ya silaha zinazoweza kutumiwa katika vita hii:

| | |
|---|---|
| ______ Dhamira safi | ______ Hasira |
| ______ Sifa za ki-Mungu | ______ Ukarimu |
| ______ Nia nyoofu | ______ Nguvu ya sala |
| ______ Tamaa kuwa kiongozi | ______ Vitendo vinavyostahili sifa |
| ______ Ufidhuli na kiburi | ______ Upendo wa Mungu |
| ______ Shauku kwa ajili ya haki | ______ Upendo wa jamii ya wanadamu |
| ______ Kujiona mnyoofu | ______ Kumwamini Mungu |
| ______ Bunduki | ______ Ushauri unaosaidia na unaofaa |
| ______ Visu | ______ Nguvu ya umoja |

_____ Nguvu ya Neno la Mungu

_____ Kujiridhisha

_____ Kujikweza mwenyewe

_____ Fedha

_____ Imani

_____ Unyenyekevu

6. Je, ni sawa kujaribu kuwatawala wengine kwa ajili ya kuleta haki? _______________

7. Ni yapi kati ya haya yafuatayo yanayowakilisha mambo tunayofanya tunapokuwa katika vita vya kiroho kwa ajili ya kuunganisha jamii ya wanadamu?

_____ Kuendeleza elimu

_____ Kuwalazimisha wengine kufanya tunayoyataka

_____ Kufundisha Hoja ya Mungu

_____ Kutangaza Hoja ya Mungu

_____ Kugawanya katika makundi kufuatana na maslahi yetu wenyewe

_____ Kupigania maslahi ya kundi ulilomo

_____ Kufanya vitendo vya hisani

_____ Kuanzisha mjadala wenye mathibitisho kuhusu ukweli wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh

_____ Kujizamisha wenyewe katika bahari ya maneno Yake

_____ Kuwadhulumu wadhaifu na wanyonge

_____ Kusali kwa shauku

_____ Kupora mali za watu

_____ Kulimbikiza mali kwa kuiba kutoka kwa wengine

## SEHEMU YA 8

Utambuzi ulionolewa wa ukuu wa Siku hii huumba ndani yetu sote hamu ya kuinuka kufundisha, kuhudumu, na kufanya vitendo vyenye dhabihu. Ili kutokuweka kando haraka ambayo kwayo unalazimika kufanya vitendo vya utumishi kwa Hoja, kariri fungu lifuatalo kutoka barua iliyoandikwa na Mlinzi:

> **"Hakuna wakati wa kupoteza. Hakuna nafasi iliyoachwa ya kuyumba. Watu wengi mno wana njaa sana kwa ajili ya Mkate wa Uhai. Jukwaa limeandaliwa. Ahadi thabiti na isiyobadilika imetolewa. Mpango wa Mungu mwenyewe umeanzishwa. Unaongeza mwendo kila siku ipitayo. Nguvu za mbinguni na duniani kwa njia isiyoelezeka husaidia utekelezaji wake. Fursa kama hiyo haina mbadala.Mwache mwenye mashaka ainuke,na yeye mwenyewe athibitishe ukweli wa madai hayo. Kujaribu, kustahimili, ni kuhakikisha ushindi wa mwisho na kamili."**[7]

## MAREJEO


1. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983, 2017 kuchapisha), VII, aya. 1, uk. 10.

2. Kama hapo juu., VII, aya. 2, ku. 10–11.

3. Kama hapo juu., IV, aya. 1, uk. 5.

4. Kama hapo juu., V, aya. 1, uk. 6.

5. Kama hapo juu., LXX, aya. 1–2, uk. 154.

6. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2010, 2015 kuchapisha), na. 207.2, ku. 359–60.

7. Kutoka barua ya tarehe 28 Januari 1939, iliyochapishwa kwenye *Muda Makataa: Jumbe kutoka Shoghi Effendi kwa Wa Bahá'í wa Amerika ya Kaskazini, 1932–1946* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002), uk. 28.

# Maisha ya Báb

## Kusudi

Kupata utambuzi wa nguvu ya kipindi cha Utume mfupi na wa kusisimua wa Báb na kujifunza kusimulia hadithi ya maisha Yake

# SEHEMU YA 1

Kipindi Kitakatibu cha Báb kilianza mnamo mwaka 1844 na kilidumu kwa miaka tisa tu. Kusudi lake la msingi lilikuwa la kuandaa njia kwa ajili ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Ingawa muhula wa utume wa Báb ulikuwa mfupi, nguvu zilizoachiliwa na Ufunuo Wake zilikuwa kali mno kiasi kwamba athari yake itahisiwa kwa mamia ya vizazi vijavyo.

Báb, ambaye jina lake lilikuwa Siyyid 'Alí-Muḥammad, alizaliwa mnamo tarehe 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, jiji lililoko kusini mwa Iran, pia iliyojulikana kama Uajemi. Watu wengi kabisa huko Iran ni wa dhehebu la Uislam ambalo linasubiri kuja kwa Yule Mwahidiwa wa Mungu aitwaye Qá'im. Neno "Qá'im" maana yake ni "Yule atakayeinuka".

Báb alitoka kwenye familia mashuhuri ambayo ilikuwa ya nasaba ya Muḥammad, Mtume wa Uislam. Baba Yake alifariki wakati alipokuwa mtoto mdogo, na yeye alilelewa na mjomba wake. Ingawa Báb alijaliwa ujuzi wa kiasili na hakuhitaji kufunzwa na mtu yeyote, lakini Yeye alifuata mapenzi ya mjomba Wake ambaye alimpeleka shule alipokuwa akingali mwenye umri mdogo. Mwalimu Wake, walakini punde tu aliutambua uwezo mkubwa wa Báb na alitambua kwamba hakuwa na chochote cha kumfundisha mtoto huyo asiye wa kawaida. Yeye alisimulia hadithi ifuatayo kuhusu siku za shuleni za Báb:

> "Siku moja nilimuomba Báb kutongoa maneno ya mwanzo ya Kur'án . . . Yeye alisita, alimjibu kuwa, kama asingeambiwa maana ya maneno yale Yeye asingejaribu kuyatamka kwa sauti. Nilijifanya kutojua maana yao. 'Mimi najua maneno haya yana maana gani,' alitanabahi mwanafunzi wangu; 'kwa ruhusa yako, nitayaelezea.' Alizungumza kwa ujuzi mkubwa mno na ufasaha kwamba nilishikwa na mshangao. . . . Utamu wa matamshi yake bado umebakia katika kumbukumbu yangu. Nilijisikia nikisukumwa kumrudisha kwa mjomba wake na kuwasilisha mikononi mwake Dhamana ambayo alikuwa amenikabidhi mikononi mwangu. Nilidhamiria kumwambia jinsi nilivyojisikia, kuwa sikustahili kumfundisha mtoto asiye kuwa wa kawaida kama huyo. Nilimkuta mjomba Wake peke yake ofisini mwake. 'Nimemrudisha kwako,' nilisema, 'na ninamkabidhi katika ulinzi wako wenye uangalifu. Yeye siye wa kutendewa kama mtoto wa kawaida tu, kwani ndani Mwake tayari ninaweza kuona ushahidi wa ule uwezo usioelezeka ambao Ufunuo wa Qá'im peke yake unaweza kuufunua. Imekupasa umzungushie uangalizi wako wenye upendo mwingi kabisa. Mwache akae nyumbani mwako, kwa kuwa Yeye, hakika, hahitaji waalimu kama mimi.' Mjomba wake kwa ukali alimkemea Báb. 'Umesahau maagizo yangu?' alisema. 'Kwani sijakuonya kufuata mfano wa wanafunzi Wenzako, kuwa kimya, na kusikiliza kwa uangalifu kila neno analolisema mwalimu wako?' Baada ya kupata ahadi Yake ya kutii kwa uaminifu maagizo yake, mjomba alimwambia Báb arudi shuleni Kwake. Lakini, roho ya mtoto yule haikuweza kuzuiliwa na maonyo makali ya mjomba Wake. Hakuna nidhamu ambayo ingeweza kuzuia mtiririko wa ujuzi Wake wa kiasili. Siku hadi siku aliendelea kudhihirisha mathibitisho ya ajabu mno ya hekima ambayo ilipita ile ya watu wa kawaida, kiasi kwamba sina uwezo wa kusimulia."[1]

Hatimaye mjomba wake Báb aliamua kumruhusu kuacha shule. Ndipo alipoanza kufanya kazi na mjomba Wake kama mfanya biashara huko Búshihr, mji ulioko kusini magharibi mwa Shíráz. Ilikuwa katika kipindi hicho ambapo Báb alioa, Yeye na mkewe walijaliwa mtoto wa kiume aliyeitwa Aḥmad, ambaye alifariki akiwa mchanga mwaka mmoja kabla Báb hajajitangaza Mwenyewe kuwa Qá'im Aliyeahidiwa.

Katika ujana Wake, Báb alionesha dalili za uwezo na ukuu ambao hakuna mtu angeweza kuushinda. Sifa zisizokuwa za kawaida ambazo zingemwainisha Yeye katika kipindi chote cha Utume Wake, cha kasi na chenye huzuni, tayari zilikuwa zimedhihirika. Mlinzi anamwongelea Yeye kama "nafsi yenye upole, ujana na isiyozuilika ya Báb, bila kifani katika unyenyekevu Wake, asiye na wasiwasi katika utulivu Wake, mwenye mvuto wa sumaku katika matamshi Yake". Sehemu zinazofuata zitaweza kuelezea bila kutosheleza matukio ya maisha Yake. Lakini hata maelezo haya mafupi yatawasha mioyoni mwetu cheche kutoka moto wa upendo ambao Yeye aliuwasha katika mioyo ya maelfu na maelfu huko Uajemi na mbele zaidi.

1. Jina la Báb lilikuwa lipi? ____________________________________________

2. Báb alizaliwa wapi na mnamo tarehe gani? ______________________________

   ________________________________________________________________

3. Je, wadhifa huu wa "Qá'im" una maana gani? _____________________________

4. Familia ya Báb ilitokea kiasili katika ya nasaba ya nani? ____________________

   ________________________________________________________________

5. Ni nani aliyewajibika kumlea Báb baada ya kufariki Baba yake? _____________

   ________________________________________________________________

6. Je, ni nini maana ya msamiati kwamba Báb alijaliwa na Mungu ujuzi wa kiasili au wa kuzaliwa? ____________________________________________________

   ________________________________________________________________

7. Je, yule mwalimu wa Báb alifikiri nini alipoutambua uwezo Wake mkuu? ________

   ________________________________________________________________

8. Fungu hili la maneno "hekima ambayo ilipita ile ya watu wa kawaida" lina maana gani?

   ________________________________________________________________

9. Báb alifanya nini baada ya kuacha shule? _______________________________

   ________________________________________________________________

10. Ni kwa maneno gani Mlinzi anamwelezea Báb? ___________________________

    ________________________________________________________________

    ________________________________________________________________

    ________________________________________________________________

11. Andika kwa maneno yako mwenyewe hadithi ya siku za shuleni za Báb, kama ilivyoelezwa na mwalimu Wake.

## SEHEMU YA 2

Kabla Báb hajatangaza Dhima Yake, watu kadhaa kote ulimwenguni walijua ndani kabisa ya mioyo yao kuwa Siku mpya ilikuwa karibu ichomoze. Miongoni mwao alikuwa mtu mmoja mtakatifu Siyyid Káẓim ambaye aliishi katika mji wa Karbilá nchini ‘Iráq. Siyyid Káẓim, alikuwa ana wanafunzi wake wengi, na alitumia maisha yake kuwaandaa kwa ajili ya ujio wa Qá’im aliyekuwa amesubiriwa sana kwa muda mrefu. Yeye aliwaambia mara kwa mara kuwa baada ya kifo chake, ingewabidi kuondoka majumbani mwao kwa mioyo iliyotakasika kutoka tamaa zote za ulimwenguni, waondoke kwenda kumtafuta yule mwahidiwa Mpendwa.

Baada ya Siyyid Káẓim kufariki, mwanafunzi wake mwenye kuheshimika, Mullá Ḥusayn, alisali na kutafakari, kwa kipindi cha siku arobaini; katika kipindi hicho aliufungua moyo wake wazi kupata upuzio wa Mungu. Ndipo, alipoondoka ‘Iráq pamoja na wenzake wawili kwa ajili ya kumtafuta Yule Mwahidiwa. Kwanza alikwenda Bú<u>sh</u>ihr. Huko hakukaa siku nyingi hata hivyo, kwani alihisi mvuto usiozuilika ukitokea mwelekeo wa kaskazini katika mji wa <u>Sh</u>íráz. Alipofika kwenye mji huo, yeye aliwaambia wenzake watangulie kwenda msikitini na wamsubiri huko, naye angewakuta huko.

Saa chache kabla ya jua kutua, nje kidogo ya lango la mji wa <u>Sh</u>íráz, alikutana na kijana Mmoja mashuhuri Ambaye alimkaribisha na kumwalika nyumbani kujiburudisha baada ya safari ndefu na ngumu. Mullá Ḥusayn alivutiwa sana na mwenendo ambao ulikuwa wenye upole lakini thabiti, wa Kijana huyu asiyekuwa wa kawaida, alipoongea. Yeye alimfuata, na punde tu walifika kwenye mlango wa nyumba moja ya kawaida. Waliingia ndani na walienda

moja kwa moja kukaa kwenye chumba cha juu. Mwenyeji wake mkarimu aliagiza liletwe jagi la maji ili mgeni Wake anawe mavumbi ya safari. Halafu Yeye Mwenyewe alitengeneza chai na kumkaribisha Mullá Ḥusayn Yeye mwenyewe. Baada ya vitendo hivi vya ukarimu, Yeye alianza kuongea. Tondoti za maongezi hayo ya kihistoria yalielezwa baadaye na Mullá Ḥusayn:

> "Ilikuwa imepita takriban saa moja baada ya jua kutua, ndipo Mwenyeji wangu kijana alipoanza kuongea nami. 'Nani baada ya Siyyid Káẓim', Yeye Aliniuliza, 'amekuwa mrithi wake na kiongozi wako?' 'Wakati wa kifo chake,' mimi nilimjibu 'yeye kwa msisitizo alitusihi kuacha makaazi yetu, na kusambaa kwa mapana na marefu m kumtafuta Mpendwa Mwahidiwa. Na mimi kufuatana na maagizo hayo, nimekuja Uajemi na nimeinuka kukamilisha mapenzi yake, na ningali namtafuta.' 'Je, mwalimu wenu,' Yeye aliendelea kuuliza, 'aliwapa maelezo yoyote ya kina kuhusu alama bainifu za kumtambulisha Yule Mwahidiwa?' 'Naam,' nilijibu, 'Yeye anatoka katika nasaba safi, wa ukoo maarufu, na wa uzao wa Fáṭimih. Juu ya rika Lake, Yeye ana umri unaozidi miaka ishirini na chini ya miaka 30. Yeye amejaliwa na ujuzi wa kiasili wa kuzaliwa. Yeye ana kimo cha wastani, havuti tumbaku, na hana dosari katika mwili.' Yeye alisita kidogo na halafu kwa sauti yenye mtetemo alitamka: 'Tazama, dalili zote hizi zinadhihirika Kwangu!' Halafu alifikiria kila moja ya dalili zilizotajwa hapo juu, na alionyesha kwa uthibitisho kwamba kila moja na zote zilikuwemo kwenye nafsi Yake."[2]

Jioni ile, Báb alimthibitishia Mullá Ḥusayn, kwa ushahidi ulio wazi na dhahiri, kwamba Yeye alikuwa Yule Mwahidiwa Qá'im. Yeye alifunua, kwa wepesi wa kushangaza, sehemu ya kwanza ya fasiri yake juu ya Súra ya Yusufu, sura muhimu ya Kurani. Yeye ndipo alipomwambia Mullá Ḥusayn maneno haya:

> "Ewe ambaye ni wa kwanza kuniamini Mimi! Hakika nasema, mimi ni Báb, Lango la Mungu, na wewe u Bábu'l-Báb, lango la Lango hilo. Roho kumi na nane lazima, hapo mwanzoni, wao wenyewe na kwa hiari yao wenyewe, wanikubali na watambue ukweli wa Ufunuo Wangu. Bila kuonywa na bila kualikwa, kila mmoja wao lazima atafute kwa uhuru kuniona Mimi.Na idadi yao itakapokamilika, mmoja wao lazima achaguliwe kufuatana Nami katika hija yangu huko Makka na Madina. Huko nitawasilisha Ujumbe wa Mungu kwa <u>Sh</u>aríf wa Makka. Halafu nitarudi Kúfih, ambako tena ndani ya msikiti wa mji huu mtakatifu, nitadhihirisha Hoja Yake. Inakubidi usifumbue, ama kwa wenzi wako au kwa roho yeyote ile nyingine, kile ambacho umekiona na kukisikia."[3]

Ufunuo huu mtukufu uliijaza roho ya Mullá Ḥusayn kwa msisimko na shangwe, kwa kicho na mshangao. "Nilijihisije dhaifu na asiye na nguvu, aliyekata tamaa na mwoga, kama nilivyojihisi hapo mwanzoni!" baadaye alisema. "Wakati huo sikuwa na uwezo wa kuandika wala kutembea, kwa jinsi ilivyotetemeka sana mikono yangu na miguu. Sasa, walakini, ujuzi wa Ufunuo Wake umeamsha nafsi yangu. Nilijisikia mwenye ujasiri mno na uwezo kiasi kwamba kama ulimwengu, watu wake wote na watawala wake, wangeinuka dhidi yangu, mimi, pekee na pasipo hofu, ningehimili mashambulio yao. Ulimwengu ulikuwa kama konzi ya vumbi tu mkononi mwangu. Nilikuwa kama Sauti ya nafsi ya Gabriel, nikiwaita wanadamu wote: 'Amkeni, kwani, tazama! Mwanga wa asubuhi umechomoza. Inukeni, kwani, Hoja Yake imedhihirishwa. Mlango wa neema yake umefunguliwa wazi kabisa; ingieni humo, Enyi watu wa ulimwengu! Kwani Yule Ambaye ni Mwahidiwa wenu Amekuja!'"[4]

Tangazo la Báb lilifanyika mnamo jioni ya kuamkia tarehe 23 Mei 1844. Yeye Alikuwa mwenye umri wa miaka ishirini na tano. Miongo mingi baadaye katika siku ya kumbukumbu ya Tangazo la Báb, 'Abdu'l-Bahá alikihutubia kikundi cha waumini katika maneno yafuatayo:

> **"Hii ni tarehe 23 Mei, siku ya kuadhimisha ujumbe na Tangazo la Báb. Ni siku iliyobarikiwa na alfajiri ya udhihirisho, kwani kutokea kwa Báb ulikuwa mwanga wa mapema wa asubuhi ya kweli, . . . ni siku iliyobarikiwa, mwanzo wa fadhila za mbinguni, mwanzo wa mng'ao mtakatifu. Mnamo siku hii mwaka 1844 Báb alitumwa kupia mbiu na kutangaza Ufalme wa Mungu, akitangaza habari za furaha za ujio wa Bahá'u'lláh na kuhimili upinzani wa taifa zima la Uajemi."**[5]

1. Siyyid Káẓim aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini yeye atakapokufa? ________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

2. Mullá Ḥusayn alifanya nini baada ya kufariki kwa Siyyid Káẓim? ________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

3. Jinsi gani Báb alijua kwamba Mullá Ḥusayn amewasili <u>Sh</u>íráz? __________________

   ____________________________________________________________

4. Ni maswali gani Báb alimuuliza Mullá Ḥusayn baada ya kufika nyumbani Kwake?

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

5. Ni maelezo gani Siyyid Káẓim alikuwa amewapa wanafunzi wake ya ambayo yangewawezesha kumtambua yule Qá'im?

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

6. Fáṭimih ni mtoto wa kike wa nani, na ina maana gani kusema “kuwa wa nasaba yake”?

_______________________________________________

_______________________________________________

7. Je, Báb alikuwa na sifa zile ambazo Mullá Ḥusayn alikuwa akizitafuta? __________

_______________________________________________

8. Je, wadhifa wa “Báb” una maana gani? ______________________

_______________________________________________

9. Je, Báb alimpa wadhifa gani Mullá Ḥusayn? ______________________

_______________________________________________

10. Je, wadhifa huu una maana gani? ______________________

_______________________________________________

11. Ni jambo gani Báb alimwambia Mullá Ḥusayn kuwa lazima litokee kwanza, ndipo yenye angeweza kuitangaza Hoja Yake? ______________________

_______________________________________________

_______________________________________________

12. Eleza katika maneno yako mwenyewe kile alichokisema Mullá Ḥusayn kuhusu usiku huo wa kukumbukwa ambapo yeye alikuja kumtambua Qá’im mwahidiwa.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

13. Tangazo la Báb lilitfanyika lini? ______________________

_______________________________________________

14. Báb alikuwa ana umri gani wakati wa Tangazo Lake? ________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 3

Baada ya Mullá Ḥusayn, watu wengine kumi na saba walimtafuta na kila mtu peke yake alimpata yule ambaye alikuwa Haja ya Moyo wake. Kila mmoja aliongozwa na Mungu kutambua ukweli wa Ufunuo mpya, baadhi kupitia njozi au ndoto, baadhi kupitia ibada na wengine kupitia nyakati za tafakari. Wote isipokuwa mmoja miongoni mwa roho hizi zilizo barikiwa waliweza kuonana na Báb mjini Shíráz. Yule ambaye hakuonana Naye alikuwa ni mwanamke wa kipekee na mshairi mahiri aliyeitwa Ṭáhirih. Yeye alijua Báb kupitia ndoto, alimtambua kama Qa'im Mwahidiwa na akawa mtetezi hodari wa Hoja Yake. Mtu wa kumi na nane aliyejiunga kwenye safu ya wafuasi Wake, alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini na mbili aliyeitwa Quddús. Ingawa alikuwa akingali kijana, Quddús alikuwa na tabia nzuri ya kuigwa, na ujasiri na imani ambavyo wachache wangeweza kulinganishwa naye. Waumini hawa wa kwanza, pamoja na Mullá Ḥusayn, Báb aliwaita "Herufi za Waliohai" kumi na nane.

Mara baada ya idadi ya Herufi za Waliohai kukamilika, Báb alimuita Mullá Ḥusayn kuja mbele Yake na alimpa maagizo yafuatayo: "Siku zetu za kuwa pamoja zinakaribia mwisho. Agano Langu na wewe hivi sasa limetimizwa. Jifunge kibwebwe cha jitihada, na inuka kueneza Hoja Yangu. Usife moyo kwa kuona uharibifu na upotofu wa kizazi hiki, kwa kuwa Bwana wa Agano kwa hakika atakusaidia. Kwa ukweli, atakuzungushia ulinzi Wake wenye upendo, na atakuongoza kutoka ushindi hadi ushindi. Mithili ya wingu linalonyesha baraka zake juu ya ardhi, pita juu ya nchi hii kutoka mwisho hadi mwisho, na wamiminie watu wake baraka ambazo Mwenyezi, katika rehema Yake, ameridhia kukujaalia. . . . Katika hija hii ambayo tutaianza hivi punde, tumemchagua Quddús kama mwenzi Wetu. Tumekuacha nyuma kukabiliana na mashambulio ya adui mkali na asiyechoka. Walakini, uwe na hakika kwamba, fadhila tukufu mno isiyosemeka itajaliwa juu yako. Fuata njia ya safari yako kuelekea kaskazini, na njiani mwako tembelea miji ya Iṣfáhán, Káshán, Qum, na Ṭihrán. Msihi Mwenyezi Mjalia kwamba akuwezeshe kwa neema kufikia, katika mji huo mkuu, kiti cha enzi ya kweli, na kuingia katika jumba la yule Mpendwa. Siri imefichwa ndani ya mji huo. Itakapodhihirishwa, itageuza dunia hii kuwa paradiso. Tumaini langu ni kwamba utaweza kushiriki katika neema yake na kuutambua utukufu wake." [6]

Baada ya kumpa maagizo Mullá Ḥusayn ya kwenda Ṭihrán, Báb aliwaita kwake wale Herufi za Waliohai wengine na kumgawia kila mmoja kazi maalum. Katika maneno ya kuagana nao, aliwasihi kuweka kando kila tamaa ya kidunia na kutawanyika kwa marefu na mapana kutangaza Hoja Yake. Yeye aliwaambia maneno haya:

> **"Enyi rafiki zangu wapendwa! Ninyi ni wachukuzi wa jina la Mungu katika Siku hii Mmechaguliwa kama ghala za siri Yake.Imempasa kila mmoja wenu kudhihirisha sifa za Mungu, na kuonesha kwa mfano wa vitedo vyenu na maneno yenu zile ishara za wema Wake, nguvu Zake na utukufu. Viungo vyenyewe vya miili yenu lazima vishuhudie ubora wa kusudi lenu, ukamilifu wa maisha yenu, uhalisia wa imani yenu, na tabia iliyotukuka ya ibada yenu. Kwani, kwa kweli ninasema, hii ni Siku iliyosemwa na Mungu katika Kitabu Chake: 'Siku hiyo ndipo Sisi tutaweka kizibo juu ya midomo yao; walakini mikono yao itaongea na Sisi, na miguu yao itashuhudia juu ya kile ambacho wao watakuwa wamefanya.'**

**Tafakarini juu ya maneno ya Yesu aliyowaambia wanafunzi Wake, alipokuwa anawatuma kwenda kusambaza Hoja ya Mungu. Kwa maneno kama haya, Yeye aliwaambia kuinuka na kutimiza dhima yao: 'Ninyi ni kama moto ambao katika giza la usiku umewashwa juu ya kilele cha mlima. Acheni mwangaza wenu uwake mbele ya macho ya watu. Usafi wa tabia yenu na kiwango cha kujikana kwenu vinapaswa kuwa wa aina ambayo vitawafanya watu wa dunia kupitia kwenu watambue na kuvutiwa karibu zaidi kwa Baba wa mbinguni ambaye ni Chanzo cha utakaso na neema. Kwa kuwa hakuna aliyemuona Baba aliye mbinguni. Ninyi ambao ni watoto Wake wa kiroho, kupitia vitendo vyenu lazima muoneshe mfano wa njema Zake, na mshuhudie utukufu Wake. Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini kama chumvi imepoteza ladha yake, itawezaje kuwekewa ladha ya chumvi? Kujitenga kwenu kunapaswa kuwa kwa kiwango ambacho, wakati wowote muingiapo katika mji wowote kwa ajili ya kutangaza na kufundisha Hoja ya Mungu, ninyi hampaswi kupokea ama nyama au zawadi kutoka watu wake. La hasha, mtakapoondoka kutoka mji huo, kunguteni vumbi kutoka miguu yenu. Kama mlivyoingia wasafi na bila ya najisi, ndivyo mnavyopaswa kuondoka kutoka mji huo. Kwa kweli ninasema, Baba wa mbinguni yu nanyi daima na anawalindeni. Ikiwa mtakuwa waaminifu Kwake, Yeye kwa uhakika atawapa katika mikono yenu hazina zote za dunia, na atawatukuza juu ya watawala na wafalme wa ulimwengu.' Enyi Herufi Zangu! Kweli ninasema, Siku hii imetukuka sana, juu ya siku za Mitume wa kale. La hasha, tofauti haipimiki! Ninyi ni mashahidi wa Alfajiri ya Siku iliyoahidiwa ya Mungu. Ninyi ni washiriki wa kalisi ya ghaibu ya Ufunuo Wake. Funga kibwebwe cha juhudi, na jalini maneno ya Mungu kama ilivyofunuliwa katika Kitabu Chake: 'Naam, Bwana Mungu wako amekuja, na pamoja na Naye kipo kikosi cha malaika Wake wakiwa wamejiandaa mbele Yake!' Safisheni mioyo yenu kutokana na tamaa za kidunia, na acheni sifa za kimalaika ziwe pambo lenu. Jitahidini ili kupitia vitendo vyenu muweze kuwa mashahidi kwa ukweli wa maneno haya ya Mungu, na mtambue kwamba isijetokea kuwa kwa 'kugeukia nyuma', Yeye ataweza 'kuwabadilisheni kwa ajili ya watu wengine,' ambao 'hawatakuwa kama ninyi,' na ambao watachukua kutoka kwenu Ufalme wa Mungu. Siku ambapo ibada tupu ilikuwa inaonekana kuwa inatosha, sasa zimekwisha. Wakati umekuja ambapo hakuna chochote ila nia safi kabisa, ikiwa yenye uhimili wa vitendo vya utakaso usio na mawaa, inaweza kupanda hadi kwenye kiti cha enzi cha Yule Aliye Juu kabisa na kukubaliwa Naye. 'Neno zuri huinuka ndani mwao kwenda Kwake, na tendo nyoofu litawasababisha kutukuka mbele Yake.' Ninyi ni duni, ambao Mungu amewaongelea katika Kitabu Chake: 'Na Sisi tunatamani kuwaonesha fadhila wale ambao walidhalilishwa nchini, na kuwafanya viongozi wa kiroho miongoni mwa watu, na kuwafanya warithi Wetu.' Ninyi mmeitwa kwa daraja hili; ninyi mtalifikia, ikiwa tu mtainuka kukanyaga chini ya miguu yenu kila tamaa ya kidunia, na kujitahidi kuwa wale 'watumishi Wake waheshimiwa ambao hawaongei isipokuwa Yeye ameongea kwanza, na wanaofuata amri Yake.' Ninyi ni Herufi za kwanza mliozaliwa kutoka kwa Nukta ya Kwanza, Chemchemi za kwanza zilizoibuka kutoka Chanzo cha Ufunuo huu. Msihini Bwana Mungu wenu kuwajaalia kuwa isije misukosuko ya kidunia, wala mapenzi ya kidunia, au shughuli za mpito, ambazo zitachafua utakaso, au kutia uchungu katika utamu, wa ile neema inayotiririka kupitia kwenu. Mimi ninawaandaeni kwa ajili ya ujio wa Siku yenye nguvu. Fanyeni juhudi zote kadiri muwezavyo, kwamba, katika ulimwengu ujao, Mimi ambaye sasa ninawapa maagizo, pengine niweze mbele ya kiti cha rehema cha Mungu, kufurahia katika vitendo vyenu na kutukuka katika**

**mafanikio yenu.Siri ya Siku ambayo inatarajiwa kuja sasa imefichwa.Siri haiwezi kufichuliwa wala kukadiriwa.Mtoto aliyezaliwa wa Siku hiyo anawapita watu wenye hekima na wanaoheshimika kabisa wa wakati huu, na watu duni kabisa na ambao hawana elimu kabisa wa wakati huo watawapita katika uelewa makasisi waliosoma sana na hodari wa zama hizi. Sambaeni kupitia marefu na mapana katika nchi hii, na, kwa miguu thabiti na mioyo mitakatifu, andaeni njia ya ujio Wake. Msiangalie unyonge wenu na udhaifu; kazieni macho yenu juu ya nguvu isiyoshindika ya Bwana wenu, Mungu wenu, Mwenyezi. Kwani katika siku zilizopita, hakumfanya Abraham, licha ya kuonekana asiyejiweza ayashinde majeshi ya Nimrodi? Hakumwezesha Musa, ambaye fimbo Yake ilikuwa mwenzi Wake pekee, kumshinda Farao na majeshi yake? Hakusitawisha ushindi wa Yesu, ambaye alikuwa masikini na duni katika macho ya watu, juu ya muungano wa majeshi ya Wayahudi? Hakuyafanya makabila ya washenzi na wagomvi ya Arabuni yakubali nidhamu takatifu na inayobadilisha ya Muḥammad, Mtume Wake? Inukeni katika jina Lake, wekeni imani yenu kabisa Kwake, na muwe na uhakika juu ya ushindi wa mwisho.”[7]**

1. Ni wadhifa gani Báb aliwapa waumini wa kwanza ambao walimtambua Yeye kama Qá’im mwahidiwa? ______________________________________________

______________________________________________________________

2. Je, walikuwepo Herufi za Waliohai wangapi? ____________________________

______________________________________________________________

3. Nani alikuwa wa kwanza kumtambua Báb?____________________________

______________________________________________________________

4. Nani alikuwa Herufi ya Waliohai wa mwisho? ___________________________

______________________________________________________________

5. Jinsi gani Herufi za Waliohai waliongozwa kuutambua ukweli wa Ufunuo wa Báb?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

6. Ni yupi miongoni mwa Herufi za Waliohai hakuwahi kufika mbele ya uwepo wa Báb?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

7. Mara baada ya idadi ya Herufi za Waliohai ilipokamilika, Báb alimwita Mullá Ḥusayn kuja mbele yake na alimpa maagizo yafuatayo: “Siku zetu za _____________ pamoja zina ___________________________ . __________________ Langu na nawe hivi sasa _______________ . Jifunge ______________ cha jitihada, na ______________

kueneza Hoja Yangu. Usife ________________ kwa kuona ________________ na ________________ wa ________________ hiki, kwa kuwa ________________ wa ______________ kwa hakika ______________. Kwa ukweli, ____________________ ulinzi Wake wenye upendo, na atakuongoza kutoka ______________ hadi ______________. Mithili ya ______________ linalonyesha baraka zake juu ya ardhi, ____________________ ya nchi hii kutoka mwisho hadi mwisho, na ______________ watu wake baraka ambazo ______________, katika ______________ Yake, ______________ kukujaalia."

8. Báb alimchagua nani amsindikize kwenda kuhiji? ____________________________

______________________________________________________________________

9. Alimwagiza Mullá Ḥusayn aende wapi? ____________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

10. Alitumaini nini kwa ajili ya Mullá Ḥusayn? ________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

11. Pengine mgependa kukariri angalau sehemu ya hotuba ya Báb kwa Herufi za Waliohai.

## SEHEMU YA 4

Mnamo mwezi Oktoba 1844 Báb, akiandamana na Quddús, alianza safari ya hija Yake kwenda Makka na Madina.Miji hii miwili, iliyoko nchini Saudi Arabia, ni mitakatifu kwa wafuasi wa Uislamu. Báb na mwenzake waliingia chomboni hapo Búshihr, ambacho kiliwapeleka kuzungukia Rasi ya Uarabuni, na kufika jirani na Makka baada ya takriban miezi miwili. Walipokuwa wakingali Makka, Báb aliandika barua kwa Sharíf, mkuu wa mji na mlinzi wa lake kaburi takatifu. Katika barua hiyo, Yeye Alieleza wazi Dhima Yake na alimwalika Sharíf kuikubali Hoja Yake. Lakini Sharíf, ambaye alikuwa akishughulika na mambo yake mengine, alishindwa kuujibu Ujumbe wa mtakatifu. Halafu Bab alisafiri pamoja na Quddús kutoka Makka hadi Madina, ambako mabaki ya kimwili ya Mtume Muḥammad yamezikwa. Baada ya kuutembelea mji huo mtakatifu, walirudi Uajemi kwa meli. Walishuka Búshihr, na Báb alimwagiza Quddús kwenda Shíráz:

> "Siku zetu za kuwa pamoja Nami zinakaribia mwisho. Saa ya utengano imewadia, utengano ambao hakuna muungano tena utakaofuata isipokuwa katika Ufalme wa Mungu . . . Katika mitaa ya Shíráz, utalundikiwa ufidhuli, na majeraha makali kabisa yatautesa mwili wako. Utaendelea kuishi baada ya vitendo vya kufedhehesha vya maadui wako, na utafika mbele ya Yule ambaye ndiye shabaha pekee ya ibada yetu na upendo. Mbele Yake utasahau madhara yote na fedheha ambavyo vitakuwa

vimekupata. Majeshi ya Asiyeonekana yataharakia mbele kukusaidia, na yatautangazia ulimwengu wote ushujaa wako na utukufu. Yako itakuwa ni furaha isiyoelezeka ya kugugumiza kikombe cha kifo cha kishahidi kwa ajili Yake. Mimi, pia, nitakanyaga njia ya kujitoa dhabihu, na nitaungana nawe katika milki ya umilele."[8]

1. Báb aliondoka lini kwenda kufanya hija Yake? ______________________________

______________________________________________________________________

2. Báb alitembelea miji ipi wakati wa hija Yake? ______________________________

______________________________________________________________________

3. Alimwandikia nani huko Makka? ________________________________________

______________________________________________________________________

4. Kwa nini Madina ni mji mtakatifu kwa Waislamu? ____________________________

______________________________________________________________________

5. Katika nafasi iliyopo hapo chini kwa maneno yako mwenyewe, andika maneno ambayo Báb alimwambia Quddús walipofika Bú<u>sh</u>ihr.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

6. Báb alimwahidi Quddús kuwa angekutana na nani? ___________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Katika mji wa Shíráz Quddús alianza kufundisha Ujumbe wa Báb kwa bidii kubwa. Lakini punde tu alikabiliwa na upinzani kutoka makasisi wa Kiislamu na gavana wa jimbo aliyeamuru Quddús akamatwe pamoja na wenzake wawili. Gavana huyo ambaye alikuwa mtu katili na muovu, aliamuru wateswe hadharani. Ndevu zao zilichomwa, na pua zao zilitobolewa na kamba ilipitishwa humo, na katika hali hii ya aibu, walivutwa kwa kamba hiyo na kutembezwa katika mitaa. "Litakuwa funzo kwa watu wa Shíráz," hiyo ilikuwa amri ya gavana, "ambao watajua ni ipi itakuwa adhabu ya uzushi wa kidini."[9] Baada ya kupitia fedheha hii, Quddús na wenziwe walifukuzwa kutoka katika mji huo, wakionywa kuwa wangeuawa kama wangejaribu kurudi. Hivyo ndivyo roho hizi shujaa zilijipatia heshima wa kuwa wa kwanza kuteswa huko Uajemi kwa ajili ya Imani yao mpya. 'Abdu'l-Bahá amewaongelea maelfu ambao baadaye waliteswa katika njia ya Mpendwa wao, Báb, katika maneno haya:

> **". . . walipata shida za kutisha na majaribu makali. Walistahimili majaribu kwa uwezo wa ajabu na kwa ushujaa mkuu. Maelfu walitupwa gerezani, waliadhibiwa, waliteswa na kuuawa kama mashahidi. Kaya zao ziliporwa na kuharibiwa, mali zao zilikamatwa. Wao walitoa dhabihu maisha yao kwa hiari na kubakia bila kutikisika katika imani yao hadi mwisho kabisa. Roho hizo za ajabu ni taa za Mungu, Nyota za utakatifu zinazong'aa kwa utukufu kutoka upeo wa milele wa mapenzi ya Mungu."[10]**

Baada ya kuamuru adhabu ya udhalimu mkubwa kama huo kutolewa kwa Quddús na wenzi wake, gavana huyo aligeuzia hasira zake kumuelekea Báb. Aliwatuma askari wake wa farasi kwenda hadi Búshihr kwa maagizo ya kumkamata na kumleta akiwa amefungwa minyororo hadi Shíráz. Wakati ule ule, Báb alikuwa amekwisha ondoka Búshihr kuelekea Shíráz. Kikundi hiki cha walinzi wapanda farasi kilikutana Naye katika pori lililokuwa kati ya miji hii miwili. Baadaye kabisa, kiongozi wa kikundi hicho alisimulia hadithi ya kukutana kwao:

> "Tulipomkaribia Báb, Yeye alitusalimu na alituuliza tulikuwa tukienda wapi. Nilifikiri ni bora kabisa kumficha ukweli, na nilijibu kwamba katika ujirani huu tumeamriwa na gavana kufanya uchunguzi fulani. Yeye alisema kwa kutabasamu: 'Gavana amewatuma kunikamata Mimi. Niko hapa; nifanyieni kama mnavyotaka. Kwa kuja kukutana nanyi, nimefupisha urefu wa mwendo wenu, na nimewarahisishia kunipata Mimi.' Nilishituliwa na maneno yake na nilishangazwa na uwazi Wake na unyofu. Sikuweza kuelezea, walakini, utayari Wake wa kujileta mwenyewe, kwa hiari Yake mwenyewe kwenye adhabu kali za maafisa wa serikali, na hivyo kuhatarisha maisha yake mwenyewe na usalama. Nilijaribu kupuuzia alichokisema, na nilikuwa najitayarisha kuondoka, ndipo aliponisogelea na kusema: 'Naapa kwa uadilifu wa Yule ambaye alimuumba mtu, akamtofautisha kutoka miongoni mwa viumbe Vyake wengine, na kuufanya moyo wake kuwa kiti cha mamlaka Yake na ujuzi, kwamba maisha Yangu yote sijawahi kutamka neno lolote isipokuwa ukweli, na sikuwa na tamaa nyingine isipokuwa usitawi na maendeleo ya wanadamu Wenzangu. Nimepuuzia raha Yangu mwenyewe na nimeepuka kuwa chanzo cha maumivu au huzuni kwa mtu yeyote. Ninafahamu kwamba mnanitafuta Mimi. Napendelea kujisalimisha Mwenyewe mikononi mwenu, kuliko kukupa wewe na wenzi wako usumbufu usio wa lazima kwa ajili Yangu.' Maneno haya yalinigusa kwa undani sana. Bila kufikiri nilishuka kutoka kwenye farasi wangu, na, nikibusu vikuku vyake, nilimwambia maneno haya: 'Ewe mwanga wa macho ya Mtume wa Mungu! Nakusihi,

kwa Yule ambaye amekuumba na kukujalia ukuu kama huo na uwezo, ukubali ombi langu na kujibu sala yangu. Nakusihi utoroke kutoka mahali hapa na kukimbia kutoka kwa gavana huyu katili na duni wa jimbo hili. Naogopa njama zake dhidi Yako; ninagoma kwa wazo la kufanywa chombo cha mipango miovu yake dhidi ya uzao wa Mtume wa Mungu ambaye ni muungwana asiye na hatia . . .' Kwa maombi yangu ya dhati Yeye alitoa jibu hili: 'Ninakuombea kuwa Bwana, Mungu wako akulipe kwa moyo wako mkuu na ukarimu wako mkuu na nia njema. Hakuna mtu ajuaye fumbo la Hoja Yangu, hakuna awezaje kuelewa siri zake. Asilani siwezi kugeuzia mbali uso Wangu kutoka kwa amri ya Mungu. Yeye peke Yake ndiye ng'ome Yangu ya uhakika, Mhimili Wangu, Kimbilio Langu. Hadi saa Yangu ya mwisho itakapowadia, hakuna awezaye kunishambulia Mimi, hakuna awezaye kuvuruga mipango ya Mwenyezi. Saa Yangu itakapowadia, furaha yangu itakuwa kubwa vilivyoje kugugumiza kikombe cha ushuhuda katika jina Lake! Mimi nipo hapa; nifikishe katika mikono ya bwana wako. Usiogope, kwani hakuna atakaye kulaumu.' Niliinama kuashiria idhini yangu na kutekeleza haja yake."[11]

Báb papo hapo aliendelea na safari Yake ya kwenda Shíráz. Akiwa huru na bila minyororo, Yeye alikwenda mbele ya walinzi Wake, ambao walimfuata kwa heshima. Alipowasili Shíráz, Báb aliletwa mbele ya gavana, ambaye alimtendea ukatili wa kuaibisha. Hadharani alimkemea na kumlaumu Báb. Halafu alimuachilia chini ya ulinzi wa mjomba Wake. Ingawa Báb aliruhusiwa kurudi nyumbani Kwake, uhuru Wake uliwekewa mipaka. Watu wa familia Yake tu na wengine wachache waliruhusiwa kumuona. Walakini, licha ya majaribio ya yule gavana na makasisi kukomesha uwezo Wake, idadi ya wafuasi Wake iliongezeka kwa haraka.

Habari za Tangazo muhimu la Báb zilienea kwa kiwango kikubwa sana kiasi kwamba mfalme wa Uajemi aliamua kumtuma msomi wake mwaminifu sana mwenye ujuzi mkubwa kwenda Shíráz kuchunguza hali. Akiwa kama mgeni nyumbani kwa gavana mwenyewe, yule mgeni msomi alikutana na Báb mara tatu. Alikuwa amedhamiria kukanusha madai ya Báb, lakini katika kila mkutano yeye aliendelea kuvutiwa zaidi kwa ujuzi Wake, ufasaha na hekima. Hadi kufikia mkutano wa tatu, Vaḥíd — jina ambalo kwalo msomi baadaye alikuja kujulikana — alikuwa amepata uhakika kabisa juu ya Daraja Tukufu la Kijana huyo. Vaḥíd baadaye alieleza kuwa, wakati wa mkutano pamoja na Báb, yeye alijihisi "duni kama vumbi chini ya miguu Yake". Yeye mara moja alituma taarifa kwa maandishi kwa baraza la mfalme na aliondoka Shíráz kwa maagizo ya Báb. Tangu siku hiyo kwenda mbele, yeye aliziweka wakfu nguvu zake kwa uendelezaji wa Hoja Yake na mwishowe aliyatoa maisha yake dhabihu katika njia ya Mpendwa wake.

Kutokana na kuongezeka kwa upendo na umashuhuri wa Báb, hasira ya gavana iliongezeka. Yeye kwa mara nyingine tena aliamuru kukamatwa Kwake. Safari hii yule gavana alikusudia kumuua Báb, na alimtuma askari polisi mmoja kumkamata nyumbani kwa mjomba Wake usiku wa manane. Usiku huohuo, hata hivyo, janga la tauni lilitokea katika mji wa Shíráz na mji mzima ulikuwa katika hali ya taharuki. Ndani ya muda mfupi, zaidi ya watu mia walikufa kutokana na janga hili la kutisha. Vilio na kelele za maumivu na huzuni viliweza kusikika kila mahali mitaani, na wakaazi wa mji walianza kuukimbia kwa vurugu. Bila uhakika wowote kuhusu kile alichotakiwa kufanya, afisa mmoja aliamua kumpeleka Báb nyumbani kwake mwenyewe. Alikuwa amefadhaika sana alipofika nyumbani na kumkuta mwanae amepatwa na tauni pia. Alihamaki kwa mshituko mkubwa, alijitupa miguuni mwa Báb na alimuomba msamaha. Mtoto wake wa kiume wa askari polisi, alipoponywa kimuujiza, yeye alitambua Mkono wa Mungu katika kuzuka kwa tauni hiyo na alimsihi yule gavana kumuachilia Báb.

Gavana akihofia maisha ya familia yake na wengine, alimwachilia Báb, kwa sharti kwamba Báb angeondoka Shíráz.

Wakati wa kipupwe cha 1846 Báb aliondoka kuelekea Iṣfáhán, mji uliopo kaskazini mwa Shíráz. Akimuaga mjomba Wake, Alimwambia: "Nitakutana nawe tena katikati ya milima ya Ádhirbáyján, kutoka hapo nitakutuma kwenda kupata taji la kifo cha kishahidi. Nami nitakufuata pamoja na mmoja wa wanafunzi wangu mwaminifu, tutaungana katika milki ya milele."[12]

1. Quddús alifanya nini alipowasili huko Shíráz? ______________________________

   ______________________________________________________________________

2. Nani alimpinga Quddús alipoanza kufundisha Ujumbe wa Báb mjini Shíráz? ______

   ______________________________________________________________________

3. Neno "kasisi" lina maana gani? ______________________________________

   ______________________________________________________________________

4. Ni maneno gani huelezea tabia ya gavana wa Shíráz? _________________________

   ______________________________________________________________________

5. Gavana aliamuru adhabu gani kwa ajili ya Quddús na wenziwe wawili? __________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

6. Neno hili "uzushi wa kidini" lina maana gani? ______________________________

   ______________________________________________________________________

7. Baada ya kuwafukuza Quddús na wenzake wawili kutoka Shíráz, gavana aliwaagiza walinzi wake wafanye nini? ______________________________________________

   ______________________________________________________________________

8. Báb alikuwa anafanya nini pale kikundi cha walinzi wapanda farasi kilipokutana Naye?

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

9. Báb alimwambia kiongozi wa maaskari waliotumwa kumkamata Yeye, "Gavana am__________________________________ Mimi. _________________ hapa; nifanyieni kama _________________. Kwa kuja kukutana nanyi, _________________ urefu wa _________________ wenu, na _________________ kunipata Mimi." Kiongozi alijaribu kupuuzia alichosema Báb na alikuwa anajiandaa

kuondoka ndipo Báb aliposema: ". . . Nimepuuzia ____________ Yangu mwenyewe na ___________ kuwa chanzo cha ________________ au ________________ kwa mtu yeyote. ________________ kwamba ________________ Mimi. Napendelea ________________________________ mikononi mwenu, kuliko ________________ wewe na wenzi wako ________________ usio ________________ kwa ajili Yangu."

10. Báb alivunjaje uadui wa maaskari? ________________________________________

____________________________________________________________________

11. Báb alifika Shíráz kwa namna gani? ________________________________________

____________________________________________________________________

12. Gavana alichukua hatua gani dhidi ya Báb?____________________________________

____________________________________________________________________

13. Yalikuwa na matokeo gani majaribio ya gavana na makasisi, katika miezi iliyofuata kukomesha ushawishi Wake?________________________________________________

____________________________________________________________________

14. Vaḥíd alikuwa nani?_____________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

15. Gavana alifanyaje alipoona watu walivyozidi kumpenda Báb? _________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

16. Ni nini kilimfanya yule gavana hatimaye kumuachilia Báb na kumruhusu kuondoka Shíráz? ___________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

17. Báb alikwenda wapi alipoondoka Shíráz? ___________________________________

18. Alifanya lini hii safari?___________________________________________________

19. Je, Alimwambia nini mjomba Wake, pale alipomuaga? _______________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

20. Unda jozi pamoja na mjumbe mwingine wa kundi lako na simulieni kwa zamu pamoja na mwenzako hadithi ya wakati wa kukutana kwa maaskari wapanda farasi na Báb katika pori lililokuwa kati ya Bú<u>sh</u>ihr na <u>Sh</u>íráz.

## SEHEMU YA 6

Báb alipokuwa anakaribia mji wa Iṣfáhán, alimuandikia barua gavana wa jimbo hilo akimuomba kupanga mahali ambapo Yeye angeishi. Tofauti na yule gavana wa <u>Sh</u>íráz, gavana huyu alikuwa mtu mwenye roho safi na mwenye haki. Aliguswa mno na adabu na mtindo wa barua ya Báb kiasi kwamba alimwagiza mtu mwenye madaraka ya juu kabisa wa dini wa jimbo hilo kumpokea Báb nyumbani kwake na kumpa mapokezi yenye upendo na ukarimu.

Katika kipindi ambamo Báb aliishi Iṣfáhán, makundi ya watu yalikuja kumuona kila siku na kusikiliza maneno Yake yenye hekima. Lakini ule umaarufu wa Báb ulioendelea kukua, uliamsha wivu wa makasisi wa mji huo, ambao waliogopa kupoteza daraja lao na mamlaka ambayo walikuwa nayo kwa muda mrefu. Walianza kueneza uvumi kuhusu Báb, wakitumaini kuamsha tuhuma dhidi yake. Jambo hili liliposhindwa, walibuni mpango wa kumuua Báb. Yule gavana, alipotambua njama za makasisi dhidi ya Báb, aliamua kumkaribisha ili akae nyumbani mwake mwenyewe. Hapo, katika muda uliotumia kuzungumza na Báb, yule gavana polepole alikuja kufahamu ukuu wa Ufunuo Wake. Siku moja, alipokuwa ameketi na Báb kwenye bustani ya nyumbani kwake, yule gavana alimwambia maneno haya:

> "Mpaji Mwenyezi amenijaalia mimi kwa utajiri mwingi. Mimi sijui njia nzuri zaidi ya kutumia utajiri huu. Sasa kwa kuwa kwa msaada wa Mungu, nimeongozwa kuutambua Ufunuo huu, ni shauku yangu ya dhati kutoa wakfu mali zangu zote kwa ajili ya kuendeleza maslahi yake na kusambaza umaarufu wake. Ni nia yangu kwenda, kwa idhini Yako kuelekea Ṭihrán, na kufanya kila niwezalo kumvutia mfalme kwa Hoja ya Mungu, ambaye imani yake kwangu ni thabiti na isiyoyumba."[13]

Kwa mmiminiko huu wa upendo na kujitolea, Báb alijibu:

> "Mungu akulipe kwa azma yako bora. Nia ya juu sana namna hiyo kwangu Mimi ni yenye thamani zaidi kuliko kitendo chenyewe. Siku zako na Zangu, walakini, ni fupi mno kuniwezesha Mimi kushuhudia, na kukuruhusu wewe kufikia na kufanikisha matumaini yako. Siyo kwa njia ambazo wewe unapenda kuzifikiria, kwamba Mjaalia Mwenyezi atatimiza ushindi wa Imani. Ni kupitia watu maskini na duni wa nchi hii, kwa damu ambayo hawa watakuwa wameimwaga katika njia Yake, ndio Mwenye mamlaka Mweza atahakikisha uhifadhi na kuimarisha msingi wa Hoja Yake. Mungu huyo huyo, katika ulimwengu ujao, Ataweka juu ya kichwa chako taji la utukufu wa milele, na kukumiminia baraka Zake zisizokadirika. Kuhusu muda wako wa maisha ya kidunia, imebaki miezi mitatu na siku tisa, baada ya hapo, kwa imani na yakini, utaharakia kwenye makazi yako ya milele."[14]

Miezi mitatu na siku tisa baadye, yule gavana wa Isfahan alifariki, sawa kabisa kama Báb alivyotabiri. Siku chache baada ya kifo chake, mrithi wake alituma ujumbe kwa mfalme huko Ṭihrán akimuuliza afanyeje kuhusu Báb. Mfalme alimuamuru kuwa ampeleke Báb kwa kumficha hadi mji mkuu huo, ambako mfalme alikusudia kukutana Naye. Hivyo, akiandamana na kikundi cha maaskari wapanda farasi, Báb alianza safari Yake kuelekea Ṭihrán.

1. Báb alimuandikia barua nani alipokuwa anakaribia mji wa Iṣfáhán? ______________

______________________________________________________________________

2. Ni maneno yapi yanayoweza kueleza tabia za gavana wa Iṣfáhán?________________

______________________________________________________________________

3. Gavana alimpa maagizo gani afisa mkuu kabisa wa kidini wa jimbo hilo?_________

______________________________________________________________________

4. Kitu gani kiliwafanya makasisi wa Iṣfáhán wawe na wivu? _____________________

______________________________________________________________________

5. Ni nini makasisi waliogopa kuwa wangepoteza kama Báb angeruhusiwa uendelea kutangaza Ujumbe Wake? _______________________________________________

______________________________________________________________________

6. Je, yule gavana wa Iṣfáhán alifanya nini kumlinda Báb dhidi ya njama za makasisi?_

______________________________________________________________________

7. Gavana alitaka kufanya nini kwa ajili Hoja ya Báb? ___________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

8. Báb alijibuje ombi la gavana? ___________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

9. Báb alieleza ukweli gani wa kina kuhusu maendeleo ya Hoja ya Mungu katika jibu Lake kwa gavana? ____________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

10. Mfalme alimpa amri gani mrithi wa gavana?________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Waziri mkuu wa Uajemi wa wakati ule alikuwa mtu mwenye ubinafsi na asiyefaa. Alihofia kwamba, kama Báb angekuja Ṭihrán na kukutana na mfalme, yeye angepoteza cheo chake mwenyewe na madaraka. Kwahiyo, alimshawishi mfalme kubadilisha maagizo yake na kumpeleka Báb kwenye jimbo la Ádhirbáyján katika upande wa kaskazini magharibi wa nchi hiyo.

Báb alikuwa chini ya ulinzi alipowasili Tabríz, mji mkuu wa jimbo hilo, mnamo Juni 1847, alipelekwa kwenye mojawapo ya nyumba za mji huo, ambayo ilichaguliwa kama kizuizi Chake. Kikosi cha askari kililinda mlango wa nyumba hiyo. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kuonana Naye, isipokuwa wafuasi Wake wawili. Watu wa mji huo walionywa kwamba yeyote ambaye angejaribu kuonana na Báb, angekamatwa na kufungwa gerezani, na mali zake zote zingenyang'anywa.

Báb aliishi mjini Tabríz kwa muda mfupi na halafu alihamishiwa kwenye ngome ya Máh-Kú, ambayo ilikuwa katika milima ya Ádhirbáyján mbali kabisa na miji mikubwa na midogo. Waziri mkuu alifikiria kuwa, kwa kumpeleka Báb katika kona hiyo ya mbali na isiyokalika ya nchi, mvuto Wake ungepungua, na Imani Yake polepole ingesahaulika. Lakini yeye hakutambua kuwa pindi taa ya dini ya Mungu ikishawashwa, hakuna mkono wa mtu unaoweza kuzima mwale wake. Kupitia utukufu Wake na wema wenye upendo, punde tu alipata heshima na mvuto kwa ofisa mwangalizi wa ngome na watu wa jimbo hilo.

Hivyo, makatazo makali aliyowekewa Báb pole pole yalilegezwa na milango ya ng'ome ilifunguliwa kwa wafuasi wake, ambao walikuja kumtembelea kwa idadi zilizoendelea kuongezeka kutoka sehemu mbalimbali za Uajemi. Katika kipindi cha kifungo Chake huko Máh-Kú, Báb alifunua Bayán ya Kiajemi, muhimu kabisa miongoni mwa Vitabu Vyake. Katika Kitabu hicho, Yeye alianzisha sheria za Kipindi Chake Kitakatifu, kwa uwazi na moja kwa moja alitangaza ujio wa Ufunuo mwingine mkuu zaidi kuliko Wake Mwenyewe, na aliwahimiza wafuasi Wake kumtafuta na kumtambua "Yule ambaye Mungu angemdhihirisha". Mmoja wa wafuasi Wake ambaye aliishi huko Máh-Kú wakati huo, alielezea ufunuo wa Bayán ya Kiajemi katika maneno haya:

> "Sauti ya Báb, alivyokuwa akiandika mafundisho na kanuni za Imani Yake, iliweza kusikika waziwazi na wale ambao walikuwa wakiishi chini ya mlima. Sauti tamu ya kughani Kwake, mtiririko wa mapigo ya aya ambazo zilimiminika kutoka midomo Yake, vilivutia masikio yetu na kupenya ndani ya roho zetu zenyewe. Mlima na bonde vilirudisha mwangwi wa ufahari wa sauti Yake. Mioyo yetu ilitetema kwa undani kabisa kwa mvuto wa matamshi Yake."[15]

Waziri mkuu alipojua kwamba Báb alikuwa amejipatia upendo uhimili wa watu wa Máh-Kú na kwamba Imani Yake ilikuwa ikiendelea kuenea nchini kote, alitoa amri kwamba Báb ahamishiwe katika ng'ome ya Chihríq. Walakini, huko pia, watu wa miji jirani na maafisa

wa ng'ome walivutiwa na haiba ya kuvutia ya Báb. Hata baadhi ya makasisi mashuhuri kabisa wa eneo hilo waliikubali Imani mpya na waliacha vyeo vyao vya heshima kuungana na wafuasi Wake.

Mara tu waziri mkuu aliposikia matukio yaliyotokea huko Chihríq, yeye alitoa amri kuwa Báb mara moja ahamishiwe Tabríz. Mkutano wa watu wa mamlaka ya kidini uliitishwa kumchunguza Báb na kupata njia ambayo ingefaa kabisa kukomesha ushawishi Wake. Wakati huo kilikuwa kipindi cha mwezi Julai 1848. Katika mkutano huo makasisi na maafisa wa Serikali walijaribu kumdhalilisha Báb, lakini walishindwa na utukufu Wake. Alipoulizwa, "Wewe unadai kuwa ni nani, na umeleta ujumbe gani?" Yeye alitangaza:

> **"Mimi ndiye, Mimi ndiye, Mimi ndiye, Yule Mwahidiwa! Mimi ni Yule ambaye jina lake kwa miaka elfu moja mmeliita, ambaye kwa kutajwa kwake mmeamka, ambaye ujio Wake mmetamani sana kushuhudia, na ambaye saa ya Ufunuo Wake mmemuomba Mungu kuiharakisha. Kwa Ukweli nasema, imewapasa watu wa Mashariki na Magharibi pia kutii neno Langu na kuahidi utiifu kwa nafsi Yangu."**[16]

Siku chache baada ya mkutano ule, Báb alirudishwa Chihríq. Maadui wake walikuwa wametumaini kwamba kwa kumleta Yeye huko Tabríz wangeweza kumshurutisha kuacha Dhima Yake. Lakini mwishowe waliamua kwamba, kama Báb angeendelea kuwa hai, isingewezekana kuzuia wimbi la nguvu Yake iliyokuwa ikiendelea kukua miongoni mwa watu wa Uajemi.

1. Ni maneno gani yanayo weza kueleza tabia ya waziri mkuu wa Uajemi wa wakati huo?

   ____________________________________________

   ____________________________________________

2. Kwa nini waziri mkuu alihofia kukutana kwa mfalme na Báb?__________________

   ____________________________________________

3. Je, waziri mkuu alifanya nini kumzuia mfalme asikutane na Báb? ________________

   ____________________________________________

4. Kwa nini askari walilinda mlango wa nyumba ambamo Báb alikaa huko Tabríz?

   ____________________________________________

   ____________________________________________

5. Watu wa mji huo walipewa onyo gani? ____________________________________

   ____________________________________________

   ____________________________________________

6. Báb alihamishiwa wapi baada ya kukaa muda mfupi mjini Tabríz? ______________

   ____________________________________________

7. Waziri mkuu alifikiri nini kingetokea kwa Hoja ya Báb kama angefungwa huko Máh-Kú?

8. Jinsi gani fikira za waziri mkuu zilikosea?

9. Milango ya gereza la Báb huko Máh-Kú ilifunguliwaje kwa wafuasi Wake?

10. Báb alifunua kitabu kipi muhimu alipokuwa amefungiwa katika ng'ome ya Máh-Kú?

11. Ni zipi baadhi ya mada za Bayán ya Kiajemi?

12. Katika Bayán, Báb aliwahimiza wafuasi Wake wamtafute na kumpata nani?

13. Je, waziri mkuu alifanya nini aliposikia kwamba Imani ya Báb ilikuwa inaendelea kuenea?

14. Je, Hoja ya Báb iliathiriwaje kwa uhamisho Wake kwenda Chihríq?

15. Je, wale maadui wa Báb walifikiria wangetimiza kitu gani kwa kumleta kutoka Chihríq kwenda Tabríz?

16. Je, ni maswali gani watu wa mamlaka walimuuliza Báb wakati wa kuhojiwa Kwake?

17. Je, Báb ilitangaza nini katika kuyajibu maswali yao? ______________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

## SEHEMU YA 8

Akirejea kwa Báb, ‘Abdu’l-Bahá amesema:

**“Kumhusu Báb — roho yangu iwe dhabihu Yake! — katika umri wa ujana, yaani pale Yeye alipofikia mwaka wa ishirini na tano wa maisha Yake yaliyobarikiwa, Yeye alisimama mbele kuitangaza Hoja Yake. . . . Yeye akiwa Peke Yake kabisa, katika namna ambayo haiwezi kufikirika, Yeye aliisimamisha Hoja miongoni wa Waajemi, ambao ni maarufu kwa msimamo wao mkali. Kiumbe huyu mwangavu aliinuka kwa uwezo mwingi kiasi kwamba Alitikisa misingi ya kidini, sheria, ya mienendo, ya desturi, ya kimaadili na tabia za Uajemi, na alianzisha sheria mpya, imani na dini mpya. Ingawa watu maarufu wa nchi, idadi kubwa ya watu na viongozi wa dini mmoja na wote waliinuka kumharibu na kumtokomeza Yeye, Yeye peke Yake alikabiliana nao na aliisukuma Uajemi nzima. Maulamaa wengi kiasi gani na viongozi, na wakaazi wa nchi hiyo, ambao waliyatoa dhabihu maisha yao kwa furaha kamili katika njia Yake, na waliharakia kwenye uwanja wa kifo cha kishahidi!**

**“Serikali, taifa, makasisi na viongozi mashuhuri walitamani kuuzima mwanga Wake, lakini hawakuweza kufanya hivyo. Hatimaye mwezi Wake ulichomoza, nyota Yake iliwaka, misingi Yake ikasimamishwa kwa uthabiti, na upeo Wake ulijaa mwangaza. Yeye aliufundisha umati mkubwa kupitia elimu takatifu na kutoa athari nzuri mno ya ajabu juu ya fikira, maadili, desturi na mienendo ya Waajemi. Yeye alitangaza habari njema za udhihirisho wa Jua la Bahá kwa wafuasi Wake na aliwaandaa kwa imani na yakini.**

**“Udhihirisho wa dalili za ajabu kama hizo na ahadi yenye uwezo; athari zilizoletwa juu ya mawazo na akili za watu, uwekaji wa misingi ya maendeleo; na usitawishaji wa kanuni za mafanikio na ufanisi vilivyofanywa na mfanyabiashara kijana, hufanyiza uthibitisho mkubwa kabisa kuwa Yeye alikuwa Mwelimishaji wa Ulimwengu — jambo ambalo mtu yeyote mwenye haki asingesita kulikubali.”[17]**

Unahamasishwa kuandaa na kutoa hotuba fupi juu ya maisha ya Báb kufuatana na maneno ya ‘Abdu’l-Bahá ya hapo juu na kutokana na historia uliyoisoma hadi sasa.

## SEHEMU YA 9

Mnamo mwaka 1850, waziri mkuu mpya wa Uajemi, mwenye hamu ya kumwaga damu kama yule aliyetangulia, aliamuru adhabu ya kifo kwa Báb. Tena Báb aliletwa kutoka Chihríq hadi Tabríz. Hapo alifungiwa kwenye chumba kidogo kando ya uwanja, ambao ndio ungekuwa mandhari ya kifo Chake cha kishahidi.

Báb alipokuwa akiongozwa kwenye chumba kidogo cha gereza, kijana mmoja alilazimisha njia yake kupitia katikati ya umati wa watu na alijitupa mwenyewe kwenye miguu ya Báb. “Usiniondoe kutoka Kwako, Ee Bwana,” alisihi kijana huyo. Alimuomba Báb kumruhusu kumfuata popote ambapo Yeye angekwenda. “Inuka,” Báb alijibu, “na uwe mwenye uhakika kwamba utakuwa pamoja Nami. Kesho utashuhudia kile ambacho Mungu amekiamuru.”[18] Yule kijana mara moja alikamatwa, pamoja na wenzi wake wawili, na aliwekwa katika chumba kile kile ambamo Báb na mwandishi Wake walifungiwa. Kijana huyu alikuja kujulikana kama Anís.

Anís alisikia juu ya Ujumbe mpya kutoka kwa Báb Mwenyewe alipokuwa huko Tabríz kwa muda mfupi — licha ya makatazo makali ambayo, kwa wakati huo, yalikuwa yamewekwa baina Yake na wakaazi wa mji. Moto wa upendo wa Mungu uliwaka sana ndani ya moyo wa Anís kiasi kwamba tamaa yake pekee ilikuwa ya kujitoa dhabihu kwa ajili ya Imani yake mpya. Lakini baba yake wa kambo, alishituka kwa vitendo vya mwanae, na alimwekea Anís vizuizi asitoke nje, pia alimwekea ulinzi mkali nyumbani mwake. Humo Anís alipitisha majuma akisali na kutafakari, akimsihi Mungu amruhusu kufika, kwa mara nyingine tena, mbele ya Mpendwa wake. Siku moja, alipokuwa amezama katika sala, yeye alipata maono yasiyokuwa ya kawaida. Yeye alimuona Báb amesimama mbele yake na anamwita. Anís alijitupa mwenyewe miguuni Pake. “Furahia,” Báb alimwambia, “saa inakaribia, ambapo, katika mji huu, nitatundikwa mbele ya macho ya umati wa watu na nitakuwa mhanga wa moto wa adui. Sitamchagua yeyote isipokuwa wewe kushiriki Nami kikombe cha kifo cha kishahidi. Uwe mwenye na hakika kwamba ahadi hii ambayo ninakupa itatimizwa.”[19] Na hivyo Anís alianza kungojea kwa subira, akijua kwamba siku ingewadia ambamo yeye mapema tu angeungana tena na Mpendwa wake. Sasa mwishowe, yeye alikuwa amepata haja ya moyo wake.

Jioni ile Báb alikuwa anang’aa kwa furaha. Alizungumza kwa uchangamfu na Anís na wale wafuasi wengine watatu waaminifu waliofungwa pamoja Naye ndani ya kile chumba cha gereza. “Kesho,” Yeye aliwaambia, “itakuwa siku ya kuuawa Kwangu kishahidi. Laiti mmoja wenu hivi sasa angeinuka na, kwa mikono yake mwenyewe, na kumaliza maisha Yangu. Napendelea zaidi kuuawa kwa mkono wa rafiki kuliko kwa ule wa adui.” Hakuna hata mmoja miongoni mwao aliyeweza kufikiria kutoa maisha ya thamani kama hayo, na walikaa kimya, machozi yakitiririka kutoka machoni mwao. Halafu ghafla, Anís alisimama na alisema kuwa yeye alikuwa tayari kutii chochote kile ambacho Báb angeamuru. “Kijana huyu ambaye ameinuka kutii mapenzi Yangu,” Báb alitangaza, “atauawa pamoja nami, kama shahidi. Yeye nitamchagua kushiriki Nami taji la kifo cha kishahidi.”[20]

Mapema asubuhi iliyofuata, tarehe 9 Julai 1850, Báb alikuwa anaendelea kuzungumza na mwandishi Wake ndipo afisa mmoja alipoingilia mazungumzo yao ghafla. “Siyo mpaka hapo nitakapokuwa nimemaliza kumwambia mambo yote Ninayotaka kumwambia,” Báb alimwambia yule afisa, “ndipo uwezo yoyote ya kidunia inapoweza kuninyamazisha Mimi. Hata kama ulimwengu wote ungetwaa silaha dhidi Yangu Mimi, walakini wangeshindwa kunizuia Mimi kutimiza kusudi Langu hadi neno la mwisho.”[21] Lakini yule afisa hakuelewa maana ya maneno ya Báb. Yeye hakujibu lolote na alimuagiza yule mwandishi amfuate. Báb

halafu alichukuliwa kutoka chumba Chake hadi kwenye nyumba za makasisi watatu wa vyeo vya juu kabisa wa mji wa Tabríz, ambao bila kusita, walitia sahihi amri ya kuuawa Kwake.

Baadaye asubuhi ile Báb aliongozwa kurudi kule kwenye uwanja ambako kundi la watu wanaokaribia elfu kumi walikuwa wamekusanyika juu ya mapaa ya nyumba kushuhudia kuuawa Kwake. Alikabidhiwa kwenye mikono ya Sám Khán, kamanda wa kikosi cha askari kilichoamriwa kumuua. Lakini Sám Khán alikuwa ana wasiwasi, akijikuta ameshikwa na hofu kwamba kitendo chake kingemletea ghadhabu ya Mungu juu yake. "Ninakiri Imani ya Kikristo," yeye alimueleza Báb, "na sina uadui wowote dhidi Yako. Kama Hoja Yako ni Hoja ya Ukweli, niwezeshe kuondokana na jukumu la kumwaga damu Yako." "Fuata maagizo yako," Báb alijibu, "na kama nia yako ni ya kweli, Mwenyezi hakika anaweza kukuondolea mfadhaiko wako."[22]

Sám Khán aliwaamuru watu wake kupigilia msumari wa chuma kwenye ukuta na kufunga kamba mbili juu yake. Kwenye kamba hizi mbili Báb na Anís walining'inizwa. Kikosi hicho ndipo kikajipanga katika safu tatu, kila safu moja ikiwa na watu mia mbili na hamsini. Moja baada ya nyingine, kila safu ilipiga risasi. Moshi kutoka kwenye zile bunduki mia saba na hamsini ulipotawanyika, umati ule ulioshangazwa uliona mandhari ambayo ilikuwa vigumu kuamini. Anís alikuwa amesimama mbele yao mzima na bila madhara, na Báb alikuwa ametoweka machoni pao. Zile risasi zilikuwa zimekata tu kamba walizokuwa wametundikwa nazo.Msako wa kumtafuta Báb kila mahali ulianza. Hatimaye alikutwa amekaa ndani ya chumba Chake za gereza akiwa na mwandishi Wake, akimalizia mazungumzo yake yaliyokuwa yamekatishwa. "Nimemaliza mazungumzo yangu," Báb alisema. "Sasa mnaweza kuendelea kutimiza azma yenu."[23]

Akiwa amepigwa butwaa na kile kilichotokea, Sám Khán alikataa kuruhusu watu wake kumdhuru Báb na aliwaamuru kuondoka pale uwanjani. Kikosi kingine kiliitwa kufanya mauaji. Kwa mara nyingine tena Báb na Anís walitundikwa katika uwanja ule, na askari walipiga risasi. Safari hii risasi zilifanikiwa. Miili ya Báb na Anís ilivunjwavunjwa kabisa; lakini nyuso zao ni kama hazikuguswa. Wakati ule kikosi kinajiandaa kupiga risasi, Báb aliuambia maneno haya ya mwisho ule umati uliokuwa ukitazama:

> **"Enyi kizazi kaidi! Laiti mngeniamini Mimi, kila mmoja wenu angefuata mfano wa kijana huyu ambaye katika daraja alisimama juu yenu, na kwa hiari angejitoa dhabihu mwenyewe katika njia Yangu. Siku itakuja ambapo mtakuwa mmenitambua Mimi; siku hiyo sitakuwa tena miongoni mwenu."[24]**

1. Báb aliuawa kishahidi katika mji gani? ______________________________

2. Nani aliamuru kuuawa kwa Báb?______________________________
______________________________

3. Katika maneno yako mwenyewe, eleza hadithi ya jinsi yule kijana, Anís, alivyokuja kuuawa kishahidi pamoja na Báb.

______________________________
______________________________
______________________________

4. Kwanini Anís alichaguliwa na Báb kushiriki naye taji la kifo cha kishahidi? ________

5. Pale yule afisa alipomkatisha Báb na mwandishi Wake asubuhi ya Mauaji Yake, Báb alimwambia hivi: “Siyo mpaka hapo nitakapokuwa nimemaliza kumwambia ________ yote ________________ kumwambia, ndipo nguvu ________________________ ________________________________ Mimi.”

6. Kamanda wa jeshi wa kile kikosi kilichoamrishwa kutekeleza mauaji ya Báb alikuwa anaitwa nani? ________________________

7. Je, Sám Khán alimuomba nini Báb? ________________________

8. Je, Báb alimuambia Sám Khán kufanya nini? ________________________

9. Ni askari wangapi walimpiga risasi Báb na mwenziwe Anís? ________________

10. Umati ulioshangazwa uliona nini pale moshi wa risasi za bunduki ulipotawanyika?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

11. Je, Báb alikuwa anafanya nini pale walipompata? ______________________

______________________________________________

12. Báb alisema nini walipompata hatimaye? ______________________

______________________________________________

______________________________________________

13. Kifo cha kishahidi cha Báb kilitokea tarehe ngapi? ______________________

______________________________________________

14. Báb alikuwa wa umri gani wakati wa kuuawa Kwake kishahidi? ____________

______________________________________________

15. Katika nafasi iyopo hapo chini, andika maneno ya mwisho yaliyosemwa na Báb kwa umati ambao ulikuwa umekusanyika kushuhudia mauaji Yake.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 10

Inapendekezwa kwamba uchore juu ya ramani kwenye ukurasa unaofuata njia ya safari za Báb na uhamisho Wake. Utakapokuwa unafanya hivyo, jaribu kukumbuka kitu gani kilitokea kila mahali na tafakari juu ya maana yake.




## SEHEMU YA 11

Katika kitengo hiki umejifunza kuhusu maisha ya mmojawapo wa Wadhihirishaji Pacha wa Mungu wa Siku hii. Wakati wa maisha Yake mafupi Báb alisababisha mapinduzi ya kiroho huko Uajemi. Maelfu kwa maelfu ya roho safi walikubali Ujumbe Wake na walianza kujiandaa wenyewe kwa ajili ya kuja kwa Mdhihirishaji wa Mungu Ambaye Báb alimtaja kama "Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha". Unajua kwamba wakati wowote Mdhihirishaji wa Mungu anapotokea duniani, wale wenye kiu ya kupata nguvu na uongozi huinuka dhidi Yake na hujaribu kuuzima mwangaza wa Ufunuo Wake. Katika tukio hili siyo tu kuwa Báb aliuawa na viongozi wajinga wa Uajemi, bali pia maelfu ya wafuasi Wake waliuawa. Maisha ya kishujaa ya Wabábí hawa wa mwanzoni, ambao waliunyweshea mti wa Ufunuo mchanga kwa damu yao, yatakuwa mada ya uchunguzi wako katika miaka ijayo. Watu kama vile Mullá Ḥusayn, Quddús, Ṭáhirih na Vahíd watakuwa chanzo cha uvuvio na ujasiri kwako katika maisha yako yote kadiri unavyoendelea kujifunza juu ya historia isiyo ya kawaida ya miaka ya

mwanzoni ya Zama za Bahá'í. Kwa hivi sasa, tutafakari juu ya swali moja la kimsingi: Jinsi gani katika kipindi cha muda mfupi kama huo maisha ya maelfu ya watu yangeweza kubadilishwa kabisa na kutoka watu waliobobea katika ushirikina na wakitawaliwa kabisa na viongozi wapotovu, roho takatifu kama hizo zingeinuka na kufanya vitendo ya ujasiri kama huo? Jibu linaweza kupatikana tu katika Nafsi ya 'Alí-Muḥammad, Báb. Hivyo, inashauriwa tujifunze na kutafakari juu ya vifungu fulani kutoka kwenye maandiko ya Bahá'u'lláh, 'Abdu'l-Bahá na Mlinzi juu ya Nafsi hii Takatifu.

Katika Wosia na Agano Lake, 'Abdu'l-Bahá anasema:

**"Huu ndio msingi wa imani ya watu wa Bahá (maisha yangu yatolewe kwa ajili yao): 'Mtakatifu, Yule Aliyetukuka (Báb), ni Udhihirisho wa Umoja na Upekee wa Mungu na Mtangulizi wa Uzuri wa Kale. Mtakatifu Uzuri wa Abhá (maisha yangu yawe dhabihu kwa ajili ya marafiki Wake thabiti) ni Mdhihirishaji Mkuu Kabisa wa Mungu na Chimbuko la Kiini Chake Kitukufu Kabisa. Wengine wote ni watumishi Kwake na hutii amri Yake.'"[25]**

Katika *Mungu Yu Nasi*, tunasoma fungu lifuatalo lililoandikwa na Mlinzi:

**"Báb, akitangazwa kwa shangwe na Bahá'u'lláh kama 'Kiini cha Viini,' 'Bahari ya Bahari zote,' 'Nukta ambayo huzungukiwa na Uhalisi wa Mitume na Wajumbe,' 'Ambaye kutoka Kwake Mungu amesababisha kutokea kwa elimu ya vyote vile vilivyokuwepo na vitakavyokuwepo,' Ambaye 'daraja Lake huyapita yale ya Mitume Wote,' na Ambaye 'Ufunuo Wake hupita kabisa ufahamu na uelewa wa wateule wao wote,' amewasilisha Ujumbe Wake na kutimiza dhima Yake. Yule Ambaye alikuwa, katika maneno ya 'Abdu'l-Bahá, 'Asubuhi ya Ukweli' na 'Mtangulizi wa Mwanga Mkuu Kabisa,' Ambaye ujio Wake huashiria kwa wakati huohuo mwisho wa 'Kipindi cha Ubashiri' na mwanzo wa 'Kipindi cha Utimizo,' kwa wakati huohuo kupitia Ufunuo Wake amefukuza vivuli vya usiku ambavyo vilikuwa vimeshuka juu ya nchi Yake, na wakati huo huo kutangaza kuchomoza kulikotarajiwa kwa lile Duara lisilolinganishika ambalo wangavu Wake ungefunika jamii nzima ya wanadamu."[26]**

Bahá'u'lláh Mwenyewe alielezea:

**"Kwamba muda mfupi kama huo ungetenganisha Ufunuo huu wenye nguvu kabisa na wa ajabu kutoka Udhihirisho Wangu uliotangulia, ni siri ambayo hakuna mtu anayeweza kuifumbua na fumbo ambalo hakuna akili iwezayo kulielewa."[27]**

'Abdu'l-Bahá anasema:

**"Kujitokeza kwa Báb hufanana na alfajiri, kwa kuwa alfajiri hubeba ahadi ya jua. Alfajiri ya Báb iliahidi kuchomoza kwa Jua la Ukweli ambalo litazingira ulimwengu mzima."[28]**

## SEHEMU YA 12

Katika maisha Yake mafupi kama Mdhihirishaji wa Mungu duniani, Báb alifunua idadi kubwa ya Vitabu na Nyaraka. Sasa kwa kuwa umemaliza masomo yako juu ya maisha Yake, inapendekezwa kwamba ukariri sala Zake mbili ziizopo hapa chini.

> **"Kuna Muondoa shida yeyote isipokuwa Mungu? Sema: Mungu asifiwe! Yeye ni Mungu! Wote ni watumishi Wake, na wote hutii amri Yake!"[29]**


> **"Sema: Mungu hutosheleza vitu vyote juu ya vitu vyote, na hakuna chochote mbinguni au duniani bali Mungu hutosheleza. Hakika, Yeye Mwenyewe ndani Mwake ni Mjuzi, Mruzuku, Mwenye nguvu zote."[30]**

## SEHEMU YA 13

Katika kitengo ca tatu cha Kitabu cha 2, mlikazia jitihada zenu juu ya kujifunza kuongea juu ya nada kadhaa, hususan pamoja na wale ambao ni wapya katika Imani, wakati wa mfuatano wa ziara zitakazofanyika kwa kaya zao ndani ya jumuiya yenu. Sasa kwa kuwa mmemaliza kitengo hiki, mnaweza kuongeza kwenye orodha ya mada ambazo mngependa kuzizungumzia, historia ya maisha ya Báb. Kiasi cha tondoti mnazotaka kueleza katika tukio lolote, kwa uhakika kitategemea mambo mengi. Lakini bila kujali hali, mnaweza kutumaini kushiriki maelezo mapana juu ya matukio makuu ya maisha Yake kama Mtangulizi wa Bahá'u'lláh Mpiga mbiu wa Zama Mpya. Mara nyingine kurasa zifuatazo zinaweza kuwasaidia.

# Báb

## Mtangazaji wa Siku Mpya




**Báb alizaliwa mnamo tarehe 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, mji uliopo sehemu ya kusini ya Iran. Yeye alikuwa akingali mtoto mdogo, pale ambapo baba Yake alipofariki. Yeye alilelewa na mjomba wake, ambaye alimuweka shuleni kwenye umri mdogo.**




**Mwalimu wa Báb haraka alitambua uwezo wake mkuu na alielewa kwamba asingeweza kumfundisha mtoto asiye wa kawaida kama huyo. Báb alijaliwa na Mungu ujuzi wa asili.**



**Wakati ule watu wa Iran walikuwa wakingojea kuja kwa Mjumbe mpya wa Mungu. Waliomba kwamba Yeye angedhihirishwa mapema, na kuleta kipindi cha amani na haki juu ya ardhi. Wengi waliacha nyumba zao kumtafuta Mwahidiwa.**



**Mnamo jioni ya 23 Mei 1844, kijana mmoja aliwasili huko <u>Sh</u>íráz akimtafuta Mwahidiwa. Báb alimkuta nje ya malango ya mji na alimkaribisha nyumbani kwake kujiburudisha baada ya safari yake ndefu. Hapo Báb alijitangaza kwamba Yeye alikuwa Yule Ambaye kuja kwake watu walikuwa wakingojea kwa shauku mno.**




**Neno “báb” maana yake “lango” au “mlango”. Báb alitangaza kwamba karibu Mjumbe mwingine wa Mungu angetokea ambaye angeunganisha watu wote wa ulimwenguni katika ukoo mmoja. Báb alikuwa kama mlango wa kuwaongoza wanadamu kwenye wakati ujao mpya na mtukufu.**



**Idadi ya wafuasi wa Báb iliongezeka kwa haraka. Kotekote Iran, wao walianza kuenezo mafundisho matakatifu ambayo Yeye Aliyafunuwa.**




**Lakini punde tu watu wa serikali na makuhani, ambao walikuwa wakiuogopa ukweli, waliinuka dhidi ya Imani hii mpya ya Mungu. Walimfunga Báb katika ng'ome katika sehemu ya mbali ya nchi, mbali kutoka kwa wafuasi wake.**



**Wafuasi wa Báb waliteswa kikatili sana. Walishambuliwa, walipigwa na kutupwa gerezani. Maelfu waliuawa, lakini Hoja ya Mungu iliendelea kuenea.**



**Katika mwaka 1850 Báb aliuawa kama shahidi. Kwa amri ya serikali, Yeye alitundikwa uwanjani pamoja na mmoja wa wafuasi Wake na alipigwa risasi na kikosi cha askari. Báb alikuwa mwenye umri wa miaka 31 tu.**



**Báb alitoa maisha Yake kuandaa njia kwa ujio wa Bahá'u'lláh, "Utukufu wa Mungu", Ambaye bendera Yake ya Imani ilikusudiwa kuinuliwa katika kila pembe ya dunia.**

# MAREJEO


1. *Wana Mapambazuko: Simulizi ya Nabil ya siku za mwanzoni wa Ufunuo was Kibahá'í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1932, 2018 kuchapisha), ku. 75–76.

2. Kama hapo juu., uk. 57.

3. Kama hapo juu., uk. 63.

4. Kama hapo juu., uk. 65.

5. Kutoka hotuba iliyotolewa tarehe ya 23 Mei 1912, uliochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Zilizotolewa na 'Abdu'l-Bahá katika Ziara Yake yato Muungano wa Majimbo ya Amerikana Canada katika 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 2, uk. 196.

6. *Wana Mapambazuko*, ku. 85–86.

7. Báb, ilinukuliwa ndani ya *Wana Mapambazuko*, ku. 92–94.

8. *Wana Mapambazuko*, uk. 142–43.

9. Kama hapo juu., uk. 146.

10. Kutoka hotuba iliyotlewa na 'Abdu'l-Bahá juu ya 23 Mei 1912, uliochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 2, uk. 196.

11. *Wana Mapambazuko*, uk. 148–50.

12. Kama hapo juu., uk. 198.

13. Kama hapo juu., uk. 212.

14. Kama hapo juu., uk. 213.

15. Kama hapo juu., uk. 249.

16. Báb, iliyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, 2019 kuchapisha), uk. 34; pia katika *Wana Mapambazuko*, ku. 315–16.

17. 'Abdu'l-Bahá, katika Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2014, 2016 kuchapisha), na. 8.1–3, ku. 38–39.

18. *Wana Mapambazuko*, uk. 507.

19. Kama hapo juu., ku. 307–8.

20. Kama hapo juu., uk. 508.

21. Kama hapo juu., uk. 509.

22. Kama hapo juu., uk. 512.

23. Kama hapo juu., uk. 513.

24. Báb, ilinukuliwa ndani ya *Mungu yu Nasi*, uk. 84; pia katika *Wana Mapambazuko*, uk. 514.

25. *Wosia na Agano wa 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1944, 2013 kuchapisha), uk. 39.

26. *Mungu Yu Nasi*, ku. 90–91.

27. Bahá'u'lláh, iliyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh: Barua Zilizochaguliwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1991, 2012 kuchapisha), uk. 124.

28. *Abdul Baha juu ya Falsafa Tukufu* (Boston: The Tudor Press, 1918), ku. 51–52.

29. Báb, katika *Sala za Kibahá'í: Uteuzi wa Sala na Dua zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002, 2017 kuchapisha), uk. 221.

30. Kama hapo juu., uk. 55.



# Maisha ya Bahá’u’lláh

## Kusudi

Kupata utambuzi wa ukubwa wa
nguvu za kiroho alizoziachilia Bahá’u’lláh
na kujifunza kusimulia hadithi ya maisha Yake

## SEHEMU YA 1

Bahá'u'lláh, Ambaye jina Lake la kuzaliwa lilikuwa Mírzá Ḥusayn-'Alí, alizaliwa mnamo tarehe 12 Novemba 1817 huko Ṭihrán mji mkuu wa Uajemi. Baba yake Mírzá Buzurg, alikuwa mtu mashuhuri muungwana ambaye alikuwa na cheo kikubwa katika baraza la mfalme wa Kiajemi. Tangu udogo Wake, Bahá'u'lláh alionyesha ishara za ukuu na ujuzi usio kuwa wa kawaida na hekima. Yeye hakuhudhuria shule ya kawaida na alipata tu mafunzo kiasi nyumbani. Kuhusu utoto Wake, 'Abdu'l-Bahá anasema:

> **"Mkamilifu Aliyebarikiwa, Bahá'u'lláh alikuwa wa nasaba bora ya Uajemi. Tangu mapema kabisa utotoni Yeye alitofautishwa miongoni mwa jamaa Zake na marafiki. Wao walisema, 'Mtoto huyu ana uwezo wa ajabu usio kuwa wa kawaida.' Katika hekima, akili na kama chanzo cha ujuzi mpya, Yeye alikuwa amepita umri Wake na alikuwa bora kabisa juu ya mazingira iliyomzunguka. Wote waliomjua walishangazwa na upevu wa akili Yake. Ilikuwa ni kawaida kwao kusema, 'Mtoto kama huyu hataishi,' kwa kuwa kawaida huaminiwa kwamba watoto waliokomaa kiakili mapema hawafiki utu uzima."[1]**

Katika Waraka mmoja, Bahá'u'lláh Mwenyewe anatuambia hadithi kutoka utoto Wake kuhusu tukio moja lililotokea alipohudhuria sherehe ya harusi ya mojawapo kati ya ndugu zake wa kiume huko Ṭihrán. Kama ilivyokuwa kawaida huko Ṭihrán wakati huo, karamu kubwa ilifanywa kwa kipindi cha siku saba mchana na usiku. Ilipofika siku ya mwisho, yalifanywa maonesho ya vikaragosi kuhusu mfalme mmoja maarufu kama burudani kwa wageni. Bahá'u'lláh aliketi katika chumba cha juu kilichokuwa kimeelekea kwenye uwanja ambapo hema lilikuwa limesimikwa kwa ajili ya maonesho hayo.

Yeye anatuambia kwamba mchezo huo ulianza kwa kuingia kwa vikaragosi vidogo vikiwa katika umbo la wanadamu, vilitangaza ujio wa mfalme. Vikaragosi vingine zaidi halafu vilitokea. Baadhi vilikuwa vinafagia na vingine vilikuwa vinanyunyizia maji kwa ajili ya kuandalia kuwasili kwa mfalme. Baadaye kidogo, mpiga mbiu wa mji aliingia na kuwaambia watu kukusanyika kwa ajili ya kusikiliza mazungumzo ya mfalme. Vikundi kadhaa vya waheshimiwa vilitokea na kukaa katika sehemu zao maalum. Hatimaye, mfalme aliingia kwa ufahari. Alivaa taji kichwani mwake, alitembea taratibu na kwa utukufu na alikaa juu ya kiti cha enzi. Risasi zilipigwa, matarumbeta yalipigwa, na hema lilijaa moshi.

Moshi ulipoondoka, mfalme alikuwa bado amekaa kwenye kiti chake cha enzi, alionekana amezungukwa na mawaziri, wana-mfalme na maafisa wa kiserikali, wote walikuwa wamesimama wima kwa utulivu mbele yake. Wakati huo, mwizi mmoja aliletwa mbele ya mfalme. Naye alitoa amri kwamba yule mwizi akatwe kichwa. Bila kuchelewa, yule muuaji mkuu alitekeleza amri ya mfalme. Baada ya mauaji, mfalme alianza kuongea na mawaziri wake na maafisa. Ghafla habari zilifika kwamba maasi yalikuwa yametokea katika sehemu moja ya mipaka. Vikosi mara moja vilitumwa kuyavunja maasi hayo. Dakika chache baadaye, sauti ya risasi ya mzinga ilisikika kwa nyuma, na ilitangazwa kwamba vikosi vya mfalme vilikuwa katika mapambano dhidi ya waasi.

Hivyo, ule mchezo uliendelea. Bahá'u'lláh alitatanishwa sana na asili ya maonesho hayo. Baada ya mchezo kumalizika na pazia kufungwa, aliona mtu akitoka nyuma ya lile hema amebeba sanduku kwapani mwake. Bahá'u'lláh alimuuliza, "Hili sanduku ni nini na nini asili ya maonesho hayo?" Yule mtu alijibu, "Vikorokoro vyote hivi, mfalme, wana-mfalme, na

mawaziri, ufahari wao na utukufu, nguvu zao na uwezo, kila kitu ulichoona, vyote hivi sasa vimo ndani ya sanduku hili."[2] Kauli hii ilimgusa sana Bahá'u'lláh Ambaye baadaye alitamka:

> **"Tangu siku ile, vikorokoro vyote vya ulimwengu vilionekana katika macho ya Kijana huyu kama maonesho yale. Kamwe havijakuwa, wala daima havitakuwa, vyenye maana wala umuhimu wowote, hata kulingana na kiasi cha punje ya mbegu ya haradali. . . .**
>
> **"Hivi punde tu vikorokoro hivi vinavyoonekana, hazina hizi zinazoonekana, majivuno yote ya kidunia, majeshi haya yaliyoandaliwa, umaridadi wote huu wa urembo, roho hizi zenye kiburi na majivuno – vyote vitaingia ndani ya kingo za kaburi, kana kwamba vimeingia ndani ya sanduku lile. Katika macho ya wale wenye umaizi, ugomvi wote huu, mafarakano na majivuno vimekuwa, na daima vitakuwa, kama mchezo wa watoto wadogo."[3]**

Hadithi nyingine inayohusu utoto wa Bahá'u'lláh ni ndoto Ambayo baba Yake aliiota ambamo Bahá'u'lláh alionekana kuwa

> "alikuwa anaogelea ndani ya bahari kubwa, isiyo na mipaka. Mwili wake uling'aa juu ya maji kwa mnururiko ambao uliangazia bahari. Kuzungukia kichwa Chake, ambacho kiliweza kuonekana kwa uwazi juu ya yale maji, nywele Zake ndefu na nyeusi zilisambaa katika pande zote, zikielea kwa wingi mno juu ya mawimbi. . . . Samaki lukuki walimzunguka, kila mmoja alishikilia imara kwenye ncha ya unywele mmoja. Walivutiwa sana na mng'ao wa uso Wake, walimfuata upande wowote ule alikoogelea. Ijapokuwa idadi yao ilikuwa kubwa mno, na japokuwa walishikilia sana nywele zake, hakuna hata unywele mmoja ulioelekea kukatika kutoka kichwani kwake, wala madhara hata kidogo kabisa kuathiri nafsi Yake. Alikuwa huru na bila kuzuiliwa, Yeye alisonga mbele juu ya yale maji na samaki wote walimfuata Yeye."[4]

Ndoto hii ilimwathiri baba Yake Bahá'u'lláh, hata alimwita mtu maarufu mwenye umaizi, na alimuomba kutafsiri ndoto kwa ajili yake. Mtu huyu, kana kwamba amevuviwa kidogo na mustakabali wa Bahá'u'lláh, alisema:

> "Ile bahari kuu isiyo na mipaka ambayo umeiona katika ndoto yako siyo kingine ila ni ulimwengu wa uhai. Bila msaada na peke Yake, mwanao atajipatia mamlaka ya juu kabisa juu ya ulimwengu. Popote atakapopenda, ataenda bila kuzuiliwa. Hakuna atakayepinga mwendo Wake, hakuna atakaye zuia maendeleo Yake. Wale samaki wengi wanamaanisha msukosuko ambao Yeye atauamsha miongoni mwa watu na jamaa za dunia. Watakusanyika kumzungukia Yeye, na Kwake watang'ang'ania. Akihakikishiwa ulinzi usioshindwa wa Mwenyezi, msukosuko huu kamwe hautadhuru nafsi Yake, wala upweke wake ndani ya bahari ya maisha hautahatarisha usalama Wake."[5]

1. Jina la Bahá'u'lláh lilikuwa lipi? ____________________________________________

2. Alizaliwa tarehe ngapi? ____________________________________________________

3. Alizaliwa wapi? ________________________________________________________

4. Uajemi inajulikana kwa jina lipi leo? ______________________________________

5. Baba Yake Bahá'u'lláh alikuwa anaitwa nani? _______________________________

6. Baba Yake Bahá'u'lláh alikuwa ana wadhifa gani? ___________________________
______________________________________________________________________

7. Je, Bahá'u'lláh alionesha dalili zipi alipokuwa mtoto? ________________________
______________________________________________________________________

8. Je, Bahá'u'lláh alipata elimu ya aina gani? _________________________________
______________________________________________________________________

9. Elezea maonesho ya vikaragosi ambayo Bahá'u'lláh aliyaona katika utoto Wake.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

10. Bahá'u'lláh alifikiria nini, alipojua kwamba ule mchezo pamoja na mfalme, mawaziri, maaskari na kiti cha enzi vyote vilikuwa vimewekwa ndani ya sanduku? _________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

11. Bahá'u'lláh alitamka kwamba tangu siku alipoona yule mfalme, mawaziri, maaskari na kiti cha enzi vikiwekwa mbali katika sanduku: " . . . ______________________ , vikorokoro vyote vya ___________________ vilionekana katika ________________ ya ______________ huyu kama maonesho yale. Kamwe ____________________ , wala daima _________________ vyenye maana wala umuhimu wowote, hata kulingana na kiasi cha ___________ ya mbegu ya ___________ . . . . Hivi punde tu

________________ hivi vinavyoonekana, ___________ hizi __________________ , majivuno yote ya ___________ , majeshi haya ______________________ , umaridadi wote huu wa ___________ , roho hizi zenye _______________ na _______________ vyote ___________ ndani ya kingo za ___________ , kana kwamba vimeingia ndani ya ___________ lile. Katika ___________ ya wale wenye ___________ , ugomvi wote huu, __________________ na majivuno __________________ , na daima vitakuwa, kama ___________ wa watoto ___________ .”

12. Simulia katika maneno yako mwenyewe ndoto ya Mírzá Buzurg.

____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________

13. Nini ilikuwa maana ya bahari kuu katika ndoto? ____________________________

____________________________________________________________________

14. Nini ilikuwa maana ya samaki wengi waliokusanyika kumzunguka Bahá’u’lláh katika ndoto? _____________________________________________________________

____________________________________________________________________

15. Je, ilikuwa na maana gani kwamba Bahá’u’lláh alikwenda mbele kwa uhuru na bila kuzuiliwa juu ya yale maji? _____________________________________________

____________________________________________________________________
____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 2

Wadhihirishaji watukufu wamejaaliwa ujuzi wa kiasili na hawahitaji kujipatia mafundisho mashuleni na vyuo vikuu. Wao ni waelimishaji na siyo waelimishwaji. Bahá’u’lláh anasema:

**"Mdhulumiwa Huyu hakwenda shule wala hakuhudhuria mijadala ya wanazuoni. Kwa uhai Wangu! Siyo kwa hiari Yangu kwamba nimejifunua Mwenyewe, lakini Mungu, kwa hiari Yake mwenyewe, amenidhihirisha Mimi."**[6]

Aliongelea juu ya ujuzi wa kiasili wa Bahá'u'lláh, 'Abdu'l-Bahá anaeleza:

**"Hakuna aliyeingia machoni Pake bila kupigwa na butwaa kutokana na uwezo Wake. Wanazuoni ambao walimwendea walishangazwa na elimu Yake, walakini Yeye abadan hakwenda shule wala hakufunzwa na watu. Marafiki Zake na ukoo Wake wote huthibitisha jambo hili, walakini Mafundisho Yake ndio roho ya zama hizi.**

**"Jua linatoa mwangaza wake kutoka kwake lenyewe, na halichoti mwangaza kutoka vyanzo vingine. Waalimu Watukufu wana mwangaza wa kiasili ndani mwao; Wao wana elimu na ufahamu wa vitu vyote ulimwenguni; ulimwengu uliobaki hupata mwangaza kutoka Kwao na kupitia Kwao sanaa na sayansi zinahuishwa katika kila zama."**[7]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

    a. Jua linatoa __________________ wake kutoka kwake lenyewe, na halichoti ______________ kutoka __________________________________ .

    b. Walimu Watukufu wana ______________________________ .

    c. Walimu Watukufu wana _______________ na ________________ wa vitu vyote ulimwenguni.

    d. Kutoka kwa Waalimu Watukufu, ulimwengu uliobaki _____________________ .

    e. Kupitia Waalimu Watukufu sanaa na sayansi ___________________________ _______________ .

2. Pamoja na wajumbe wengine wa kikundi chenu, jadilianeni maana ya "elimu ya kiasili" na jinsi elimu ya asili unatofautiana na elimu ya kujifunza.

3. Kariri teuzi la hapo juu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh.

## SEHEMU YA 3

Kadri Bahá'u'lláh alivyoendelea kukua, ishara za Ukuu Wake zilizidi kudhihirika. Alipofikia rika la ujana Wake, alikuwa mashuhuri kwa ajili ya akili Yake makini, tabia Yake bora, ukarimu Wake na huruma. Aliweza kufumbua matatizo makubwa mno na kujibu maswali ya kutatiza na yenye undani mkubwa. Lakini licha ya uwezo Wake usio wa kawaida, hakutafuta cheo au umaarufu. Baba Yake alipofariki, Bahá'u'lláh aliombwa kufuata nyayo zake na kujitwalia cheo cha baba Yake katika baraza la mfalme. Lakini Yeye alikataa. Yeye hakuvutiwa na vyeo na heshima ya ulimwengu huu. Shauku Yake ilikuwa katika kuwatetea maskini na

kuwalinda wenye dhiki. Alipofikisha umri wa miaka kumi na nane Bahá'u'lláh alimuoa Ásíyih Khánum na nyumba yao ikawa kimbilio kwa wote. Hakuna mtu aliyenyimwa ukarimu wao.

Bahá'u'lláh alikuwa mwenye umri wa miaka ishirini na saba, ambapo mnamo 23 Mei, 1844 Báb alipotangaza Dhima Yake kwa Mullá Ḥusayn huko Shíráz. Hata miezi mitatu ilikuwa haijapita baada ya tukio hili la kihistoria, Bahá'u'lláh alipokea hati kutoka kwa Báb lililokuwa na baadhi ya Maandiko Yake. Yeye mara moja alishuhudia juu ya ukweli wa Ufunuo wa Báb na aliinuka kutetea Mafundisho Yake. Hadithi kuhusu jinsi Bahá'u'lláh alivyokuja kupokea hati hiyo ni kama ifuatavyo.

Muda mfupi baada ya Báb kuteua wanafunzi Wake wateule, wale Herufi za Waliohai kumi na nane, Yeye Aliwaita mbele Yake na kuwapa maagizo ya kusamba kila mahali na kufundisha Imani Yake. Alimpa kila mmoja jukumu maalum, baadhi yao, Akiwatuma kwenda katika majimbo yao walikotoka kama uwanja wa juhudi zao. Kutoka miongoni mwa hawa roho kumi na nane zilizobarikiwa, Quddús aliteuliwa kuambatana Naye katika safari Yake ya kuhiji Makka, ambako angetangaza Dhima Yake. Yeye Alimwambia Mullá Ḥusayn, yule wa kwanza kumwamini, maneno haya: "Usihuzunike kwamba hukuchaguliwa kuambatana Nami katika safari Yangu ya hija huko Ḥijáz. Badala yake, nitaelekeza hatua zako kwenye mji ule ambao unatunza Fumbo lenye utakatifu mkubwa mno, kiasi kwamba, siyo Ḥijáz wala Shíráz inaweza kutumaini kushindana nao."[8] Yeye Alimpa Mullá Ḥusayn hati na alimuagiza kwenda Ṭihrán. Alimwambia amsihi Mungu kwamba amuwezeshe kuutambua mwanga wa siri iliyofichwa katika mji ule na kuingia katika uwepo wa Mpendwa.

Mullá Ḥusayn aliondoka kufanya dhima yake na, baada ya kupitia miji kadhaa, alifika Ṭihrán. Hapo alichukua chumba katika shule ya mafunzo ya kidini. Mojawapo ya vitendo vyake vya kwanza ilikuwa ni kuutangaza Ujumbe wa Báb kwa mkuu wa shule hiyo, ambaye aliukataa kwa ufidhuli. Walakini, mwanafunzi mmoja kijana wa shule hiyo aliyasikia mazungumzo yao bila kukusudia na aliguswa mno na maneno ya Mullá Ḥusayn. Aliamua kumtembelea usiku wa manane na kujua zaidi juu ya ujumbe alioutangaza kwa shauku kubwa kama hiyo. Mullá Ḥusayn alimpokea kijana huyo na alizungumza naye kwa heshima kuu na wema. Alimuambia kwamba yeye sasa alikuwa ameelewa kile kilichomleta hadi mahali hapo. Mkuu wa shule aliukataa kwa dharau Ujumbe aliokuwa ameuleta. "Tumaini langu," Mullá Ḥusayn alisema, "ni kwamba mwanafunzi wake angeweza, kuutambua ukweli wake, tofauti na mwalimu wake."[9]

Wakati wa mazungumzo yao, Mullá Ḥusayn alimuuliza mwanafunzi huyo alikokuwa anatoka. Alimjibu kwamba alitoka wilaya ya Núr, katika jimbo la Mázindarán. "Niambie," Mullá Ḥusayn aliuliza, "yupo hivi leo miongoni mwa ukoo wa marehemu Mírzá Buzurg-i-Núrí, ambaye anasifika kwa tabia yake, ucheshi wake, na mafanikio yake ya kisanii na ufanisi wa kiakili, yeyote ambaye amejithibitisha kuwa mwenye uwezo wa kudumisha zile mila za hali ya juu za nyumba hiyo mashuhuri?"[10]

"Naam," yeye alijibu, "miongoni mwa watoto wake wa kiume waishio hivi sasa, mmoja amejitofautisha Mwenyewe kwa zile sifa zilizombainisha baba Yake. Kwa maisha Yake adilifu, mafanikio Yake ya hali ya juu, wema Wake wenye upendo na ukarimu Wake, yeye amejithibitisha Mwenyewe mwana bora wa baba bora." "Yeye ana shughuli gani?" Mullá Ḥusayn aliuliza. "Yeye hufariji wenye huzuni na hulisha wenye njaa." "Je, Yeye ana cheo gani na daraja?" "Yeye hana kazi yoyote, isipokuwa kufanya urafiki na maskini na watu asiowajua." "Anaitwaje?" "Husayn-'Alí."[11]

Kwa kila jibu, Mullá Ḥusayn alijawa na furaha zaidi. “Je, Yeye hutumiaje muda Wake?” aliuliza zaidi. “Hutembea mwituni na hufurahia uzuri wa mashambani.” “Ana umri gani?” “Miaka Ishirini na nane.” Uso wa Mullá Ḥusayn ulichangamka kwa kuridhika na furaha alipomuuliza yule kijana: “Nadhani unakutana Naye mara nyingi?” “Mara kwa mara ninatembelea nyumbani Kwake,” yeye alijibu. “Utaweza kuwasilisha mikononi Mwake dhamana kutoka kwangu?” “Bila shaka kabisa,” lilikuwa jibu lake. Ndipo Mullá Ḥusayn alipompa lile hati likifunikwa ndani ya kitambaa na kumuomba kuiwasilisha kwa Bahá’u’lláh siku iliyofuata alfajiri. “Kama akiridhia kunijibu mimi,” Mullá Ḥusayn aliongezea, “kwa hisani yako tafadhali utanijulisha jibu Lake?”[12] Yule mwanafunzi alilichukua ile hati na, wakati wa alfajiri, aliinuka kutimiza ombi la Mullá Ḥusayn.

Alipokaribia nyumba ya Bahá’u’lláh, alimuona ndugu Yake, Mírzá Músá, amesimama kwenye lango na alimuelezea sababu ya ziara yake. Mírzá Músá alimuongoza yule kijana kufika mbele ya Bahá’u’lláh, na ile hati likawekwa mbele Yake. Bahá’u’lláh aliwaomba wakae kitako. Aliikunjua ile hati, alianza kusoma kwa sauti baadhi ya vifungu vyake. Alipomaliza kusoma kama ukurasa mmoja tu hivi, alimgeukia ndugu yake na kusema: “Músá, únalo la kusema? Kweli mimi nasema, yeyote ambaye anayeamini Kurani na anatambua asili yake Takatifu na bado anasita, hata iwe kwa kitambo kidogo, kukubali kwamba maneno haya yanayosisimua roho yamejaliwa uwezo uleule wa kuhuisha, kwa uhakika kabisa amekosea na amepotea sana kutoka katika njia ya haki.”[13] Akimruhusu yule kijana kuondoka mbele Yake, Bahá’u’lláh alimuomba kumpelekea Mullá Ḥusayn, kibonge cha sukari na kifurushi cha chai, kama zawadi kutoka Kwake, na kumpelekea shukrani Zake na upendo.

Akijawa na furaha, yule kijana aliinuka na kuharakia kurudi kwa Mullá Ḥusayn. Aliwasilisha ile zawadi na ujumbe kutoka kwa Bahá’u’lláh. Hakuna maneno yanayoweza kuelezea furaha ambayo kwayo Mullá Ḥusayn alivipokea. Kwa kichwa kilichoinamishwa, aliipokea ile zawadi na kuibusu kwa upendo mkubwa. Halafu alimkumbatia yule kijana, akayabusu macho yake, na akasema: “Rafiki yangu mpendwa sana! Naomba kwamba kama vile wewe ulivyoufurahisha moyo wangu, Mungu akujaalie furaha ya milele na kujaza moyo wako kwa furaha isiyo kwisha.”[14] Yule kijana alitatanishwa sana na vitendo vya Mullá Ḥusayn. Ni nini, alijiuliza kwa mshangao, kinachoweza kuwa asili ya fundo lililounganisha roho hizi mbili? Ni nini kinachoweza kuwa sababu ya urafiki kati yao? Kwa nini Mullá Ḥusayn alionyesha furaha kubwa sana alipopokea zawadi ndogo kama ile kutoka kwa Bahá’u’lláh? Yule kijana alikabiliwa na fumbo ambalo hakuweza kulifumbua.

Siku chache baadaye, Mullá Ḥusayn aliondoka kwenda Khurásán, jimbo lililoko kaskazini mashariki mwa Iran. Alipokuwa akimuaga yule mwanafunzi kijana kutoka Núr, alimwambia: “Usimnong’oneze mtu yeyote yale uliyoyasikia na kushuhudia. Acha hii iwe siri iliyofichwa kifuani mwako. Usilifichue jina Lake, kwani wale wanaohusudu daraja lake watainuka kumdhuru. Katika nyakati zako za taamuli, omba kwamba Mwenyezi amlinde, kwamba, kupitia kwake, awatukuze waliodhulumiwa, atajirishe maskini, na kuwaokoa walioanguka. Siri ya mambo imefichwa kutoka macho yetu. Jukumu letu ni kupaza wito wa Siku Mpya na kutangaza Ujumbe huu Mtukufu kwa watu wote. Roho nyingi, katika mji huu, zitamwaga damu yao katika njia hii. Damu hiyo itanywesha Mti wa Mungu, itaufanya ustawi, na kufunika wanadamu wote.”[15]

1. Je, Báb alifanya nini baada ya kuwateua wale Herufi za Waliohai kumi na nane? __

____________________________________________________________

2. Je, Báb alimchagua nani kuambatana Naye katika safari Yake ya hija kule Makka? _
__________________________________________________________________

3. Je, Ḥijáz hurejelea kwenye nchi gani? ______________________________________

4. Báb Alimwambia Mullá Ḥusayn, yule wa kwanza kumwamini, maneno haya: "_____________________ kwamba hukuchaguliwa kuambatana Nami katika _________________ Yangu ya hija huko ___________________ . Badala yake, nitaelekeza hatua zako kwenye mji ule ambao ______________________________ ______________________ mkubwa mno, kiasi kwamba, siyo ______________ wala _____________ inaweza kutumaini _______________________________ ."

5. Báb Alimpa nini Mullá Ḥusayn? _________________________________________
__________________________________________________________________

6. Alipofika Ṭihrán Mullá Ḥusayn alichukua chumba katika shule ya mafunzo ya kidini. Mkuu wa chuo alimjibuje kuhusu Ujumbe wa Báb? __________________________
__________________________________________________________________

7. Kwa nini Mungu alikuwa amemuongoza Mullá Ḥusayn kwenye shule hiyo? ______
__________________________________________________________________

8. Yule mwanafunzi aliyeukubali ujumbe wa Báb alikuwa akitokea wapi? __________
__________________________________________________________________

9. Makazi ya jadi ya Bahá'u'lláh yalikuwa wapi? ______________________________

10. Kama ilivyoelezwa na mwanafunzi kutoka Núr, alipokuwa anajibu maswali ya Mullá Ḥusayn:

- Baba Yake alijulikana kwa jambo gani? _______________________________
______________________________________________________________
- Bahá'u'lláh ilikuwa akifanya nini? ___________________________________
______________________________________________________________
- Alikuwa na cheo na daraja gani? _____________________________________
______________________________________________________________
- Je, Yeye aliutumiaje muda Wake? ____________________________________
______________________________________________________________

11. Mullá Ḥusayn alimuomba yule mwanafunzi kutoka Núr afanye nini? ____________

_____________________________________________________________________

12. Baada ya kusoma ukurasa wa hati ililotumwa na Báb, Bahá'u'lláh alisema: "Kweli mimi nasema, yeyote ambaye anayeamini _____________ na anatambua __________ ____________ Takatifu na bado _______________ , hata iwe kwa ______________ _______________ , kukubali kwamba _________________ haya yanayosisimua roho yamejaliwa _________________________________ , kwa uhakika kabisa amekosea na __________________ sana kutoka ____________ njia ya haki."

13. Mullá Ḥusayn alipokeaje zawadi kutoka kwa Bahá'u'lláh? ____________________

_____________________________________________________________________

14. Kitu gani kilimtatanisha yule mwanafunzi kijana kuhusu vitendo vya Mullá Ḥusayn pale alipopokea zawadi? _______________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

15. Eleza katika maneno yako mwenyewe kile Mullá Ḥusayn alichomwambia mwanafunzi kutoka Núr pale alipokuwa anamuaga.

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Báb humtaja Bahá'u'lláh kama "Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha". Maandiko ya Báb, kikiwemo Kitabu Kitakatifu kabisa Chake, Bayán, kina marejeo mengi mno yanayomsifu Yule ambaye Mungu atamdhihirisha. Hapo chini ni mateuzi machache tu kutoka Maandiko ya Báb kukupa fununu ya Daraja la Bahá'u'lláh na uhusiano kati ya Wadhihirishaji Pacha.

> **"Na ujue kwa hakika kwamba kwa Paradiso inamaanishwa utambuzi wa, na utii kwa Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha; na kwa moto, uenzi wa roho zile ambazo zingeshindwa kumtii Yeye au kujiweka chini ya ridhaa Yake njema."[16]**

> **". . . takasa sikio lako ili usisikie mtajo wowote kando ya Mungu, na takasa jicho lako ili lisione kingine ila Mungu, na dhamira yako ili isione chochote kile kuliko Mungu, na ulimi wako ili usitangaze chochote ila Mungu, na mkono wako ili usiandike chochote kile isipokuwa maneno ya Mungu, na ujuzi wako ili isielewe chochote ila Mungu, na moyo wako ili usifikirie tamaa yoyote ila Mungu, na hali kadhalika takasa vitendo vyako vyote na shughuli zako ili uweze kulelewa katika paradiso ya upendo mtupu, na pengine utaweza kufikia machoni pa Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha, ukipambwa kwa usafi ambao Yeye huupenda sana, na utakasike kutoka yeyote yule ambaye amekengeuka kutoka Kwake na hamsaidii Yeye."[17]**

> **"Sema, kwa ukweli, ridhaa njema ya Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha ni ridhaa njema ya Mungu, wakati maudhi kwa Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha siyo kingine ila maudhi kwa Mungu."[18]**

1. Kwa nani "Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha" hurejelea? ___________________

2. Báb anawahimiza wafuasi wake kujiandaa wenyewe ili wakubaliwe mbele ya Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha. Yeye aliwaambia wafanye nini?

_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________

3. Chagua teuzi mojawapo kati ya mateuzi ya hapo juu na ulikariri.

## SEHEMU YA 5

Tangu Bahá'u'lláh alipoushuhudia ukweli wa Ufunuo wa Báb, Yeye aliinuka kuutangaza. Ziara ya kwanza aliyoifanya kufundisha Imani mpya ilikuwa ni nyumbani kwa

babu Zake huko Núr, katika jimbo la Mázindarán. Huko alikwenda kwenye kaya ya ukoo Wake katika kijiji cha Tákur.

Habari za kuwasili kwa Bahá'u'lláh huko Tákur zilienea haraka katika mkoa wote. Wengi kati ya maafisa wa sehemu hizo na waheshimiwa walikuja kumwamkia na wakati huo huo kupata habari za Mfalme kutoka Kwake, za baraza lake na masuala ya nchi. Lakini Bahá'u'lláh alipokea maswali yao kwa shauku kidogo tu. Yeye kwa haraka alibadilisha mazungumzo na kuanza kuelezea, kwa ufasaha kabisa, ujumbe uliotangazwa na Báb. Maneno Yake yalikuwa ya kusadikisha mno na hoja zake thabiti kabisa kwamba wote walishangaa. Wale waliomsikiliza walishangazwa kwamba mtu mwenye daraja Lake la juu, angevutiwa sana na masuala ambayo kwa kawaida yalihusu makasisi na viongozi wa dini. Shauku Yake na kina cha ujuzi Wake punde tu vilivutia idadi kubwa ya watu kwa Hoja ya Báb, wakiwemo watu mashuhuri na watu wa ukoo Wake mwenyewe. Hakuna yeyote aliyefika mbele Yake angeweza kumudu mvuto wa maneno Yake matamu au kuthubutu kupinga ukweli wa kauli Yake, hakuna yeyote isipokuwa mjomba Wake mwenyewe.

Mjomba huyu alifanya kila jambo lililowezekana kumuaibisha Bahá'u'lláh na ukweli wa Ujumbe ambao alikuwa ameuleta. Alipotambua asingeweza kufanya hivyo, alikwenda kwa kasisi mashuhuri wa Kiislamu na kuomba msaada wake. Alilalamika kwamba Bahá'u'lláh alikuja Núr na, ingawa hakuwa miongoni mwa makasisi, alikuwa akizungumza masuala ya kidini. Alimuonya mwanazuoni huyo kwamba kila mtu aliyekwenda mbele ya Bahá'u'lláh alivutiwa na uchawi Wake na alikumbwa na nguvu ya maneno Yake. "Sijui kama ni mchawi," yeye alisema, "au kama anachanganya pamoja na chai dawa fulani ya ajabu ambayo humfanya kila mtu anayekunywa chai hiyo kuathiriwa na uchawi wake."[19]

Akijua kwamba asingeweza kamwe kufanikiwa kushindana na Bahá'u'lláh, yule mwanazuoni alipuuzia maombi ya mjomba huyo. Lakini Ujumbe wa Báb uliendelea kuenea kama moto wa pori, katika wilaya nzima. Wakiingiwa na hofu, wafuasi wa mwanazuoni yule walianza kumshinikiza kuchukua hatua ya namna fulani, na hatimaye aliamua kuwatuma wanafunzi wake wawili wenye weledi mkubwa kumtembelea Bahá'u'lláh na kuchunguza asili ya Ujumbe ambao alikuwa akiueneza. Hii ni hadithi ya kile kilichotokea, pale wale wawakilishi wawili walipokwenda mbele ya Bahá'u'lláh.

Walipowasili huko Tákur na kuambiwa kwamba Bahá'u'lláh ameondoka kwenda kwenye nyumba Yake ya majira ya baridi, wawakilishi wa mwanazuoni huyo waliamua kumfuata huko. Walipowasili, walimkuta Bahá'u'lláh akishughulika na kufunua fasiri juu ya mojawapo ya sura za Kurani. Walipoketi na kumsikiliza, walivutiwa mno na ufasaha wa maelezo Yake na namna isiyo ya kawaida aliyokuwa akizungumza. Mmojawapo wa wawakilishi hao, akishindwa kujizuia, aliinuka kutoka kwenye kiti chake na alikwenda nyuma ya chumba hicho na alisimama wima kando ya mlango, katika hali ya heshima na kunyenyekea, Huku akitetemeka na macho yakiwa yamejaa machozi, alimuambia mwenzi wake: "Sina uwezo wa kumhoji Bahá'u'lláh. Maswali ambayo niliyapanga kumuuliza yametoweka ghafla kutoka kwenye akili yangu. Una uhuru kuendelea na uchunguzi wako au kurudi peke yako kwa mwalimu wetu na kumjulisha juu ya hali ambamo nimejikuta mwenyewe. Mwambie kwa niaba yangu kwamba siwezi kamwe kurudi tena kwake. Siwezi kukiacha tena kizingiti hiki." Lakini yule mwakilishi mwingine vilevile alivutiwa na maneno ya Bahá'u'lláh na alifuata mfano wa rafiki yake. "Nimeacha kumtambua mwalimu wangu," lilikuwa jibu lake. "Katika muda huu huu, nimeapa kwa Mungu kujitolea siku zilizobaki za maisha yangu kwa kumtumikia Bahá'u'lláh, Bwana wangu wa kweli na wa pekee."[20]

Habari za kubadilika kwa wanafunzi wa yule mwanazuoni zilienea kwa haraka miongoni mwa watu wa Núr. Watu mashuhuri, maafisa wa serikali, viongozi wa dini, wafanya biashara na wakulima walisongamana kwenye uwepo wa Bahá'u'lláh. Mamia waliletwa chini ya bendera ya Hoja ya Bab. Hakuna yeyote, walakini, isipokuwa Bahá'u'lláh, alijua kwamba mateso mabaya sana yangefuata punde tu, mateso ambayo yangeingoa kwa mizizi yao yenyewe mingi ya miche hii mipya na michanga.

1. Bahá'u'lláh alifanya nini baada ya kushuhudia juu ya ukweli wa ufunuo wa Báb? __

_______________________________________________

2. Bahá'u'lláh alipokelewa vipi na wakazi wa Núr? _______________________

_______________________________________________

3. Kwa nini baadhi ya watu walishangazwa na jinsi ambavyo Bahá'u'lláh alijibu maswali yao? _______________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

4. Mjomba Wake Bahá'u'lláh alifanyaje, Bahá'u'lláh alipoanza kutangaza Hoja ya Báb?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

5. Kwa nini kasisi msomi maarufu wa Kiislamu alipuuzia ombi la mjomba wa Bahá'u'lláh? _______________________________________

_______________________________________________

6. Yule kasisi aliamua kufanya nini hatimaye pale aliposhinikizwa na wafuasi wake?

_______________________________________________

_______________________________________________

7. Simulia katika maneno yako mwenyewe hadithi ya wale wawakilishi wawili wa yule mwanazuoni ambao walikwenda mbele ya Bahá'u'lláh.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

8. Je, ubadilikaji wa wawakilishi hawa wawili ulikuwa na matokeo gani juu ya maendeleo ya Hoja ya Báb huko Núr? ______________________________________________

## SEHEMU YA 6

Kile ambacho Bahá'u'lláh alifanya katika wilaya ya Núr, ndicho anachotuambia tufanye — kuinuka na kufundisha Hoja ya Mungu. Hebu basi tujifunze na tutafakari juu ya maneno yafuatayo ya Bahá'u'lláh, tukikumbuka kwamba baada ya kuukubali Ufunuo wa Báb, kitendo Chake cha kwanza kilikuwa kuinuka na kufundisha mamia na mamia ya roho.

> **"Ewe msafiri katika njia ya Mungu! Twaa sehemu yako ya bahari kuu ya neema Yake, na usijinyime mwenyewe vitu vile vilivyofichwa katika vina vyake. Uwe miongoni mwa wale ambao wameshiriki katika hazina zake. Tone la umande kutoka bahari hii kuu, kama lingemwagwa juu ya vitu vyote viliyomo mbinguni na duniani, lingetosheleza kuvitajirisha kwa fadhila za Mungu, Mwenyezi, Mjua-yote, Mwenye Hekima Kabisa. Kwa mikono ya kujikana teka kutoka maji yake yatiayo uzima, na unyunyizie kwayo viumbe vyote, ili viweze kutakaswa kutoka vizuizi vyote vya kibinadamu na viweze kukaribia kiti chenye nguvu cha Mungu, Mahali hapa patukuzwapo na paangavu.**

> **"Usihuzunike kama utatenda wewe peke yako. Acha Mungu awe atoshelezaye vyote kwako. Zungumza kwa ndani na Roho Yake, na uwe kati ya wale wenye shukurani. Tangaza Hoja ya Bwana wako kwa wote walio mbinguni na duniani. Kama mtu yeyote ataitika mwito wako, muwekee wazi mbele yake lulu za hekima**

**ya Bwana, Mungu wako, ambazo Roho Yake imekushushia wewe, na uwe miongoni mwa wale ambao kwa hakika huamini. Na kama yeyote akiikataa zawadi yako, geukia mbali kutoka kwake, na weka tumaini na imani kwa Bwana, Mungu wako, Bwana wa malimwengu yote."**[21]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Bahá'u'lláh anatuambia kutwaa sehemu yetu ______________________________ ________________________ .

   b. Tusijinyime wenyewe __________________________________________________ __________________________________________ .

   c. Tone la umande la bahari ya neema Yake, kama lingemwagwa juu ya vyote viliyomo mbinguni na duniani, lingetosheleza ku __________________________ ______________________________________________________________________ ___________________________________________ .

   d. Tunaambiwa kuteka _________________________ na ______________________ , kunyunyizia _________________________________________________________ .

   e. Tusihuzunike kama ____________________________________________________ .

   f. Tunapaswa kuongea ___________________________________________________ na kuwa ____________________________ .

   g. Tunapaswa kutangaza _________________________________________________ __________________________________________ .

   h. Kama mtu yeyote akiitika wito wetu, Bahá'u'lláh anatuambia ku _________ ______________________________________________________________________ __________________________________________________ .

   i. Kama mtu yeyote akiikataa zawadi yetu, tunapaswa __________________ ______________________________________________________________________ ______________________________________________________________________ .

## SEHEMU YA 7

Ufunuo Mtukufu ni endelevu. Mungu hufunua Mapenzi Yake hatua kwa hatua kupitia Wadhihirishaji Wake Ambao hujitokeza wakati baada ya wakati kadiri jamii ya wanadamu inavyokua kutoka hatua moja hadi nyingine. Huku akithibitisha baadhi ya kweli za lazima, kila Mdhihirishaji huleta seti mpya ya sheria na amri zinazolingana na uwezo wa jamii ya wanadamu na hubatilisha nyingine, ambazo hazihitajiki tena, zilizoletwa na Yule Aliyetangulia kabla Yake. Walakini inaweza kuwa vigumu kwa watu kuacha nyuma ya siku zilizopita, na

aghalabu mwanzoni hata wanafunzi Wake wa karibu kabisa, hawawezi kuufahamu maana kamili ya Ufunuo Wake. Wao huendelea kushikilia desturi na mazoea ya kidini ambavyo vizazi vimefuata kwa mamia ya miaka. Ni baada ya muda kupita huanza kuelewa kuwa Mdhihirishaji mpya ameweka sheria mpya kwa ajili ya hatua inayofuata ya ukuaji wa jamii ya wanadamu.

Huu ulikuwa ukweli kuhusu Ufunuo wa Báb. Waislamu, ambao miongoni mwao Báb alitokea, waliamini kwamba hakuna hata "herufi" moja kutoka Mafundisho ya Mtume Muḥammad ingeweza kubadilishwa hadi mwisho wa ulimwengu. Kwa hiyo, Báb aliruhusu Ujumbe Wake kamili kujulishwa polepole tu. Katika miaka ya mwanzo ya Utume Wake, hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanywa katika sheria za Uislamu. Lakini, kama ujuavyo, baadaye alipokuwa amefungwa katika ng'ome ya Máh-Kú, Báb alifunua idadi mpya ya sheria katika Bayán ya Kiajemi. Sasa wakati ulikuwa umewadia kwa wafuasi Wake kuachana kabisa na ya wakati uliopita na kutangaza Daraja Lake la kweli. Hili lilifanyika katika Mkutano wa Badasht.

Badasht ni kijiji kilicho mbali kidogo kutoka Ṭihrán katika sehemu ya kaskazini mashariki ya nchi hiyo. Mkutano wa Badasht lilifanywa katika mwezi Julai 1848. Wafuasi themanini na moja mashuhuri kabisa wa Báb walikuja pamoja katika mkutanno huo. Washiriki wakuu walikuwa Bahá'u'lláh, Quddús na Ṭáhirih.

Ingawa hapo mwanzoni Bahá'u'lláh Alikuwa anaheshimika sana miongoni mwa Wabábí wenzake, ambao walitambua ujuzi Wake na hekima na walimtazama Yeye kwa ajili ya kupata mwongozo, katika mkutano huo ukuu Wake na ufahari vilidhihirika kwa kiwango kikubwa zaidi. Yeye alikodi bustani ambako Mkutano huo ulifanywa, na kwa siku ishirini na mbili, wote wale ambao walikuwa wamekusanyika walifurahia ukarimu Wake mkubwa. Kila siku Bahá'u'lláh alifunua Waraka mmoja wa kusomwa mbele ya waumini waliokusanyika. Alimpa kila mmoja jina jipya. Aliwapa Ṭáhirih na Quddús, majina ya heshima ambayo kwayo watajulikana katika historia nzima. Jina la heshima Ṭáhirih lina maana ya "Yule Msafi", na Quddús maana yake "Mtakatifu". Yeye Mwenyewe, kutoka wakati ule na kuendelea, angejulikana kwa jina la Bahá. Baadaye Báb alifunua Waraka maalum kwa kila mmoja miongoni mwa wale ambao walikuwa wamehudhuria mkutano huo, akiwaita kwa majina ambayo walikuwa wameyapokea kwenye tukio hilo.

Siku moja Bahá'u'lláh alikuwa amelala kitandani Mwake kwa ugomjwa, na kila mmoja alikusanyika mbele Yake. Ndipo, ghafla, Ṭáhirih, ambaye alifikiriwa kuwa kiini cha usafi na ubikira, alitokea mbele yao bila ushungi ambao, kwa mujibu wa itikadi za Waislamu huko Iran, wanawake wote iliwabidi kuvaa hadharani. Baadhi ya Wabábí waliokuwepo waliona kwamba alijiaibisha mwenyewe na Imani yao mpya. Quddús kwa udhahiri alikuwa ameghadhibishwa. Lakini Ṭáhirih, bila kutikiswa na aking'aa kwa furaha, aliwahutubia wenzi wake kwa ufasaha. Aliwaita kuachana na wakati uliopita — pamoja na itikadi zake za kidini, mila zake na taratibu. Mvutano uliotokea kati ya Quddús na Ṭáhirih ulitulizwa na Bahá'u'lláh kwa kuingilia kati. Wakati wachache wa wafuasi wa Báb waliiacha Imani kama matokeo ya tangazo hili, wengi walibakia imara na walijawa na shauku mpya. Bahá'u'lláh kwa umahiri alitumia tukio hilo kusherehekea mapambazuko ya Siku mpya. Ṭáhirih kwa kitendo chake cha ujasiri, alikuwa amepiga ile baragumu kutangaza mwisho wa ya kale na mwanzo wa Imani mpya.

Mkutano wa Badasht pia liliashiria mwanzo wa hatua ya ghasia kubwa kabisa katika ukuaji wa Imani ya Kibábí. Punde tu mateso ya wafuasi Wake yangefikia viwango vipya vya ukali, na wengi wangeitwa kwenye kifo cha ushuhidi. Ilikuwa kana kwamba mkutano huo

ulikuwa mkusanyiko wa kuagana, kutoka hapo wangekwenda kufanya vitendo vya ushujaa mkuu, na kuunganishwa tena tu katika Ufalme wa Abha.

Wale waliokuwepo kwenye mkutano waliondoka pamoja kwenda Mázindarán. Walakini walisipomama kupumzika nje ya kijiji kimoja, walishambuliwa na wakazi wa kijiji hicho ambao hawakujua kusudi lao la kweli. Wabábí walilazimika kukimbia na kutawanyika sehemu mbali mbali. Bahá'u'lláh aliendelea na safari Yake kuelekea Núr ya Mázindarán.

Habari za Mkutano wa Badas͟ht mara zilifika Ṭihrán, na mfalme na mawaziri wake walikuja kutambua matukio yaliyofanyika na nafasi ambayo Bahá'u'lláh alikuwa nayo katika mkutano huo. Mfalme, ambaye alikuwa dhaifu kutokana na maradhi ambayo baada ya muda mfupi yangechukua maisha yake, alishauriwa na waziri mkuu kuamuru Bahá'u'lláh akamatwe. Hivyo, amri ilipelekwa kwa mmojawapo wa maafisa wa Mázindarán, ikimuagiza kumkamata Bahá'u'lláh na kumleta katika mji mkuu. Ilitokea kwamba, ile amri ilifika siku moja kabla afisa huyo huyo angemfanyia tafrija Bahá'u'lláh ambaye alikuwa anampenda sana. Alifadhaisha sana na aliamua kutomuambia mtu yeyote. Siku iliyofuata habari zilifika Mázindarán kwamba mfalme alikuwa amekufa; amri ya kumkamata ikawa sio halali tena.

1. Mkutano wa Badas͟ht ulikuwa na kusudi gani? ______________________________

   ______________________________________________________________

2. Mkutano wa Badas͟ht ulifanyika lini? ______________________________

3. Mkutano wa Badas͟ht ulifanyika kwa siku ngapia? ______________________________

4. Wafasi wangapi wa Báb walihudhuria mkutano huo? ______________________________

5. Nani walikuwa washiriki wakuu? ______________________________

   ______________________________________________________________

6. Nani alikuwa Mtu wa muhimu kabisa miongoni mwa wale waliokuwepo? ________

7. Wadhifa wa "Ṭáhirih" una maana gani? ______________________________

8. Wadhifa wa "Quddús" una maana gani? ______________________________

9. Katika maneno yako mwenyewe, simulia matukio ambayo yaliyotokea siku ambayo Ṭáhirih alijitokeza bila ushungi katika mkutano.

   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________

10. Kitendo cha kishujaa cha Ṭáhirih katika mkutano kiliashiria nini? ______________

11. Serikali ilifanya nini ilipopokea habari za ule mkusanyiko wa Badasht? __________

12. Elieza nini kilitokea baada ya serikali kutoa amri ya kumkamata Bahá'u'lláh.

## SEHEMU YA 8

Mkutano wa Badasht uliweka alama ya kupukusa mambo ya zamani na kuchukua yale mapya. Fungu linalofuata kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá linaeleza jinsi, kutoka wakati hadi wakati tangu zamani, dini ya Mungu lazima ifanywe upya tena. Fikiria juu ya maana ya fungu hili kufuatana na yale ambayo umekwisha jifunza juu ya Mkutano wa Badasht.

> **"Kutoka mbegu ya uhalisia dini imekua kama mti ambao umepata majani na matawi, maua na matunda. Baada ya muda mti huu umeingia katika hali ya kuoza. Majani, na maua yamesinyaa na kuharibika; mti umeathirika na umebaki bila matunda. Si busara kwa mtu kuushikilia mti wa zamani, akidai kuwa nguvu zake za uhai hazipungui, matunda yake hayana kifani, uwepo wake ni wa milele. Mbegu ya uhalisia lazima ipandwe upya katika mioyo ya watu ili kwamba mti mpya uweze kuota kutoka humo na matunda matakatifu mapya yaburudishe ulimwengu. Kwa njia hii mataifa na watu wanaotofautiana katika dini sasa, wataletwa kwenye umoja, uigaji utaachwa, na udugu wa wote katika uhalisia wenyewe utasitawishwa. Vita na ugomvi vitaisha miongoni mwa jamii ya wanadamu; wote watapatanishwa kama watumishi wa Mungu. Kwa kuwa wote**

**wanakingwa chini ya mti wa majaliwa Yake na rehema. Mungu ni mwema kwa wote; Yeye ni Mpaji wa baraka kwa wote sawasawa, kama vile Yesu Kristo alivyotamka kwamba Mungu 'hutuma mvua kwa wenye haki na wasio na haki' — ndio kusema kwamba, rehema ya Mungu ni ya wote. Jamii nzima ya binadamu ipo chini ya ulinzi wa upendo na fadhila Yake, na wote amewaonesha njia ya uongozi na maendeleo."**[22]

## SEHEMU YA 9

Náṣiri'd-Dín Sháh, mfalme ambaye alipanda kwenye kiti cha enzi mnamo mwaka 1848, alikuwa katili zaidi kuliko baba yake, mfalme aliyetangulia. Kutoka mwanzo wa utawala wake, mateso ya Wabábí yaliongezeka mno. Báb Mwenyewe aliuawa kama shahidi mnamo mwezi Julai 1850 huko Tabríz. Wafuasi Wake waliodhulumiwa, ambao walishuhudia vifo vya huzuni vya maelfu ya waumini wenzao, sasa walikuwa wamempoteza Mpendwa kabisa wa mioyo yao. Katika fikira zao, wengi walimlaumu mfalme kwa ajili ya ukatili uliolundikwa juu yao kwa miaka mingi iliyopita. Lakini licha ya hisia hizi, waliendelea kuwa watakia mema kwa serikali na watu. Nguvu zao zilielekezwa kwenye kueneza Imani mpya kupitia nguvu za matendo mema na hoja za kuridhisha. Kulikuwepo, walakini, kundi dogo, lililosukumwa na hasira kali, ambalo lililokuwa wana mawazo ya hatari. Katika hali ya kukata tamaa, hawa wajinga wachache waliamini kwamba wangeweza kubadilisha hatima ya jamii ya Kibábí kwa kuushambulia udhalimu kwenye mizizi yake. Walianza kupanga njama za kumuua Mfalme.

Makusudi ya kikundi hicho yaliwasilishwa kwa Bahá'u'lláh na mmoja wa viongozi wake. Bahá'u'lláh alimshauri katika maneno dhahiri kabisa kwamba waache huo mpango wao. Aliwaonya kwamba tendo kama hilo lingeleta maafa mapya kwa wafuasi wa Báb ambao tayari walikuwa wamepatishwa huzuni. Lakini wale waliopanga njama walikuwa katika hali ya uchungu mkubwa, na moto wa kulipiza kisasi uliwaka kwa nguvu sana mioyoni mwao, kwamba hata ushauri wa Bahá'u'lláh haukuweza kuwazuia. Waliendelea kufanya tendo ambalo daima litafikiriwa kuwa doa kwenye kurasa za historia ya Kibábí, ambayo vinginevyo ilikuwa imepambwa na vitendo visafi, visivyo na ubinafsi na vya kishujaa.

Mnamo tarehe 15 Augusti 1852, mfalme aliyaacha makazi yake ya majira ya joto karibu na Ṭihrán akiwa amepanda farasi kwenda katika matembezi yake ya asubuhi. Mlinzi wake binafsi alitembea hatuta chache mbele yake, hewa ilikuwa shwari, na mambo yote yalikuwa mazuri. Halafu, akimshangaza kila mmoja, kijana mmoja, aliyekuwa akingojea kando ya barabara akijifanya kuwa mtazamaji mwenye ombi alilotaka kumpa Mfalme, alijaribu kumuua mfalme. Mtu huyu ambaye alitarajia kuwa muuaji, alikuwa mjinga mno kwamba bastola aliyotumia ilikuwa na risasi ndogo ambazo zilikuwa hazifai kabisa kwa kusudi alilodhamiria. Mfalme alijeruhiwa kidogo tu, lakini ghadhabu iliyosababishwa na jaribio juu ya maisha yake iliwapa maadui wa Imani fursa ya kuwachochea watu kufanya vitendo vya ukatili visivyofikirika dhidi ya Wabábí.

Yule kijana mwenye nuksi, aliyemfyatulia risasi mfalme aliuawa papo hapo; mwili wake ulifungwa kwenye mkia wa nyumbu na kukokotwa njia nzima hadi Ṭihrán, ambako ulikatwa kuwa vipande viwili na kuning'inizwa kwa ajili ya watu kuuangalia. Risasi iliyoyeyushwa ilimiminwa ndani ya koo la mwenzake — hii ilikuwa tu baada ya kuteswa kwa ukatili kwanza, lakini alikuwa amekataa kutoa majina ya yeyote miongoni mwa rafiki zake. Mwenziwe mwingine alivuliwa nguo zake, aliwekewa mishumaa iliyowashwa ndani ya

matundu yaliyotobolewa kwenye mwili wake, na alitembezwa mbele ya umati wa watu ambao walimzomea na kumlaani.

Kilichofuata hakiwezi kuelezeka kwa maneno. Serikali, makasisi, na wasaidizi wao wajinga waliinuka kuwateketeza Wabábí. Malango ya kuingilia mjini yalifungwa, na hakuna mtu aliruhusiwa kuondoka bila kuulizwa. Wabábí walitasakwa nyumba kwa nyumba, walikamatwa na kuuawa kwa ukatili wa kutisha, ambao hauwezi kuelezwa katika kurasa hizi.

Mnamo siku ile ambapo lilipofanyika jaribio juu ya maisha ya mfalme, Bahá'u'lláh alikuwa ni mgeni wa ndugu wa waziri mkuu katika kijiji jirani na Ṭihrán. Habari za janga hilo mara zilimfikia, na alishauriwa ajifiche hadi hapo dhoruba itakapopita. Mama yake mfalme alimlaumu Bahá'u'lláh kwa ajili ya jaribio juu ya maisha ya mwanae na alidai akamatwe. Lakini Bahá'u'lláh alikataa kwenda kujificha; badala yake, siku iliyofuata, alipanda farasi Wake na kwenda kuelekea kwenye makao makuu ya mfalme. Mfalme na baraza lake walishangazwa walipopata habari juu ya kukaribia kwa Bahá'u'lláh. Ingewezekanaje kwa mtu ambaye anatuhumiwa kwa kosa la kutisha kama hilo, badala ya kukimbilia mbali, alipanda farasi kwa kujiamini, na kuelekea kwenye hatari? Mfalme mara moja aliamuru kukamatwa kwa Bahá'u'lláh. Jitihada za baadhi ya marafiki Zake ambao walijaribu kumtafutia kimbilio katika nyumba ya waziri mkuu zilishindwa. Alikamatwa katika kijiji cha Shimírán, kama kilometa 30 hivi kutoka mji mkuu, na alitiwa katika minyororo.

Kwa miguu peku na akiachwa wazi chini ya mionzi mikali ya jua la katikati ya kiangazi, Bahá'u'lláh aliletwa kutoka Shimírán hadi Ṭihrán. Umati ambao waliambiwa kwamba Yeye alikuwa adui wa mfalme wao, walimpigia kelele za matusi njia nzima. Hadithi ya yule mwanamke mzee ambaye alitaka kumtupia jiwe Bahá'u'lláh, inaeleza wazimu wa kundi hilo katika siku hiyo na huonyesha upendo ambao uliokuwa ndani ya moyo Wake alipokuwa anakabiliana na maafa ya kuhuzunisha kabisa.

Alipokuwa anakaribia shimo ambako angefungiwa, mwanamke mzee na mnyonge alionekana akijilazimisha kupita katika kundi hilo akiwa na jiwe mkononi mwake. Akiwa mwenye dhamira na ushupavu wa imani kali ambavyo wanawake wachache wa rika yake wangeweza kuthubutu. Mwili wake wote ulitetemeka kwa ghadhabu. Alisonga mbele na kuinua mkono wake akijitayarisha kutupa jiwe lake. "Nawaomba," aliwasihi, wakati alivyokuwa akiwakimbilia wale ambao walikuwa wakimuongoza Bahá'u'lláh kwenye shimo hilo, "nipeni nafasi kumtupia jiwe langu usoni mwake!" "Msimwache mwanamke huyu kuvunjwa moyo," yalikuwa maneno ya Bahá'u'lláh kwa walinzi wake, alipomuona akikurupuka kumuelekea Yeye. "Msimnyime kile anachofikiri kama kitendo stahiki mbele ya uoni wa Mungu."[23]

1. Mfalme aliyepanda kiti cha enzi huko Uajemi mnamo mwaka 1848 aliitwa nani? __

   ____________________________________________________________

2. Kupanda kwa Náṣiri'd-Dín Sháh juu ya kiti cha enzi kulikuwa na athari gani juu ya vitendo walivyofanyiwa Wabábí? ________________________________

   ____________________________________________________________

3. Wabábí kwa ujumla wanajihisije baada ya kifo cha kishahidi cha Báb? __________

   ____________________________________________________________

4. Kundi lilikuwa linadhamiria kumwua mfalme lilikuwa katika hali gani kiakili? ____
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

5. Bahá’u’lláh alimwambiaje kiongozi wa kundi hilo pindi alipopata habari za kusudi lao?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

6. Jaribio juu ya maisha ya mfalme lilitokea mnamo tarehe ngapi? ________________

7. Ni nini ilikuwa hatima ya wale ambao walidiriki mauaji hayo? _________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

8. Je, lile jaribio la mauaji lilikuwa na matokeo gani juu ya jumuiya ya Wabábí?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

9. Je, Bahá’u’lláh alikuwa wapi alipopata habari juu ya jaribio juu ya maisha ya mfalme?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

10. Je, Bahá’u’lláh alifanya nini alipopokea habari za jaribio la mauaji? _____________
______________________________________________________________________

11. Je, Bahá’u’lláh Alikamatwa katika kijiji gani? ______________________________

12. Maadam Bahá'u'lláh hakuwa mnyonge mbele ya maadui zake, kwa nini basi unafikiri Alijiruhusu Mwenyewe kukamatwa, akijua fika hatari aliyokuwa Akienda kukabiliana nayo? ____________________

____________________

____________________

13. Bahá'u'lláh aliletwa kutoka Shimírán hadi Ṭihrán katika hali gani? ____________________

____________________

____________________

14. Katika maneno yako mwenyewe, simulia hadithi ya yule mwanamke mzee ambaye alitaka kumtupia jiwe Bahá'u'lláh alipokuwa akiongozwa kwenye lile shimo na walinzi. Hadithi hii hudhihirisha nini?

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

## SEHEMU YA 10

Katika maisha Yake yote, Bahá'u'lláh alizungukwa na maadui wakitafuta kumdhuru. Lakini kamwe hakujaribu kujificha Mwenyewe; kamwe hakujilinda Mwenyewe. Kinyume chake, wakati wote Yeye alikuwa akionekana mbele ya macho ya watu na alihimili kwa shwari na utulivu mashabulio ya wale ambao walimpinga. Ingawa walidhamiria kuuzima mwangaza Wake, walishindwa kufanya hivyo, na siku hadi siku utukufu Wake ulizidi kuwa mwangavu zaidi.

**“Hata kwa kitambo kidogo Mdhulimiwa huyu kamwe hajapata kujificha Mwenyewe. Bali wakati wote Yeye ameendelea kuwa thabiti na kuonekana mbele ya macho ya watu wote. Kamwe hatutarudi nyuma, wala hatutatafuta kukimbia. Kwa kweli ni wale watu wapumbavu wanaokimbia kutoka machoni Petu. . . . Mungu asifiwe! Hoja ambayo Mdhulumiwa huyu ni Mchukuzi wake imesimama juu mno kama mbingu na hung’aa kwa wangavu kama jua. Maficho hayana njia katika daraja hii, wala hakuna nafasi kwa ajili ya hofu wala ukimya.”[24]**

**“Akiwa amefunuliwa na wazi, Mdhulumiwa huyu, wakati wote, ametangaza mbele ya watu wote wa ulimwengu kile ambacho kitasaidia kama ufunguo wa kufungua milango ya sayansi, ya sanaa, ya elimu, ya hali njema, ya usitawi na ukwasi. Si uovu uliolazimishwa na wadhalimu haujafanikiwa kuinyamazisha sauti kali ya Kalamu Iliyotukuka Kabisa,wala mashaka ya wapotovu na wachochezi yameweza kumzuia Yeye kufunua Neno Lililotukuka Kabisa.”[25]**

Eleza katika maneno yako mwenyewe jinsi sisi tunapofanya kazi ya kutetea Hoja ya Bahá’u’lláh, tunavyopaswa kufanya mbele ya majaribu.

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Síyáh-Chál, jina la gereza ambako Bahá’u’lláh alipelekwa siku ile ya maafa mnamo mwaka 1852, lina maana ya “shimo jeusi”. Mwanzoni lilikuwa hodhi ya maji kwa ajili ya mojawapo ya mahamamu huko Ṭihrán, wakati huo lilikuwa gereza la ardhini ambamo wahalifu wabaya kabisa walifungiwa.

Kulifikia gereza hilo, mtu alipitishwa katika njia nyembamba yenye giza zito na halafu alishuka ngazi tatu zilizokuwa wima. Gereza hilo lilikuwa limefunikwa na giza zito, ilikuwepo baridi ya barafu, sakafu ilifunikwa na uchafu na wadudu wanaotambaa. Bahá’u’lláh mwenyewe alieleza hali mbaya sana ya mahali alikofungiwa:

**“Tulipofika pale, kwanza Sisi tulipelekwa kupitia katika njia nyembamba yenye giza totoro na halafu Tulishuka ngazi tatu zilizokuwa wima hadi tukafika mahali pa kifungo Chetu. Shimo lilikuwa gizani na wafungwa wenzetu takriban watu mia moja na hamsini: wezi, wauaji na maharamia. Ingawa tulisongamana hapakuwepo mlango wowote wa kutokea isipokuwa ile njia Sisi tulioitumia kuingia. Hakuna kalamu inayoweza kueleza hali ya mahali hapo, wala ulimi wowote kueleza harufu mbaya mno ya humo. Wengi wa watu hawa, hawakuwa**

**na nguo wala matandiko. Mungu peke Yake anajua kilichotusibu Sisi ndani ya mahali pale palipokuwa pananuka na pa kuhuzunisha!”[26]**

Katika mazingira haya ya kikatili, Bahá’u’lláh na idadi ya Wabábí, walifungwa na mfalme. Miguu ya Bahá’u’lláh iliwekwa ndani ya kiunzi cha miti na mnyororo mzito wenye uzito wa kama kilo 50 hivi ulizungushiwa shingoni Mwake. Kwa siku tatu za kwanza usiku na mchana hawakupewa chakula chochote wala maji. Familia ya Bahá’u’lláh ilitayarisha chakula kwa ajili Yake na kuwaomba wale walinzi kumpelekea. Ingawa mwanzoni walikataa, hatimaye walikubali maombi yao. Lakini, hata baada ya hayo, hakuna aliyeweza kuwa na uhakika kwamba chakula hicho kilimfikia au kama angekubali kukila wakati wafungwa Wenzake walikuwa na njaa.

Bahá’u’lláh na Wenzake, pia wakiwa katika viunzi vya miti na minyororo, wote walibanana katika chumba kimoja kidogo. Walikuwa wamewekwa katika safu mbili, wakitazamana. Bahá’u’lláh aliwafundisha kukariri aya fulani ambazo, kila usiku, waliziimba kwa juhudi kubwa. “Mungu ananitosheleza mimi; Yeye kwa hakika ni Mtoshelezi-kabisa,” safu moja iliimba, na nyingine ilijibu: “Kwake Yeye acha waaminio waamini.” Wakati wa saa za mapema za asubuhi, kibwagizo cha sauti zao zenye furaha kiliweza kusikika. Sauti yao tamu ilikuwa yenye nguvu mno kiasi kwamba iliyafikia masikio ya mfalme, ambaye jumba lake halikuwa mbali kutoka Síyáh-Chál. “Sauti hii ina maana gani?” ilitaarifiwa kuwa aliuliza. “Ni wimbo ambao Wabábí wanauimba gerezani mwao,”[27] lilikuwa jibu. Mfalme alinyamaza.

Kila siku askari magereza, wangeingia katika chumba gereza, na waliita jina la mmojawapo wa Wabábí, wakimuamuru kuinuka na kuwafuata hadi chini ya kiunzi cha kunyongea. Kwa shauku, yule mwenye jina hilo aliitikia wito! Minyororo yake ikiondolewa, angeruka na, katika hali ya furaha isiyozuilika, angemsogelea Bahá’u’lláh na kumkumbatia. Halafu angemkumbatia kila mmoja kati ya wafungwa wenzake na angetoka nje, kwa moyo uliojawa na matumaini na furaha, kukutana na kifo kilichomgojea. Mara baada ya kifo cha kishahidi cha kila mmoja wa roho hizi shujaa, yule muuaji, ambaye alikuwa ameanza kumpenda Bahá’u’lláh angekuja kwake na kumuarifu juu ya hali ya kifo cha shahidi huyo, na juu ya furaha ambayo kwayo alivumilia hadi mwisho kabisa, maumivu aliyopatishwa.

1. Jela ambamo Bahá’u’lláh alifungiwa linaitwaje? ______________________________

______________________________________________________________________

2. Ni nini maana ya “Síyáh-Chál”? ____________________________________________

3. Síyáh-Chál mwanzoni ilitumiwa kwa kazi gani? ______________________________

______________________________________________________________________

4. Elezea hali ya Síyáh-Chál.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

5. Bahá'u'lláh alipowasili huko Síyáh-Chál, kitu gani kilizungushiwa shingoni Mwake?

6. Nini kilifungiwa miguuni Mwake?

7. Bahá'u'lláh na wenzake waliwekwaje katika chumba chao cha gereza?

8. Bahá'u'lláh aliwafundisha kufanya nini?

9. Je, safu moja ya Wabábí ingeimba nini usiku mzima?

10. Je, safu nyingine ingeitikiaje?

11. Je kuimba kwao kulikuwa na matokeo gani juu ya mfalme?

12. Kila siku wale maaskari gereza walikuja kwenye chumba ambako Bahá'u'lláh na wenzake walifungwa na waliita jina la Mbábí mmoja. Katika maneno yako mwenyewe, elezea kingetokea nini baada ya hapo.

13. Licha ya hali mbaya sana ya kifungo chao unafikiri kwa nini Wabábí walikuwa wenye kujawa na furaha? ______

## SEHEMU YA 12

Kuna wazo la kina sana ambalo kila mwanafunzi wa historia ya Kibahá'í sharti alifahamu, yaani, kwamba Hoja ya Mungu huendelea mbele kupitia mfululizo wa hali ya hatari na ushindi. Wakati wowote nguvu za ujinga, udhalimu, ukatili, na ushupabu wa kidini yanaposhambulia Hoja, yakisababisha hatari, nguvu sambamba za kiasili huachiliwa, na kuushinda uovu, na kuisukuma Hoja mbele kupata ushindi mwingine, ambao mapema au baadaye husababisha upinzani mwingine, ambao haukuwahi kufikiriwa kabla, ambao tena husababisha uachiliaji wa kiwango kingine cha uwezo wake Mtakatifu. Hivyo ndivyo Hoja ya Mungu inavyojongea kutoka hali ya hatari hadi kwenye ushindi na tena kwenye hatari na tena ushindi, na hakuna uwezo duniani unaoweza kuzuia mjongeo wake wa kwenda mbele.

Utume wa Báb tayari ulikuwa umeshafuata njia kama hiyo. Walakini mchunguzi wa kawaida angechukulia kuwa hali ya hatari ya wakati huu isingeweza kushindika: Báb alikuwa ameuawa kishahidi. Maelfu ya wafuasi Wake walikuwa wameuawa katika mauaji ya ukatili usioelezea. Mwanafunzi Wake bora kabisa alikuwa ameuawa kishahidi na Yule ambaye pekee angefufua matumaini alikuwa katika minyororo katika gereza la giza kabisa. Hatari kwa uhakika ilikuwa kubwa mno, lakini ule ushindi uliofuata ulikuwa mtukufu kabisa.

Huko Síyáh-Chál, Mungu alimjulisha Bahá'u'lláh ukuu wa Daraja Lake. Akiwa amefunikwa na utusitusi, akivuta hewa mbaya kabisa, miguu Yake ilkiwa katika viunzi, na shingo Yake ikielemewa na mnyororo mkubwa sana, Bahá'u'lláh alipokea dokezo la kwanza la ufunuo wa Mungu ndani ya roho Yake. Katika hali hizi za kutisha, ile "Roho Kuu Kabisa" ilijifunua yenyewe Kwake, ikimuamuru kuinuka na kunena Neno la Mungu.

Mara nyingi, Yeye angehisi kama kitu fulani kilitiririka kutoka utosi wa kichwa Chake hadi kifuani Mwake, kama maporomoko yenye nguvu yanavyoanguka juu ya ardhi kutoka kilele cha mlima mrefu. Yeye Alimuona Mwanamwali wa Mbinguni akining'inizwa mbele Yake, akiongea na nafsi Yake ya ndani na ya nje, akimtaja Yeye kama Mpenzi-Kabisa wa malimwengu, Uzuri wa Mungu, na nguvu ya enzi ya Mungu. Alihakikishiwa kwamba atafanywa mshindi kwa Yeye Mwenyewe na kwa Kalamu Yake, na kwa msaada wa wale ambao Mungu atawainua.

Hivyo kutoka katika giza la Shimo Jeusi lilichomoza Jua la Ukweli. Ahadi ya Báb ilikuwa imetimizwa. Ufunuo wa Kibahá'í ulizaliwa. Lakini Bahá'u'lláh hakumfahamisha yeyote kilichokuwa kimetokea. Yeye angengojea saa iliyowekwa, iliyoamuriwa na Mungu, kuifanya Dhima Yake ijulikane.

1. Eleza katika maneno yako mwenyewe jinsi hali ya hatari ilivyo kuwa kubwa sana ambamo Jumuiya ya Kibábí ilijikuta yenyewe wakati wa kifungo cha Bahá'u'lláh.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

2. Ni ushindi gani ambao ulifuata hatari hii kubwa? ____________________

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

## SEHEMU YA 13

Jamii ya wanadamu ina bahati kwamba tukio hili la maana sana katika historia ya dini likiandikwa katika maneno ya Bahá'u'lláh Mwenyewe. Someni kifungu kutoka kwenye Maandiko Yake lililopo hapo chini na jaza nafasi katika sentensi zinazofuata kila kimoja.

Akijikumbusha jinsi Ufunuo wa Mungu ulivyomjaza roho Yake kwanza, Bahá'u'lláh anasema:

> **"Usiku mmoja, katika ndoto, maneno haya yaliyotukuka yalisikika katika kila upande: 'Hakika, Sisi tutakufanya Wewe mshindi kupitia Wewe mwenyewe na kwa Kalamu Yako. Usihuzunike kwa yale ambayo yamekupata, wala usiogope, kwa kuwa Wewe u usalama. Hivi punde Mungu atainua hazina za dunia — watu ambao watakusaidia Wewe kupitia Wewe Mwenyewe na kwa kupitia Jina Lako, ambalo kwalo Mungu ameihuisha mioyo ya wale ambao wamemtambua Yeye.'"**[28]

Katika fungu hili, Bahá'u'lláh anatuambia kwamba Usiku mmoja, katika ndoto, maneno haya yaliyotukuka yalisikika katika kila upande: 'Hakika, Sisi tutakufanya Wewe ________________ kupitia ________________ mwenyewe na kwa ________________ ______________ . Usihuzunike kwa yale ambayo ______________ , wala ______________ , kwa kuwa Wewe u ______________ . Hivi punde Mungu ____________________________ za dunia – ____________________ ambao watakusaidia ___________________ kupitia ____________________________ na kwa kupitia ___________________________ , ambalo kwalo Mungu ______________ mioyo ya wale ambao ______________ Yeye."

Katika fungu lingine Bahá'u'lláh anaelezea athari ya Ufunuo wa Mungu kwenye nafsi Yake:

> **"Katika siku zile nilipokuwa ndani ya gereza la Ṭihrán, ingawa uzito wenye kuumiza wa minyororo, na hewa iliyojaa harufu mbaya viliniruhusu usingizi kidogo tu, hata hivyo katika dakika chache za kusinzia, nilihisi kama kitu kilitiririka kutoka utosi wa kichwa Changu hadi kifuani Mwangu, hata kama vile maporomoko makubwa mno ambayo hujiporomosha yenyewe juu ya ardhi kutoka kilele cha mlima mrefu sana. Kila kiungo cha mwili Wangu, kama matokeo, kiliwaka moto. Katika dakika hizo ulimi Wangu ulitamka yale ambayo hakuna mtu angeweza kuvumilia kuyasikia."**[29]

Bahá'u'lláh anasema kwamba katika siku zile alipokuwa ndani ya ____________ la Ṭihrán, ingawa ______________ wenye ______________ wa ______________ , na hewa iliyojaa _________________ vilimruhusu ____________ kidogo tu, hata hivyo katika _____________ chache za ______________ , Alihisi kama kitu _____________ kutoka ____________ wa ________________________ hadi ____________ Mwake. Kama matokeo, kila kiungo cha mwili Wake ________________________ . Katika dakika hizo Bahá'u'lláh alitamka ____________ ambayo hakuna mtu ____________________________________ .

Tena katika kifungu kingine Yeye anaelezea jinsi Mwanamwali, akiwa alama ya "Roho Kuu Kabisa," alivyomtokea Yeye:

> **"Tulipokuwa tumezongwa na taabu nilisikia sauti ya ajabu kabisa, tamu kabisa, ikiita juu ya kichwa Changu. Nikigeuza uso Wangu, nilimuona Mwanamwali — mfano halisi wa kumbukumbu la jina la Bwana Wangu — akining'inizwa hewani mbele Yangu. Alikuwa mwenye furaha sana katika roho yake yenyewe kana kwamba wajihi wake uling'aa kwa pambo la ridhaa njema ya Mungu, na mashavu yake yalimetameta kwa wangavu wa Mwenye-rehema kabisa. Kati ya dunia na mbingu alikuwa akipaza wito ambao ulivutia mioyo na akili za watu. Alikuwa akiipasha nafsi Yangu ya ndani na ya nje pia habari ambazo zilifurahisha roho Yangu, na roho za watumishi waheshimiwao wa Mungu. Akionesha kidole chake kwenye kichwa Changu, yeye aliwahutubia wote walio mbinguni na wote walio duniani, akisema: 'Kwa Mungu! Huyu ndiye Mpenzi–Kabisa wa malimwengu, na bado hamfahamu. Huu ndio Uzuri wa Mungu miongoni mwenu, na nguvu za enzi Yake ndani yenu, kama mngeweza tu kuelewa.**

**Hili ni Fumbo la Mungu na Hazina Yake, Hoja ya Mungu na utukufu Wake kwa wote walio katika falme za Ufunuo na za muumbo, kama mngekua miongoni mwa wale wanaotambua.’”**[30]

Bahá’u’lláh anatuambia kwamba, Alipokuwa tumezongwa na taabu Yeye ______________________________ , ______________________ , ikiita juu ya kichwa Chake. Alipogeuza uso Wake, Bahá’u’lláh alimuona Mwanamwali akining’inia ____________ mbele ____________ . Uso wa Mwanamwali __________________ kwa ____________ la ___________________ ya ____________ , na mashavu yake yalimeremeta kwa ____________ wa _________________________ kabisa. Mwanamwali alikuwa akizipasha zote mbili nafsi Yake ya ____________ na ya ___________ habari ambazo zilifurahisha __________ Yake, na roho za ___________________ wa Mungu. Akionyesha kidole chake kwenye kichwa cha Bahá’u’lláh, yeye aliwahutubia wote walio ___________ na wote walio ___________ , akisema: “Kwa Mungu! Huyu ndiye ___________–___________ wa ___________ , na bado hamfahamu. Huu ndio _______________________ miongoni mwenu, na ______________ ___________ ndani yenu, kama mngeweza tu kuelewa. Hili ni ___________ la ___________ na ___________ Yake, ___________ ya ___________ na ___________ Wake kwa wote walio katika falme za ____________ na za ___________ , kama mngekua miongoni mwa wale wanaotambua.”

## SEHEMU YA 14

Wazo la hali ya hatari na ushindi ni muhimu mno kiasi kwamba inafaa kwako kusita katika wakati huu na kutafakari juu ya nguvu ya Hoja, ambayo inaweza kushinda kila kizuizi katika njia yake. Kukusaidia kufanya hivyo, inapendekezwa kwamba usome mateuzi hayo hapo chini — moja kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh na lingine kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi — na ujibu swali linalofuata.

**“Tazama jinsi gani katika Kipindi Kitakatifu hiki wale wasiofaa na wajinga wamefikiria kwa matumaini ya kijinga kwamba kwa njia kama vile mauaji ya kikatili, uporaji na uhamisho wao wangeweza kuizima Taa ambayo Mkono wa nguvu ya Mungu umeiwasha, au kufunika Nyota ya Mchana ya utukufu wa milele. Jinsi gani wanaonekana ka hawatambui kabisa ukweli huu kwamba taabu kama hizi ndio mafuta yanayoongeza nguvu ya mwali wa Taa hii! Hiyo ndivyo ulivyo uwezo wa ubadilishaji wa Mungu. Yeye hubadilisha chochote apendacho; Yeye kwa kweli ana uwezo juu ya vitu vyote.”**[31]

**“Hoja hii, kama kila Hoja Takatifu, haiwezi kusitawishwa ipasavyo isipokuwa ikikabiliana na kuzishinda kwa ushujaa zile nguvu zote za upinzani zinazo ishambulia. Historia ya Imani yenyewe ni uthibitisho wa kutosha wa jambo hilo. Majaribu na mateso daima yamekuwa, na yataendelea kuwa, fungu la wateule wa**

**Mungu. Lakini haya, wao sharti wayachukulie kama baraka ziliyofichwa, kwa kuwa kupitia humo imani yao itahuishwa, itatakaswa na kuimarishwa. Bahá'u'lláh hulinganisha majaribu yaumizayo kama haya, na mafuta yaongezayo nguvu ya taa ya Hoja ya Mungu."[32]**

Uelewa wa kwamba Imani huendelea mbele kupitia mfululizo wa hali ya hatari na ushindi itakusaidiaje wewe kuamua kutembea njia ya huduma kwa Hoja na kwa jamii ya wanadamu?

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 15

Wakati Bahá'u'lláh akiendelea kuwa katika minyororo huko Síyáh-Chál, maadui Wake walikuwa wakijishughulisha kupata hukumu Yake ya kifo kutoka kwa mfalme. Walakini, Bahá'u'lláh alipendwa na watu wakubwa kwa wadogo kadhalika na hasingeweza kuuawa kwa urahisi. Ushahidi ulihitajika ambao ungemhusisha Yeye na jaribio juu ya maisha ya mfalme. Kadiri walivyojaribu kupata ushahidi, ndivyo ilivyokuwa dhahiri zaidi kuwa Yeye alikuwa hana hatia kabisa. Waliposhindwa kupata hukumu ya mauaji Yake, maadui hawa katili waliamua kukitia sumu chakula Chake. Sumu hiyo ilikuwa kali mno, kwa hiyo, matokeo yake ya mwanzoni yalionekana kwa haraka na Bahá'u'lláh aliacha kula kile chakula chenye sumu ambacho walikuwa wamempa. Hatimaye, wale watu wa mamlaka hawakuwa na chaguo lingine isipokuwa kumwachilia kutoka gerezani, lakini kwa sharti kwamba alitakiwa kuondoka nchini na kwenda uhamishoni.

Bahá'u'lláh alistahimili muda wa miezi minne ndani ya gereza. Sasa alikuwa mgonjwa na amechoka. Hali zisizokuwa za kiutu za gereza lile, mnyororo wa takriban kilo 50 hivi uliozungukia shingo Yake, na mwishowe ile sumu, vilimuacha katika hali ya kudhoofishwa kiasi kwamba alilazimika kulala katika kitanda Chake chini ya uangalizi. Zile tepe za mnyororo zilifanya vidonda vichimbike shingoni Mwake na, ingawa vilipona baada ya muda, makovu yalibakia hadi mwisho wa maisha Yake. Katikati ya yote haya, familia Yake ililazimika kujiandaa kufanya safari ngumu ndani ya muda wa mwezi mmoja. Bahá'u'lláh alikuwa amepewa uhuru kuchagua mahali pa uhamisho Wake. Yeye alichagua Baghdád, wakati huo mji katika Ufalme wa Ottoman na leo mji mkuu wa 'Iráq.

Safari hiyo ilianza tarehe 12 Januari 1853 hadi tarehe 8 Aprili ya mwaka huo huo. Ilikuwa katikati ya majira ya baridi, na Bahá'u'lláh na familia Yake walakazimika kusafiri

kupitia sehemu ya magharibi ya Iran ambako nyakati za baridi ni baridi mno. Vyakula walivyokuwa navyo kwa ajili ya safari havikutosha, na iliwalazimu kuridhika na chakula kidogo. Lakini Mlinzi wa kikundi hiki kidogo cha wasafiri alikuwa ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe, na kwa kupitia msaada Wake usiokoma, waliwasili huko Baghdád kwa usalama.

Iran ilikuwa imejinyima yenyewe baraka ya kuwepo kwa Bahá'u'lláh na ilimshurutisha kuondoka, na kamwe kutorudi tena katika nchi Yake ya kuzaliwa. 'Iráq sasa ingekuwa maskani kwa ile Nafsi ya kuthaminiwa kabisa duniani. Mwana historia mashuhuri wa Kibahá'í ana maneno haya ya kusema kuhusu uhamisho wa Bahá'u'lláh kutoka Iran:

> "Kadiri Bahá'u'lláh alivyokaribia mpakani, muhula mmoja ulifikia mwisho wake. Je, watu wa Iran walitambua hasara waliyoipata? Wakiwa wamebobea katika ujinga, wakiwa wamedidimia katika ushupavu wa kidini, kupofushwa na ubaguzi, wakiongozwa na watu wenye ubinafsi wa kujinufaisha, wakighilibiwa na uongo, yao ilikuwa sio kuona na kujua. Na hivyo ndivyo Mkombozi wa ulimwengu alivyoondoka miongoni mwao. Yule Ambaye wakati fulani alipendwa na kuheshimiwa na matajiri na maskini, wakubwa kwa wadogo, mwana mfalme na mkulima kadhalika hivi sasa alitelekezwa na watu wale wale ambao Yeye alikuwa amewapa kwa wingi rehema nyingi mno, upendo, haki na hisani wakati wote. Iran ilipoteza kuwepo kwa Bahá'u'lláh, lakini je, roho Yake ingeweza kukosa kuwepo katika nchi hiyo au katika nchi nyingine yoyote?"[33]

1. Kwa nini maadui wa Bahá'u'lláh walishindwa kupata hukumu ya kifo Chake? ____
   ____________________________________________________________
   ____________________________________________________________
   ____________________________________________________________

2. Maadui wa Bahá'u'lláh hawakufanikiwa katika hila zao kumhusisha Yeye na jaribio juu ya maisha ya mfalme. Kwa hiyo wao walifanya nini? ______________________
   ____________________________________________________________
   ____________________________________________________________

3. Bahá'u'lláh alikuwa ndani ya Síyáh-Chál kwa miezi mingapi? __________________

4. Alifunguliwa kwa masharti gani? ___________________________________________
   ____________________________________________________________

5. Bahá'u'lláh alichagua mji gani kama mahali pa uhamisho Wake? ________________

6. Wakati ule mji wa Baghdád ulikuwa sehemu ya ufalme gani? Sasa ni mji mkubwa wa nchi gani? ___________________________________________________
   ____________________________________________________________
   ____________________________________________________________

7. Bahá'u'lláh na familia Yake walianza safari yao ya kwenda Baghdád mnamo tarehe ngapi? Safari yao ilifikia mwisho mnamo tarehe ngapi, takriban miezi mitatu baadaye?

______________________________________________

______________________________________________

8. Eleza hali ya safari hiyo.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 16

Sala ifuatayo iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh inatusaidia kupata kianga juu ya mateso aliyoyapata huko Síyáh-Chál na taabu alizozivumilia katika miezi iliyofuatia kwa karibu.

> **"Mungu Wangu, Bwana Wangu, Haja Yangu! . . . Wewe umeumba atomu hii ya vumbi kwa nguvu za kamili za uwezo Wako, na ukamlea kwa mikono Yako ambayo hakuna anayeweza kuifunga minyororo. . . . Wewe ulimkusudia majaribu na taabu ambayo hakuna ulimi unaweza kueleza, wala hakuna Nyaraka Zako zozote zinazoweza kuzieleza ipasavyo. Koo ambalo Wewe umelizoesha mguso wa hariri, mwishoni, Wewe umelifumbatia kwa minyororo yenye nguvu, na mwili ambao uliustarehesha kwa zari na mahameli Wewe hatimaye umeupatisha udhilifu wa gereza la shimoni. Amri Yako imenifunga Mimi kwa pingu zisizohesabika, na kunitupia minyororo shingoni Mwangu ambayo hakuna awezaye kuikata. Miaka kadhaa imepita ambamo mateso, kama manyunyu ya rehema, yameninyeshea Mimi. . . . Ni siku ngapi usiku ambamo uzito wa minyororo na pingu havikuniruhusu kupumzika, na ni nyingi jinsi gani siku ambamo nimenyimwa amani na utulivu, kwa sababu ya kile ambacho kwacho mikono na ndimi za watu vimenitesa Mimi! Vyote mkate na maji ambavyo Wewe, kupitia rehema Yako ikumbatiayo vyote, umeviruhusu kwa wanyama wa kondeni, kwa muda, mtumishi huyu alinyimwa, na mambo ambayo wamekataa kuwapatisha wale ambao wamejiondoa kutoka Hoja Yako, hayo hayo wameruhusu nipatishwe Mimi, hadi, hatimaye, amri Yako iliwekwa imara isibatilishwe, na amri Yako ilimuita mtumishi huyu kuondoka toka Uajemi, akiandamana na idadi ya watu wenye miili dhaifu na watoto wenye umri mchanga, katika kipindi ambamo baridi ni kali mno kwamba mtu hawezi hata kuongea, na barafu na theluji ni nyingi mno kiasi kwamba haiwezekani kusogea."**[34]

Pengine ungependa kukariri sala hiyo iliyopo hapo juu. Lakini hata kama unaisoma kwa kuipitia mara kadhaa, baadhi ya matamko kuhusu mateso ya Bahá'u'lláh yataingia akilini mwako. Ni yapi baadhi ya matamko haya?

## SEHEMU YA 17

Huko Baghdád, Bahá'u'lláh alikodi nyumba katika mtaa wa zamani wa mji. Katika miezi iliyofuata kuwasili Kwake, idadi iliyoongezeka ya Wabábí walikwenda Baghdád. Kwa bahati mbaya, wengi walikuwa wamekwisha zama katika hali ya kutia huruma; walikuwa wamechanganyikiwa na kufadhaishwa, na baadhi walikuwa wakifanya vitendo visivyomstahili mfuasi wa Báb. Bahá'u'lláh aliwapokea wote waliowasili kwa upendo mkubwa mno na aliwasaidia kusafisha mioyo yao na kuhuisha roho zao. Kwa ushawishi Wake, ustawi wa jamii ya Kibábí ulianza kubadilika na matumaini yalichanua tena. Lakini ole, hali ya hatari tena ilikuwa inanyemelea. Mara hii chanzo chake kilikuwa ndani ya jumuiya yenyewe; chanzo cha balaa hiyo siyo mwingine isipokuwa ndugu wa kambo wa Bahá'u'lláh mwenyewe, Mírzá Yaḥyá, ambaye alidai kuwa mrithi wa Báb.

Kwa kweli, Báb hakuona haja ya kumtaja mrithi, kwa kuwa Yeye alijua fika kwamba yule Mwahidiwa wa Zama Zote angetokea punde tu. Alichofanya kutokana na ushauri wa Bahá'u'lláh na mfuasi mmoja mwaminifu, ni kumteua Mírzá Yaḥyá, kama mkubwa wa jina tu. Hilo lingemuwezesha Bahá'u'lláh kuendeleza Hoja katika hali ya usalama kidogo. Mírzá Yaḥyá alikuwa amepokea upendo mwingi na msaada kutoka kwa Bahá'u'lláh katika maisha yake yote, lakini alikuwa mwenye kutaka makuu na pia mwoga. Kuuawa kishahidi kwa Báb kulimshtua mno kiasi kwamba karibu angepoteza imani yake. Alitangatanga kwa muda kama darweshi katika milima ya Mázindarán, mwenendo wake ukiwa wa kuaibisha mno kiasi kwamba aliwasababisha baadhi ya Wabábí wa eneo hilo kuondoka katika Hoja. Akitumia udanganyifu wa mavazi ya kujificha kwa kujigeuza tena na tena, hatimaye alikuja Baghdád, na baada ya kujipatia kiasi cha fedha kutoka kwa Bahá'u'lláh cha kuanzia biashara, alikuwa akiishi kwa jina jipya katika mojawapo ya ujirani wa mji huo.

Kuongezeka kwa heshima na upendo alivyokuwa anaonyeshwa Bahá'u'lláh na wafuasi wa Báb, pia hadhi Yake iliyokuwa inaendelea kukua miongoni mwa maafisa wa mji, vilikuwa na athari mbaya kwa Mírzá Yaḥyá. Wivu wake uliamshwa na moto wake uliwaka kwa ukali mno kiasi kwamba uliteketeza kila dalili ya adabu. Akiwa pamoja na mshiriki asiye na aibu zaidi kuliko yeye mwenyewe, Mírzá Yaḥyá alianza kupanda mbegu za mashaka miongoni mwa Wabábí kuhusu nia ya Bahá'u'lláh. Kwa mara nyingine tena mawingu ya tuhuma, hofu na mawazo ya kipuuzi yalishuka juu ya jumuiya ya Kibábí. Kpindi kifupi cha shwari na utulivu ulikuwa umefika mwisho na, siku hadi siku, maumivu ya Bahá'u'lláh yaliongezeka.

Asubuhi ya tarehe 10 Aprili 1854, familia ya Bahá'u'lláh iliamka na kukuta kwamba Yeye ameondoka. Aliuacha mji bila kumuambia mtu yeyote kusudi Lake au mwisho wa safari Yake. Alipoona mwelekeo wa vitendo vya Mírzá Yaḥyá ulikokuwa unaongozea, Bahá'u'lláh alichagua kujiondoa na kwenda kwenye milima ya Kurdistán, kaskazini mashariki mwa Baghdád. "Kusudi moja tu la kujiondoa Kwetu", Yeye Mwenyewe baadaye alisema, "lilikuwa kuepuka kuwa sababu ya ugomvi miongoni mwa waaminifu, chanzo cha msukosuko kwa wenzi Wetu, njia ya madhara kwa roho yeyote, au sababu ya huzuni kwa moyo wowote."[35]

Huko porini, mbali kidogo kutoka mji wa Sulaymáníyyih, Bahá'u'lláh aliishi peke Yake katika mazungumzo na Mungu. Yeye aliridhika na chakula kidogo tu. Wakati mwingine alipokea maziwa kutoka kwa wachungaji katika maeneo jirani na, mara chache alikwenda mjini kupata mahitaji machache muhimu ya maisha. Walakini, hata wakati wa mawasiliano haya mafupi na watu wa jimbo hilo, ukuu Wake usingeweza kufichwa kutoka macho yao. Upendo Wake na hekima vilivutia wakazi wa Sulaymáníyyih na umaarufu Wake ulianza kuenea katika maeneo jirani. Habari za mtu mwenye busara isiyokuwa ya kawaida na ufasaha aliyekuwa akiishi katika eneo hilo la Kurdistán hatimaye zilifika Baghdád. Familia Yake, ikitambua kwamba Mtu huyu asingeweza kuwa mwingine yeyote isipokuwa Bahá'u'lláh, ilimtuma muumini mwaminifu kumuomba arudi. Bahá'u'lláh alikubali ombi lao, hivyo akamaliza muda wa kujitenga Kwake kwa hiari kwa miaka miwili.

1. Wale Wabábí waliokwenda Baghdád baada ya Bahá'u'lláh kuwasili katika mji huo walikuwa katika hali gani? ____________________

2. Kwa nini walikuwa wameangukia katika hali ya namna hiyo? ____________________

3. Ni nini kilichoanza kutokea katika jumuiya ya Wabábí chini ya ushawishi wa Bahá'u'lláh? ____________________

4. Je, Báb alikuwa amekwisha mtaja mrithi? Kwanini hakufanya hivyo? ____________________

5. Báb alimtaja nani kama mkubwa wa jina tu? ________________________________

6. Uhusiano wa Mírzá Yaḥyá na Bahá'u'lláh ulikuwa upi? ______________________

7. Elezea tabia ya Mírzá Yaḥyá: ____________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

8. Mírzá Yaḥyá alifanya nini baada ya Báb kuuawa? ___________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

9. Je, heshima na upendo uliokuwa ukiongezeka ambao Bahá'u'lláh alikuwa akioneshwa na wafuasi wa Báb, pia na hadhi Yake iliyokuwa ikiongezeka miongoni mwa maafisa wa mji, vilikuwa na athari gani juu ya Mírzá Yaḥyá? _________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

10. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini alipoona mwelekeo wa vitendo vya Mírzá Yaḥyá? ____
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

11. Je, Bahá'u'lláh aliondoka kwenda katika eneo lipi? ___________________________

12. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba kusudi moja tu la kujiondoa Kwake lilikuwa kuepuka kuwa sababu ya ____________________________________, chanzo cha ___________________________, njia ya ______________________, au sababu ya _____________________________.

13. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini katika pori la Kurdistán? _________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

14. Je, kujiondoa kwa Bahá'u'lláh kutoka Ba<u>gh</u>dád kulidumu kwa muda gani? _______

15. Je, ni hali gani zilizomfanya arudi? ________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 18

Kila Mdhihirishaji wa Mungu hufanya Agano na wafuasi Wake. Wafuasi wa Báb walikuwa waliigia katika Agano Naye kwamba wangemtafuta na kumkubali Yule Ambaye Mungu angemdhihirisha na kuishi kwa kutii amri Zake. Ingawa Bahá'u'lláh bado alikuwa hajawaambia wengine kuwa Yeye alikuwa Yule aliyeahidiwa na Báb, ukuu Wake ulikuwa unazidi kuwa dhahiri zaidi kwa kila siku ipitayo, na wachache hata walianza kutambua Daraja Lake. Mírzá Yaḥyá hakuwa kipofu kwa ufahari na utukufu wa Bahá'u'lláh, alieendelea kuchochea fitina miongoni mwa Wabábí. Katika miaka itakayofuata, kama utakavyoona, njama zake dhidi ya Bahá'u'lláh zingeongezeka kwa ukubwa zaidi, hadi mwishowe yeye kwa uwazi angevunja Agano la Báb. Akirejelea kwenye ghasia na taabu zilizokuwa zinawasubiri, Bahá'u'lláh aliwaonya wenzi Wake waaminifu:

> **"Siku za majaribu sasa zimefika. Bahari za mafarakano na taabu zinasuasuka, na Beramu za Mashaka, katika kila pembe na kila kona, zinajishughulisha kuchochea fitina na kuwaongoza watu kwenye maangamizi kabisa. . . . Msiache sauti ya baadhi ya maaskari wa ukanaji kutia mashaka miongoni mwenu, wala msijiruhusu wenyewe kuwa wasiomjali Yule Ambaye ni Ukweli, kwasababu katika kila Maongozi ushindani kama huo ulianzishwa. Mungu, walakini, atasimamisha Imani Yake, na kudhihirisha mwanga Wake ingawa wachochezi wa maasi huuchukia. . . . Iangalieni sana kila siku Hoja ya Mungu. . . . Wote ni mateka katika mikono Yake. Hakuna mahali pa yeyote kukimbilia. Usifikirie Hoja ya Mungu kuwa kichukuliwacho kwa urahisi, ambamo mtu yeyote anaweza kuzifurahisha haja zake. Katika maeneo mbalimbali idadi ya roho katika wakati huu, zimeendeleza dai hili hili. Wakati unakaribia ambapo. . . . kila mmoja wao atakuwa amekwisha angamia na kupotea, la, atakuwa si kitu na atakuwa kitu kisichokumbukwa, hata kama vumbi lenyewe."[36]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Bahá'u'lláh Aliwaambia wenzi Wake wasiache ______________ ya baadhi ya ______________ wa ______________ kutia ______________ miongoni ______________ .

   b. Aliwaonya wasijiruhusu wenyewe kuwa ______________________________ ____________ ni ____________ .

   c. Yeye Aliwahakikishia kuwa Mungu, atasimamisha ________________________ , na kudhihirisha ________________________ ingawa ____________ wa ____________ watauchukia ______________________ .

d. Mtu yeyote asifikirie kuwa Hoja ya Mungu kuwa _______________ cha ________________ kwa _________________ , ambamo yeye anaweza ______________________________ zake.

e. Wakati unakaribia ambapo kila mmoja wao atakuwa amekwisha ____________ na _____________________ . Kama vumbi lenyewe watakuwa si kitu cha _________________ .

2. Bahá'u'lláh anawaita wale wanaotafuta kuweka mashaka kama "maaskari wa ukanaji". Wao wanakana nini?

## SEHEMU YA 19

Wakati wa kutokuwako kwa Bahá'u'lláh kwa kipindi cha miaka miwili, usitawi wa Imani ulikuwa umefikia wakati mbaya kabisa katika historia yake. Kama ilivyotarajiwa, Mírzá Yaḥyá alikuwa amejithibitisha mwenyewe kuwa hawezi kuongoza hata jumuiya ndogo huko Baghdád. Katika sehemu mbalimbali, idadi ya Wabábí walikuwa wakishughulika katika shughuli ambazo zilileta aibu kwenye Hoja yenye thamani ya Báb. Hivyo, kwa mara nyingine tena, Bahá'u'lláh alijitwisha kazi ya uhuishaji jumuiya hiyo. Kuwasili Kwake mnamo Machi 1856 kulitangazwa kwa waumini, na mlango Wake ulifunguliwa kwa wale wote waliotamani sana ukweli. Ile nyumba ya wastani ambamo Yeye aliishi pamoja na familia Yake ikawa kituo ambamo ndani yake walikusanyika watafutaji, na wageni. Kila mmoja aliyekuja mbele Yake alibadilishwa na nguvu ya maneno Yake matamu na yenye upendo. Wale ambao walikuwa na baraka ya kuishi katika ujirani wa karibu na Yeye waliona kana kwamba walikuwa katika paradiso. Wao waligeuka kuwa muumbo mpya, ambao walijitenga kabisa kutokana na mambo ya ulimwengu huu. Hivi ndivyo jinsi Nabíl, mwanahistoria mkuu wa Enzi ya Kibahá'í ya mwanzoni, ameelezea hali ya roho hizo:

> "Siku nyingi wakati wa usiku si chini ya watu kumi walijikimu kwa tende za thamani isiyozidi senti ishirini. Hakuna aliyejua hasa viatu vilikuwa vya nani, majoho ya nani, au kanzu zilizokuwemo majumbani mwao. Yeyote aliyekwenda dukani angeweza kudai kuwa viatu miguuni mwao vilikuwa vyake mwenyewe, na yeyote aliyekuja mbele ya Bahá'u'lláh angeweza kuthibithisha kuwa joho na kanzu alivyokuwa amevaa wakati huo vilikuwa vyake. Majina yao wenyewe waliyasahau, ndani ya mioyo yao kila kitu kilikuwa kimeondolewa isipokuwa upendo wa kumwabudu Mpenzi wao. . . . Ah, kwa furaha ya siku zile, na nderemo na maajabu ya saa zile!"[37]

Bahá'u'lláh alibakia huko Baghdád kwa miaka saba baada ya kurudi Kwake kutoka Sulaymáníyyih. Katika wakati huu wote, Yeye aliendelea kuficha Daraja Lake kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Walakini upendo Mtakatifu ulimiminika kutoka Kwake kwa kiasi ambacho kwamba mioyo pokevu haikuwa na jinsi ila tu kuguswa nao. Uongozi alioufunua katika mazungumzo na katika aya zilizoandikwa na Nyaraka vilibadilisha tabia ya Wabábí ambao walikuwa wameachwa bila mchungaji kwa muda mrefu mno. Hii ni miaka ambamo Yeye alifunua Kitabu cha Yakini, ambamo Yeye alielezea asili ya Ufunuo wa Mungu katika maneno yaliyo wazi kabisa kiasi kwamba misingi ya imani zilizobuniwa na watu ya wakati uliopita iliteketezwa. Ni katika kipindi hiki hiki kwamba Yeye alifunua, alipokuwa

anatembea kwenye kingo za mto wa Tigris akiwa amezongwa katika tafakari, Maneno Yaliyofichwa, yanayopendwa na kila mmoja wetu kama mwongozo kwa ukuaji wetu wa kiroho. Wepesi ambao kwao aya zilitiririka kutoka kwenye Kalamu Yake ulikuwa wa kushangaza. Hivi ndivyo jinsi Yeye Mwenyewe amesema kuhusu kipindi kile chenye uwezo usiokuwa wa kawaida:

> **“. . . Sisi tulifunua kwa wingi kama mvua kubwa, kwa msaada wa Mungu na Neema Yake Takatifu na rehema, aya Zetu, na kuzituma katika maeneo mbalimbali ya ulimwengu. Tuliwashawishi watu wote, hususan watu hawa, kwa kupitia ushauri Wetu wa hekima na maonyo yenye upendo, na tuliwakataza kushughulika katika uchochezi, ugomvi, mabishano na mapigano. Kama matokeo yake, na kwa neema ya Mungu, ukaidi na upuuzi vilibadilishwa kuwa uchaji Mungu na ufahamu, na silaha zilibadilishwa kuwa zana za amani.”[38]**

Ile miaka saba ya maisha ya Bahá’u’lláh huko Baghdád ilionyesha kipindi cha ushindi adhimu. Ilikuwa itarajiwe, basi, kwamba mara au baadaye hali ya hatari sharti ijitokeze, ambayo baadaye ingefuatwa na ushindi mkubwa zaidi. Uongezekaji wa hadhi ya Bahá’u’lláh haukwenda bila kuonwa na maadui wa Imani. Mwenye juhudi kabisa miongoni mwao alikuwa Shaykh mmoja ambaye alitumia kila njia alizokuwa nazo kuwasadikishia maafisa wa Serikali za Uajemi, na Uturuki pia, na vilevile makasisi, kuinuka katika upinzani dhidi Yake.

Kwa miaka mingi, jitihada za Shaykh huyo zilizuiwa kwa hekima ya Bahá’u’lláh na ubora wa maneno Yake na vitendo. Wakati mmoja, kwa mfano, Shaykh huyu aliwaita pamoja makasisi mashuhuri kabisa katika eneo hilo akiwa na nia ya kumpatia Bahá’u’lláh laana ya pamoja kutoka kwao. Wote walikuwa tayari kuanzisha mashambulizi dhidi ya kikundi hiki kidogo cha wakimbizi hapo Baghdád ili kuiangamiza Imani kwenye kiini chake. Kwa mshangao wao, walakini, yule mwenye daraja ya juu kabisa miongoni mwao, mtu ambaye alijulikana kwa haki yake na uchaji, alikataa kutoa hukumu iliyotakiwa dhidi ya Wabábí. Yeye alikiambia kikundi hicho kwamba, kwa ufahamu wake, jumuiya ya Kibábí ilikuwa haijafanya chochote ambacho kingestahili kitendo kama hicho na aliondoka katika mkusanyiko huo.

Kwa kuwa mpango wao wa mwanzo ulishindwa, kikundi hicho kiliamua kumtuma mtu mwenye elimu kwenda kwa Bahá’u’lláh na kumwuliza idadi fulani ya maswali kwa ajili ya kuupima ujuzi Wake. Bahá’u’lláh alipoyajibu maswali yote, mjumbe huyu kwa niaba ya kikundi cha makasisi, alikubali ukubwa mno wa ujuzi Wake. Lakini basi, yeye alisema, ili kumridhisha kila mmoja ahusikaye juu ya ukweli wa Utume Wake, Yeye sharti awafanyie muujiza. Bahá’u’lláh alijibu, “Ingawa huna haki kuomba jambo hili, kwa kuwa Mungu ndiye anayewajaribu viumbe Wake, na wao hawapaswi kumjaribu Mungu, bado ninaruhusu na kukubali ombi hili.”[39] Walakini, alimpa yule mjumbe sharti moja: kwanza wale makasisi sharti wachague muujiza mmoja na kuandika kwamba, baada ya utimizwaji wake, wasiwe tena na mashaka juu Yake na wangetambua na kukiri ukweli wa Hoja Yake. Wao wangeipiga muhuri hati hii na kuileta Kwake.

Jibu hili la wazi na lenye kutoa changamoto lilimgusa sana mjumbe yule. Mara aliinuka, akalibusu goti la Bahá’u’lláh na kuondoka. Aliuwasilisha ujumbe wa Bahá’u’lláh kwa kikundi kile cha makasisi. Walijadiliana juu yake kwa muda wa siku tatu, lakini hawakuweza kufikia uamuzi wowote. Hatimaye, hawakuwa na chaguo lingine ila kuliacha jambo lenyewe.

Bado maadui hawa katili wa Imani hawakuacha hila zao dhidi ya Bahá’u’lláh. Waliendelea kuchochea fitina na kutafsiri vibaya nia Yake kwa watu wa mamlaka, mpaka

hatimaye, katika majira ya machipuko ya mwaka 1863, juhudi zao zilifanikiwa, na hali nyingine ya hatari ikatokea.

1. Je, jamii ya Kibábí ilikuwa katika hali gani wakati Bahá'u'lláh aliporudi Baghdád?

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Je, Mírzá Yaḥyá alikuwa amejithibitisha mwenyewe kuwa mwenye uwezo wa kuongoza jumuiya? ______________________________

3. Je, kurudi kwa Bahá'u'lláh huko Baghdád kulikuwa na matokeo gani juu ya Wabábí?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

4. Ukichota kutoka maelezo ya Nabíl, sema maneno machache juu ya wale waliokuwa wakiishi katika ujirani wa karibu na Bahá'u'lláh.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

5. Je, Bahá'u'lláh alibakia huko Baghdád kwa muda wa miaka mingapi baada ya kurudi Kwake kutoka Sulaymáníyyih? ______________________________

6. Taja kazi (vitabu) mbili zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh katika muda wa miaka ile saba huko Baghdád: ______________________________

_______________________________________________

7. Je, dhamira kuu ya Kitabu cha Yakini ni nini? ______________________________

_______________________________________________

8. Mada za aina gani zinaongelewa katika Maneno Yaliyofichwa? ________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

9. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Bahá'u'lláh anatuambia kwamba kwa __________________________ wa Mungu na __________________ na __________________ Yake, Yeye alifunua aya Zake kama __________________________________________________________ .

b. Alizituma aya hizi kwa ________________________________________________ .

c. Katika aya hizi, Yeye ____________________ jamii ya wanadamu kwa kupitia _________________________ Wake _______________ na _________________ .

d. Yeye aliwakataza ______________ katika ______________ na _____________ , ____________________________ , na ____________________.

e. Yeye aliwakataza ______________ katika ______________ na _____________ , ____________________________ , na ____________________ .

10. Hadhi ya Bahá'u'lláh ilivyo kuwa ikiongezeka iliwaathirije maadui wa Imani? ____

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

11. Je, kifungu hiki cha maneno "laana ya pamoja" kina maana gani? ______________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

12. Simulia katika maneno yako mwenyewe hadithi ya kikundi kile cha makasisi na yule mjumbe waliyemtuma kwa Bahá'u'lláh huko Baghdád.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 20

Katika kujifunza Imani, utasoma Kitabu cha Yakini na utatafakari juu ya maana yake ya undani sana ya mada zake nyingi. Wewe, bila shaka, tayari unafahamu Maneno Yaliyofichwa. Kitabu hiki kitakuwa mwenzi wako wa siku zote maisha yako yote, na mwongozo mtakatifu uliomo humo utakuwa na nguvu kubwa juu ya maendeleo yako ya kiroho. Katika wakati huu, unapotafakari juu ya kipindi cha maisha ya Bahá'u'lláh huko Baghdád, wakati ambapo vitabu hivi viwili vilifunuliwa, pengine ungependa kukariri kifungu cha ufunguzi cha kila kitabu. Kitabu cha Yakini huanza kwa maneno haya:

> **"Hakuna mtu atakayezifikia fuko za bahari ya ufahamu wa kweli isipokuwa akijitenga na vyote vilivyomo mbinguni na duniani. Takaseni roho zenu, Enyi watu wa ulimwengu, ili huenda muweze kulifikia daraja lile ambalo Mungu amelikusudia kwa ajili yenu na hivyo kuingia katika hema ambalo, kufuatana na vipindi vitatatifu vya Mjalia, limeinuliwa katika mbingu ya Bayán."[40]**

Na kifungu cha ufunguzi cha Maneno Yaliyofichwa husoma:

> **"Hiki ndicho kile kilichoshuka kutoka katika milki ya utukufu, kilichotamkwa na ulimi wenye uwezo na nguvu na kufunuliwa kwa Mitume wa kale. Tumechukua kiini chake tu na kukivisha vazi la ufupisho kama ishara ya neema kwa wote walio wanyofu ili wawe waaminifu kwa Agano la Mungu, ili waweze kutimiza katika maisha yao dhamana Yake na katika milki ya roho wapate kito cha wema mtakatifu."[41]**

## SEHEMU YA 21

Kuelekea mwisho wa kukaa Kwake huko Baghdád, Bahá’u’lláh mara kwa mara alianza kuongelea juu ya mitihani na majaribu ambayo yalikuwa mbele yao. Ndoto ambayo wakati mmoja aliwasimulia wenzi Wake ilisababisha majonzi makubwa kwao. “Niliwaona” Aliandika katika Waraka: “Mitume na Wajumbe wakikusanyika na kukaa pamoja kunizunguka Mimi wakipiga kite, wakilia na kuomboleza kwa sauti. Kwa mshangao Nilliwauliza sababu, ndipo kuomboleza kwao na kilio viliongezeka zaidi, na wakaniambia: ‘Sisi tunakulilia Wewe, Ewe Fumbo Kuu kabisa, Ewe Hema la Umilele!’ Walilia kwa kilio kikubwa mno kwamba Mimi pia nililia nao. Ndipo Umati wa juu uliniambia ukisema: ‘. . . Hivi punde utaona kwa macho Yako mwenyewe kile ambacho hakuna Mtume amepata kukiona. Uwe na subira, uwe na subira.’ . . . Waliendelea kunisemesha usiku mzima hadi kukaribia mapambazuko.”[42]

Mapema katika majira ya machipuko ya 1863, Bahá’u’lláh alifunua Waraka wa Baharia Mtakatifu ambao, katika lugha ya fumbo, alibashiri matukio ya siku zijazo na alizungumza juu ya usaliti na utengano. Waraka huu ulisomwa kwa marafiki waliokusanyika mbele Yake. Bahari kuu za huzuni zilisukasuka mioyoni mwao walivyohisi kwamba Bahá’u’lláh angechukuliwa kutoka kwao. Baadaye siku hiyo hiyo, tarishi alimletea Bahá’u’lláh taarifa iliyomuomba akafanye mahojiano na gavana wa Baghdád. Siku iliyofuata, alipofika kwa ajili ya mahojiano, Bahá’u’lláh alipewa barua kutoka kwa waziri mkuu wa milki ya Ottoman kwa gavana, ilikuwa imeandikwa kwa namna ya adabu, ilimualika Bahá’u’lláh kusafiri hadi mji mkuu wa Uturuki, Constantinople. Kikundi cha walinzi wapanda farasi kiliamuriwa kumsindikiza kwa ajili ya ulinzi Wake. Bahá’u’lláh alikubali ombi hilo mara moja, lakini alikataa kupokea fedha ambayo serikali ilikuwa imeitoa kwa ajili ya safari Yake.Mwakilishi wa gavana alisisitiza kwamba aikubali, akisema kwamba wale watu wa mamlaka wangechukizwa kama asingefanya hivyo. Hatimaye, alikichukua kile kiasi kikubwa cha fedha na hapo hapo alikigawa miongoni mwa masikini wa mji huo.

Habari za uhamisho wa Bahá’u’lláh kutoka Baghdád ziliitikisa jumuiya ya Wabábí. Zile roho, waliokuwa wanampenda sana, walikuwa wamezoea Uwepo Wake mwangavu, walielemewa na huzuni. Na mwanzoni, hakuna mtu aliyeweza kulala au kula. Polepole, walakini, walitulizwa kwa maneno mema na ya huruma ya Bahá’u’lláh na walikubali kuwa wengi mno watanyimwa baraka ya kuandamana Naye katika hatua iliyofuata ya uhamisho Wake. Kama dalili ya upendo Wake, aliandika, kwa mkono Wake mwenyewe Waraka kwa kila mmoja wa waumini walioishi katika mji huo — mume, mke na mtoto.

Katika ujirani wa Baghdád, ilikuwepo bustani nzuri iliyojaa mawaridi, na waridi lilikuwa ua lipendwalo zaidi na Bahá’u’lláh. Mchana wa tarehe 22 Aprili 1863, aliondoka mjini na kuingia ndani ya bustani hii. Waumini, na hakika idadi kubwa ya watu wa Baghdád, walipatwa na huzuni. Jumuiya ya Kibábí, ikiwa imehuishwa kabisa kupitia utunzaji wa upendo wa Bahá’u’lláh, ilikuwa sasa imeingia tena katika hali ya hatari nyingine. Je, upi ungekuwa mustakabali wa Imani hii changa ambayo Tumaini pekee lilikuwa linahamishwa kwenda mahali ambako ni mbali mno kutoka wengi wa wafuasi wake? Jibu lililokuwa likiwangojea wale marafiki waliovunjika mioyo ambao walikusanyika kumuaga lilikuwa la kushangaza ajabu. Bahá’u’lláh angepasulia mbali utando ambao ulificha Daraja Lake halisi na angetangaza kwamba Yeye alikuwa Yule Mwahidiwa wa Zama zote.

Bahá’u’lláh alikaa katika bustani hiyo, ijulikanayo leo kama Bustani ya Riḍván, kwa muda wa siku kumi na mbili kabla hajaondoka kwenda Constantinople. Maadui Zake walikuwa wamejaribu kuipa kipigo cha kuiuwa Hoja Yake kwa kumtenganisha Yeye kutoka wengi wa

wafuasi wake. Mungu, walakini, aliyageuza maagano hayo kuwa tukio la furaha kubwa mno. Tangazo la Utume Wake liliumba uhai mpya katika roho za wenzi Wake. Hii ndiyo ilikuwa Siku ya Siku ambayo kwayo Báb alikuwa amewaandaa. Bahá'u'lláh Mwenyewe amesema kwamba katika Siku hiyo "vitu vyote vilivyoumbwa vilizamishwa katika bahari ya utakaso."[43]

Kuna tondoti kidogo zinazojulikana juu ya mazungumzo ambayo Bahá'u'lláh aliyafanya na mmiminiko wa wageni aliowapokea katika Bustani ya Riḍván. Maneno yafuatayo ya mwana historia Nabíl yanatupa tu kianga juu ya utukufu wa siku zile:

> "Kila siku, kabla ya saa ya mapambazuko watunza bustani wangechuma mawaridi ambayo yalikuwa yamejipanga katika mstari pembezoni mwa njia nne za bustani, na wangeyalundika katikati ya sakafu ya hema Lake lililobarikiwa. Lile lundo lilikuwa kubwa mno kiasi kwamba pale wenzi Wake walipokusanyika kunywa chai yao ya asubuhi mbele Yake, wale waliokaa upande mmoja wangeshindwa kuwaona waliokaa upande wa pili. Mawaridi yote haya, Bahá'u'lláh kwa mikono Yake mwenyewe, angeyakabidhi kwa wale Aliyowaaga kutoka mbele Yake kila asubuhi ili wayawasilishe, kwa niaba Yake, kwa marafiki Zake wa Kiarabu na wa Kiajemi mjini humo. . . . Usiku mmoja, usiku wa tisa wa mwezi mwandamo, nilitokea kuwa mmoja wa waliofanya doria kando ya hema Lake lililobarikiwa. Saa sita ya usiku ilipokaribia, nilimuona akitoka katika hema Lake, akipita karibu na mahali ambapo baadhi ya wenzi Wake walikuwa wamelala, na alianza kutembea huku na huko katika zile njia za bustani ilizoangaziwa na mwezi, zilizo kuwa na maua kingoni mwao. Uimbaji wa ndege shorwe ulikuwa wa sauti kubwa sana kila upande kiasi kwamba, ni wale tu waliokuwa karibu Naye wangeweza kuisikia sauti Yake kwa uwazi. Aliendelea kutembea hadi aliposita katikati ya mojawapo ya njia hizi, alisema: 'Fikiria ndege shorwe hawa. Upendo wao kwa mawaridi haya ni mkubwa mno, kiasi kwamba, bila usingizi kutoka machweo hadi mapambazuko, wao huimba nyimbo zao na kuzungumza kwa shauku kali na kusudi la ibada yao. Inawezekanaje basi, kwamba wale wanaodai kuwa wanawaka kwa ajili ya uzuri wa Mpendwa mfano wa mawaridi wangeweza kuchagua kulala?' Kwa siku tatu usiku mfululizo nililinda na kulizunguka hema Lake lililobarikiwa. Kila wakati nilipopita karibu na kitanda alicholalia, ningemkuta yuko macho, na kila siku, tangu asubuhi hadi jioni, ningemuona akijishughulisha bila kukoma katika mazungumzo na mmiminiko wa wageni ambao waliendelea kumiminika kutoka Baghdád. Hata kwa mara moja sikuweza kugundua katika maneno aliyoyasema dalili yoyote ya kuigiza."[44]

Leo, Siku Kuu ya Riḍván inasherehekewa kila mwaka kote ulimwenguni kuadhimisha Tangazo la Dhima ya Bahá'u'lláh. Zile siku kumi na mbili ni siku kuu takatifu kabisa na zenye maana sana kati ya siku kuu zote za Kibahá'í.

1. Simulia katika maneno yako mwenyewe ile ndoto Bahá'u'lláh aliyoiona kuelekea mwishoni mwa kukaa Kwake huko Baghdád.

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

2. Je, ile ndoto ilikuwa na maana gani? ______________________

3. Je, Bahá'u'lláh alifunua lini Waraka wa Baharia Mtakatifu? ______________________

4. Waraka wa Baharia Mtakatifu ulikuwa unatabiri nini? ______________________

5. Je, yule mjumbe kutoka serikalini alimletea nini Bahá'u'lláh mnamo siku ile pale ule Waraka uliposomwa kwa marafiki waliokusanyika mbele Yake? ______________________

6. Je , kitu gani kiliwasilishwa kwa Bahá'u'lláh siku iliyofuata? ______________________

7. Je, serikali iliamua kumpeleka wapi Bahá'u'lláh? ______________________

8. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini na kile kiasi cha fedha ambacho serikali ilikuwa imempa kwa ajili ya Safari Yake? ______________________

9. Je, jumuiya ya waumini ilizipokeaje habari za kuondoka kwa Bahá'u'lláh kulikouwa kunakaribia? ______________________

10. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini kama ishara ya upendo Wake kwa ajili ya waumini wa Baghdád? ______________________

11. Ile bustani ambapo Bahá'u'lláh alitangaza Dhima Yake inajulikana kwa jina gani sasa?

____________________________________________________________

12. Alikaa siku ngapi katika bustani?__________________________________

13. Ukirejea kwa siku zile tukufu, Bahá'u'lláh alikaa katika Bustani ya Riḍván, Nabíl anatuambia:

a. Kila siku, saa ya alfajiri, watunza bustani wali _________________________ ____________________________________________ , na ______________________ _______________________________________________________ .

b. Lile lundo la mawaridi lilikuwa kubwa mno, kiasi kwamba wenzi wa Bahá'u'lláh ____________________________________________________________ mbele Yake wasingeweza _________________________________________________ _______________________________________________ .

c. Mawaridi yote haya Bahá'u'lláh, kwa mikono Yake mwenyewe, aliyakabidhi kwa wale aliowaaga kutoka mbele Yake kila siku asubuhi kuwasilishwa, kwa niaba Yake, __________________________________________________________ .

d. Usiku mmoja, Nabíl alitokea kuwa mmoja wa wale ambao __________________ ______________________ .

e. Usiku saa sita ilivyokuwa ikikaribia, Nabíl alimuona Bahá'u'lláh akitoka _____________________ , akipita karibu ________________________ , na Alianza ______________________________________________________________ .

f. _________________________________________ ulikuwa kwa sauti kubwa sana _____________ kiasi kwamba ni wale tu ambao walikuwa karibu na Bahá'u'lláh Wangeweza ________________________________________ .

g. Bahá'u'lláh aliendelea kutembea hadi, ____________________________________ _______________________ , Yeye alisema: "Fikiria ____________________ hawa _________________________ . Ni mkubwa mno ____________________ wao kwa _________________________ , kiasi kwamba _____________________ kutoka _______________________________________________ , wao _____________ zao _____________ na ______________________________________ . Wanawezaje wale wana ______________ kuwa _______________ na ______________________ ____________________ kuchagua _______________ ?"

h. Kwa siku tatu usiku mfululizo Nabíl _________________________________ _______________________________________________ .

Kila mara Nabíl alipita karibu na kitanda ambapo Bahá'u'lláh alikuwa amepumzika, yeye ali ______________________________ , na kila siku, kutoka asubuhi hadi jioni, yeye ali ______________________________________________________
______________________________________________________________________
____________________________________________________________________ .

i. Hata mara moja Nabíli hakuweza kugundua maneno Bahá'u'lláh aliyoakisema ____________________________________________ .

14. Je, maadui wa Imani walikuwa wakijaribu kutimiza nini kwa kuwatenganisha Bahá'u'lláh kutoka kundi lote la waumini, na Mungu alikusudia nini badala yake?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

15. Ni siku kuu gani ambayo tunaiadhimisha leo kama kumbukumbu ya Tangazo la Dhima ya Bahá'u'lláh? ________________________________________________

16. Je, Siku kuu ya Riḍván inadumu kwa muda gani, na inasherehekewa katika tarehe gani?
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

17. Sasa kwa kuwa umemaliza mafunzo juu ya uhamisho wa Bahá'u'lláh kutoka Iran hadi 'Iráq, andaa na utoe mazungumzo mafupi juu ya kipindi hiki cha maisha Yake.

## SEHEMU YA 22

Hapo chini vipo vifungu kutoka Waraka uliofunuliwa na Bahá'u'lláh. Visome vifungu hivyo kwa sauti na kubwa wakati unafanya hivyo, kumbuka Tangazo katika Bustani ya Riḍván na acha Maneno Yake yaujaze moyo wako kwa furaha.

> **"Majira Matakatifu ya kuchipua yamekuja, Ee Kalamu Uliyetukuka kabisa, kwa kuwa Sikukuu ya Mwenye Rehema kabisa inakaribia kwa haraka. Jishughulishe na litukuze, mbele ya muumbo mzima, jina la Mungu, na adhimisha sifa Yake, kwa jinsi ambayo vitu vyote vilivyoumbwa viweze kuongoka na kufanywa vipya. Sema, na usinyamaze. Nyota ya mchana ya furaha kuu inang'aa juu ya upeo wa jina Letu, Mwenye-Furaha kuu, kwa kuwa ufalme wa majina ya Mungu umepambwa kwa pambo la jina la Bwana wako, Muumba wa mbingu. Inuka mbele ya mataifa ya dunia, na jihami kwa silaha ya uwezo wa Jina hili Kuu Kabisa, na usiwe miongoni mwa wale ambao hukawia. . . .**

**“Je, unaweza kumgundua mwingine yeyote ila Mimi, Ewe Kalamu, katika Siku hii? Nini kimeutokea muumbo na madhihirisho yake? Vipi kuhusu majina na ufalme wao? Vimeenda wapi viumbe vyote, vinavyoonekana na visivyoonekana? Na vipi kuhusu siri zilizofichwa za ulimwengu na funuo zake? Tazama, muumbo mzima umepita! Hakuna kilichobakia isipokuwa Uso Wangu, Adumuye-Daima, Ang’aaye, Mtukufu-Kabisa.**

**“Hii ni Siku ambamo hakuna kinachoweza kuonekana isipokuwa wang’avu wa Mwanga ambao ung’aa kutoka uso wa Bwana Wako, Mwenye Neema, Mkarimu Kabisa. Kwa ukweli, tumesababisha kila roho kukupoteza uhai kutokana na mamlaka Yetu yasiyozuilika, yashindayo vyote. Ndipo kwa hiyo tumeumba muumbo mpya, kama dalili ya neema Yetu kwa wanadamu. Mimi, kwa ukweli ni Mkarimu Kabisa, Mkale wa Siku. . . .**

**“Sema: Hii ndiyo ile Paradiso ambayo juu ya majani yake, divai ya matamshi imechapisha ushuhuda: ‘Yule ambaye alifichwa kutoka macho ya watu amefunuliwa, akizungukwa na mamlaka na uwezo!’ Hii ndiyo ile Paradiso, ambayo mchakacho wa majani yake hutangaza: ‘Enyi ambao huishi mbinguni na duniani! Kimetokea kile ambacho kamwe hakijatokea hapo kabla. Yule Ambaye, kutoka milele, alikuwa ameuficha Uso Wake kutoka upeo wa muumbo sasa amekuja.’ Kutoka upepo mwanana unong’onao ambao hupeperuka kati ya matawi yake sauti inasikika: ‘Yule Ambaye ni Bwana Mwenye-enzi wa wote amedhihirishwa. Ufalme ni wa Mungu,’ ambapo kutoka maji yake yatiririkayo, mvumo unaweza kusikika: ‘Macho yote yamefurahishwa, kwa kuwa Yule Ambaye hakuna aliyewahi kumuona, Ambaye siri yake hakuna aliyeigundua, ameuinua utaji wa utukufu, na kuufichua uso wa Uzuri.’**

**“Ndani ya Paradiso hii, na kutoka vilele vya vyumba vyake ya juu kabisa, Wanawali wa Mbinguni wamepaza sauti na kupiga ukelele: ‘Furahini, ninyi wakazi wa milki za juu, kwa kuwa vidole vya Yule Ambaye ni Mkale wa Siku vinagonga, katika jina la Mtukufu Kabisa, Kengele Kuu Kabisa, katikati ya kiini cha mbingu. Mikono ya fadhila imezungusha kikombe cha uzima wa milele. Karibia na ugugumize funda yako. Kunyweni kwa ladha yenye afya, Enyi ambao ni mifanano yenyewe hasa ya shauku, ninyi ambao ni mifano halisi ya matamanio makali!’”**[45]

## SEHEMU YA 23

Bahá’u’lláh, familia Yake, na kile kikundi kidogo cha waumini waliokuwa wakiandamana nao walikaa Constantinople kwa muda wa miezi minne tu. Serikali ya Uajemi iliendeleza kutoka mbali utesaji wa Yule ambaye ushawishi Wake waliuona kama tishio. Balozi wake katika baraza la Sulṭáni — mtawala wa Milki ya Ottoman — alianzisha kampeni ya kiutaratibu dhidi ya Bahá’u’lláh. Mazingira ambamo Sulṭáni, mawaziri wake na washiriki wao waliishi yalikuwa ya usaliti, njama, na unafiki. Bahá’u’lláh alikataa kuwa na uhusiano wowote na wajumbe wa baraza na malengo yao yasiyo na thamani. Hili lilirahisisha kazi ya yule Balozi wa Uajemi kujaza akili za watu wa mamlaka kwa tuhuma na uwongo. Juhudi zake zisizochoka zilikuwa na matokeo na hatimaye amri ilitolewa ya kumhamisha Bahá’u’lláh kwenda kwenye mji wa Adrianople, mbali zaidi kutoka mpaka wa Uajemi.

Bahá’u’lláh Alipokea amri hii kwa ujasiri usio wa kawaida. Papo hapo alifunua Waraka mrefu ambamo alimuandikia Sulṭáni mwenyewe, alimkemea yeye na mawaziri wake, na aliufichua uchanga wao na kutofaa kwao. Waraka huo uliwasilishwa kwa waziri mkuu katika bahasha iliyofungwa kwa muhuri. Inasemekana kwamba alipoifungua barua hiyo na kuanza kuisoma, alikwajuka na alisema: “Ni kama Mfalme wa Wafalme alikuwa akitoa amri yake kwa mfalme mtumishi wake wa chini kabisa na akirekebisha mwenendo wake.”[46]

Ile safari ya siku kumi na mbili kutoka Constantinople kwenda Adrianople ilikuwa ngumu sana Bahá’u’lláh na familia Yake, ambao sasa walikuwa katika uhamisho wao wa tatu. Ulikuwa ni mwezi Desemba na hali ya hewa ilikuwa ya baridi mno. Hata kupata maji kutoka chemichemi njiani mwao iliwalazimu kuwasha moto kuyeyusha barafu. Wengi miongoni mwa wahamishwa hawa hawakuwa na nguo zinazohitajika kujikinga na hali mbaya ya hewa kama hiyo.

Bahá’u’lláh aliingia Adrianople mnamo tarehe 12 Desemba 1863 na alikaa katika mji huo kwa jumla ya miaka minne na nusu. Kipindi hiki tena kilikuwa kimojawapo cha hali ya hatari ya kuumiza na ushindi wa fahari sana. Kadiri uwezo wa Bahá’u’lláh ulivyokua, ndivyo moto wa wivu uliwaka kwa ukali zaidi katika moyo wa Mírzá Yaḥyá. Akawa mjasiri zaidi na zaidi katika upinzani wake na alijaribu kila lililowezekana kuwazuia Wabábí wasimkubali Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Matatizo aliyoyasabisha siyo tu yalileta shida ndani ya jumuiya yenyewe, lakini pia yaliwapa silaha maadui wa nje wa Imani ambazo walizitumia kuanzisha mashambulizi zaidi dhidi ya Bahá’u’lláh na wafuasi Wake. Usaliti wa Mírzá Yaḥyá ulionekana kutokuwa na mipaka. Yeye hata aliamua kumtilia sumu Bahá’u’lláh, na baada ya njama nyingi na jitihada yeye hatimaye alifanikisha madhumuni yake. Athari ya ile sumu kwa Bahá’u’lláh ilikuwa ya kubwa, na ingawa alipona, aliachwa na mkono wenye kutetemeka hadi mwisho wa maisha Yake.

Adrianople, bila shaka, haitakumbukwa kwa ajili ya vitendo vya aibu ya Mírzá Yaḥyá, bali kwa ushindi mkuu ambao Bahá’u’lláh aliupata katika mji ule. Ilikuwa ni kutoka hapa kwamba Bahá’u’lláh alituma Nyaraka Zake nyingi zilizoandikwa kwa wafalme na watawala wa ulimwengu na aliitangaza Imani Yake kwa marefu na mapana.

Tangazo Lake la hadharani lilikuwa ni hatua ya tatu ya mchakato uliokuwa ukiendelea taratibu ambao kupitia humo Dhima ya Bahá’u’lláh ulijulishwa kwa jamii ya wanadamu. Hatua ya kwanza ilianza katika gereza la Síyáh-Chál huko Ṭihrán wakati Roho Takatifu ilipojifunua yenyewe kwa Bahá’u’lláh na ilimtangazia Yeye kwamba Yeye alikuwa Mbebaji wa Ujumbe wa Mungu kwa siku hii. Ingawa kuzaliwa kwa Ufunuo Wake ulibakia bila kujulikana kwa miaka kumi, lakini kama mapambazuko, ulichochea roho zilizokuwa zimelala, ukiamsha wale wapokevu na kuwaandaa kumtambua Bahá’u’lláh. Hatua ya pili ilifunguliwa katika Bustani ya Riḍván, ambako Yeye alitangaza Dhima Yake kwa baadhi ya marafiki waliokuwa wamekusanyika kumuaga. Sasa kundi dogo la roho ziliopendelewa zilitambua Daraja Lake. Hatua ya tatu ilikuwa tangazo la Dhima Yake kwa watu wote. Ilianzia Constantinople, na ikachapuzwa zaidi huko Adrianople, na kufikia vilele vyake vya juu kabisa katika ‘Akká, hatua iliyofuata na ya mwisho ya uhamisho Wake.

1. Bahá’u’lláh alibakia huko Constantinople kwa muda gani? ____________________

2. Kwa nini kukaa Kwake pale kulikuwa wa muda mfupi hivyo? ___________________

3. Kwa nini Bahá'u'lláh hakujihusisha na masuala ya baraza la Sulṭán alipokuwa anaishi katika mji mkuu? ___________________

4. Balozi wa Uajemi alitumiaje fursa hii ya ukataaji wa Bahá'u'lláh kujihusisha na masuala ya wajumbe wa baraza na malengo yao yasiyokuwa yenye thamani? ___________________

5. Je, Yeye alihamishiwa wapi baadaye? ___________________

6. Kwa nini Serikali ya Uajemi ilitaka apelekwe mbali zaidi kutoka mipaka yake? ___________________

7. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini alipopokea habari za uhamisho Wake kutoka Constantinople? ___________________

8. Je, waziri mkuu alisema nini aliposoma barua ya Bahá'u'lláh? ___________________

9. Bahá'u'lláh aliwasili lini huko Adrianople? ___________________

10. Ni kwa muda gani Yeye alibakia katika mji huo? ___________________

11. Ni tukio gani la muhimu ambalo lilitukia huko Adrianople? ___________________

12. Tangazo la Dhima ya Bahá'u'lláh kwa jamii ya wanadamu lilipitia hatua ngapi? ___________________

13. Je, hatua ya kwanza ilikuwa ipi? ________________________________________

________________________________________________________________

14. Je, hatua ya pili ilikuwa ipi? ________________________________________

________________________________________________________________

15. Je, hatua ya tatu ilikuwa ipi? ________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 24

Upinzani dhahiri wa Mírzá Yaḥyá dhidi ya Bahá'u'lláh huko Adrianople ulisababisha msukosuko mkubwa miongoni mwa kundi dogo la wahamishwa, ambao wengi wao ndio kwanza walikuwa wanaanza kuona kianga cha Daraja Bahá'u'lláh. Hii iliwapa maadui wa Hoja, ambao nyuma yao kulikuwa na nguvu ya serikali mbili — ya Uajemi na ya Ottoman — fursa waliyoihitaji ya kushambulia kwa pigo lingine Imani changa ya Mungu. Ghafla asubuhi moja nyumba ya Bahá'u'lláh ilizungukwa na askari, na kila mmoja aliambiwa ajiandae kuondoka mara moja. Kwa muda, hakuna aliyejua hatma yao ingekuwa nini. Hofu kubwa katika mioyo ya wengi ulikuwa utengano kutoka kwa Mpendwa wao, kwa sababu zilikuwepo tetesi kuwa Bahá'u'lláh na familia Yake wangehamishwa kwenda sehemu moja na wengine wangelazimishwa kutawanyika. Mwishowe, ikawa wazi kuwa Bahá'u'lláh angehamishiwa kwenye mji-gereza wa 'Akká, na Mírzá Yaḥyá kwenye kisiwa cha Cyprus. Wengi wa wahamishwa, takriban watu sabini, walipelekwa 'Akká, wakiwemo pia wafuasi wawili waovu kabisa wa Mírzá Yaḥyá. Kwa upande mwingine, wanne miongoni mwa wenzi wa Bahá'u'lláh, walihamishwa pamoja na kundi la Mírzá Yaḥyá kwenda Cyprus.

Bahá'u'lláh na familia Yake waliondoka Adrianople mnamo tarehe 12 Agosti 1868, na baada ya safari ya taabu kwa nchi kavu na bahari, waliwasili 'Akká mnamo tarehe 31 Agosti. Wakazi wa 'Akká walizoea kuwasili kwa wafungwa, kwa kuwa mji huo ulitumiwa na watawala wa Ottoman kama mahali pa uhamisho kwa ajili ya wahalifu na wachochezi. Safari hii, waliambiwa kwamba hao wapya wanaowasili walikuwa maadui wa Serikali, wa Mungu na dini Yake. Sulṭáni aliamuru wawekwe katika kifungo kikali, akitumaini kwamba ukali wa hali ngumu za 'Akká hatimaye ungewaangamiza. Amri ya Sulṭáni ilisomwa hadharani msikitini, na ilieleweka kwa wote kwamba hawa Waajemi wamehukumiwa kifungo cha kudumu na kwamba ushirikiano nao ulikatazwa kabisa.

Baada ya kushuka kutoka chomboni huko 'Akká, wahamishwa walipelekwa kwenye kambi ya jeshi, sehemu moja yake ndio ingekuwa gereza lao. Usiku wa kwanza, walinyimwa chakula na kinywaji, na baadaye kila mmoja aligawiwa mikate mitatu hafifu kila siku. Mara, kila mmoja akaugua, isipokuwa wawili, na baada ya muda mfupi, watatu miongoni mwao walifariki. Walinzi walikataa kuzika wale maiti bila kulipwa gharama zinazohitajika. Zulia dogo la sala lililotumiwa na Bahá'u'lláh liliuzwa, na kiasi cha fedha kilichopatikana walipewa wale walinzi. Baadaye, ilijulikana kwamba hawakutimiza ahadi yao na waliwazika wale maiti bila kuwaosha, bila sanda na bila majeneza. Kwa ukweli walikuwa wemepewa maradufu ya kiasi kilicho hitajika kwa mazishi.

Ingawa hali za kifungo pole pole zilikuwa zikiboreshwa, miaka ya mwanzoni huko ‘Akká ilikuwa kipindi cha mateso makali kwa Bahá’u’lláh. Yale aliyoyavumilia huko Síyáh-Chál Alisababishiwa na maadui wa nje wa Imani tu. Ile ghasia ya kule Adrianople ilikuwa ya ndani kwa asili yake. Hali ya hatari ya ile miaka ya mwanzoni huko ‘Akká, walakini, ilikuwa ni matokeo ya kazi za maadui wa Imani wa nje na wa ndani pia. Yeye Mwenyewe amekirejelea kipindi hiki katika maneno kama yafuatayo:

> **“Ujue kwamba wakati wa kuwasili Kwetu mahali hapa, tulichagua kupaita ‘Gereza Kuu Kabisa’. Ingawa wakati uliopita katika nchi nyingine (Ṭihrán) tuliwekwa katika minyororo na pingu, bado tulikataa kupaita kwa jina hilo. Sema: Fikirini juu ya jambo hilo, Enyi mliojaliwa ufahamu!”[47]**

Licha ya amri ya Sulṭán kwamba asiwepo mtu wa kushirikiana na Bahá’u’lláh na familia Yake, idadi ya waumini huko Uajemi walifanya safari ndefu ya kwenda ‘Akká, aghalabu kwa miguu, wakitumaini kwamba wangeweza kuruhusiwa kufika mbele Yake. Walipowasili, roho hizi zilizojifunga, wakishindwa kumkaribia, walisimama mbali wakielekea gereza Lake, wakiridhika kuona japo kidogo tu mwili Wake kupitia nondo za dirisha Lake. Kuuona mkono Wake uliobarikiwa ukiwapungia ilikuwa tuzo tosha kwa safari ya miezi waliyofanya, na wengi wao hapo wangerudi nyumbani, wakishukuru kwa baraka ambayo wameipata.

Tukio la kuhuzunisha mno katika kipindi hiki ni kifo cha ghafla cha Mírzá Mihdí mwanae Bahá’u’lláh, aliyejulikana kama Tawi Safi Kabisa. Jioni moja alikuwa juu ya paa la kambi, akitembea huku na huko katika sala na tafakari, ndipo alipoanguka kupitia dirisha dogo la mwangaza lililokuwa juu ya paa, hadi kwenye kasha la mbao juu ya sakafu chini. Mbavu zake zilichomwa, na ingawa daktari aliitwa kuja ndani, hapakuwa na la kufanya. Katika muda wa saa ishirini na mbili alikuwa amekwishafariki. Kabla hajafariki, Bahá’u’lláh alimuuliza Tawi Safi Kabisa kile alichotamani. Yeye alijibu: “Ningependa watu wa Bahá waweze kufika mbele Yako.” “Na hivyo itakuwa,” Bahá’u’lláh alisema. “Mungu atakukubalia matakwa yako.”[48]

Japo mateso ya Bahá’u’lláh yalikuwa makali mno katika Gereza Kuu Kabisa, lazima ikumbukwe kwamba uhamisho Wake kwenda ‘Akká ulikuwa utimilizo wa utabiri wa zamani. Ilikuwa ni huko ‘Akká ambako Jua la Ukweli lingewaka kwa miaka ishirini na nne katika mngao wake kamili. Ingekuwa katika kipindi hiki wakati akiutembelea Mlima Karmeli ulioko Haifa, Bahá’u’lláh angemuonyesha ‘Abdu’l-Bahá mahali ambapo kaburi Takatifu la Báb baadaye lingejengwa. Kaburi Lake mwenyewe hapo Bahjí, ambalo lingekuwa katika ujirani wa ‘Akká ndilo lingekuwa Pahali Patakatifu Kabisa duniani, ambako waumini wa dunia nzima watageukia wakati wa kusali kila siku. Ni katika viwanja vilivyo jirani ya Kaburi Takatifu la Báb kwamba makao makuu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yangesitawishwa. Ile miji pacha ya Haifa na ‘Akká ingekuwa makao makuu ya kiroho na kiutawala ya ulimwengu wa Imani ya Kibahá’í. Hivyo, ni pamoja na maneno haya, katika Waraka uliofunuliwa katika miaka ya mwanzo ya kukaa Adrianople, Bahá’u’lláh alidokeza kuhusu uhamisho Wake kwenda ‘Akká:

> **“Tulipofika tulikaribishwa na beramu za mwangaza, ndipo Sauti ya Roho iliita ikisema: ‘Punde tu vyote viishivyo duniani vitaorodheshwa chini ya beramu hizi.’”[49]**

1. Jinsi gani maadui wa Imani kule Adrianople walitumia matatizo aliyosababishwa na Mírzá Yaḥyá kwa manufaa yao? ____________________________________________
_______________________________________________________________________

2. Je, Bahá'u'lláh alihamishiwa wapi baadaye? ________________________________

3. Je, Mírzá Yaḥyá alipelekwa wapi? ____________________________________

4. Je, wangapi waliandamanana Bahá'u'lláh kwenda 'Akká? ___________________

5. Je, unafikiri kwanini baadhi ya wafuasi wa Bahá'u'lláh walipelekwa Cyprus pamoja na Mírzá Yaḥyá na wawili kati ya wasaidizi wa Yaḥyá walipelekwa 'Akká? ______
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________

6. Je, Bahá'u'lláh aliondoka tarehe ngapi Adrianople? ___________________________

7. Je, Yeye aliwasili huko 'Akká tarehe ngapi? _______________________________

8. Je, Sulṭáni alitoa amri gani kuhusu kifungo cha Bahá'u'lláh na waumini waliokuwa wakiandamana Naye? _____________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________

9. Watu wa 'Akká walijuaje kuhusu amri hizo? _______________________________
_______________________________________________________________________

10. Je, Bahá'u'lláh na wenzi Wake walipelekwa wapi walipowasili huko 'Akká? _____
_______________________________________________________________________

11. Katika maneno yako mwenyewe eleza hali za siku zao chache za mwanzo humo gerezani: _________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________

12. Bahá'u'lláh aliita 'Akká kwa jina gani? ___________________________________

13. Ni tukio gani la kuhuzunisha mno lilitokea wakati wa miaka ya mwanzoni huko 'Akká?

____________________________________________________________

14. Ni katika mazingira gani mahujaji wa mwanzoni walivyokuwa wakifika 'Akká? ___

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

15. Kwa maneno yako mwenyewe elezea mazingira ya kifo cha Tawi Safi Kabisa.

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

16. Je, Bahá'u'lláh alikaa 'Akká na katika ujirani wake kwa miaka mingapi? __________

17. Bahá'u'lláh alimwonesha nini 'Abdu'l-Bahá walipokuwa wanatembea juu ya Mlima Carmel huko Haifa? ________________________________________

18. Ni wapi Pahali Patakatifu Kabisa duniani na pako katika nchi gani? ______________

____________________________________________________________

19. Je, makao makuu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yako wapi? _______________

____________________________________________________________

20. Je, makao makuu ya kiroho na ya kiutawala ya ulimwengu wa Imani ya Bahá'í yako wapi? ____________________________________________________

____________________________________________________________

21. Je, unajua mahujaji wanafanya nini hivi leo wanapotembelea Haifa na 'Akká? Labda ungependa kumuuliza rafiki mmoja katika jamii yenu ambaye amewahi kwenda Nchi Takatifu kuhiji asimulie tajiriba yake.

## SEHEMU YA 25

Alipokuwa ‘Akká Bahá’u’lláh aliendelea na utangazaji Wake kwa watu wote. Hapa yapo baadhi ya mafungu ambayo Yeye aliandika kutoka Adrianople na ‘Akká kwa wafalme na watawala wa ulimwengu:

Kwa Mfalme wa Wafaransa, Napoleon III:

**“Ee Mfalme wa Paris! Mwambie kasisi asipige kengele tena. Kwa Mungu, Mmoja wa Kweli! Kengele Yenye Uwezo Kabisa imetokea katika umbo la Yule Ambaye ni Jina Kuu Kabisa . . .”**[50]

Kwa Nicolaevitch Alexander II Czar wa Urusi:

**“Inuka wewe miongoni mwa watu katika jina la Hoja hii ishurutishayo vyote, na yaite, basi, mataifa kwa Mungu, Aliyetukuka, Aliye mkuu.”**[51]

Kwa Malkia Victoria wa Uingereza:

**“Weka kando tamaa yako, na elekeza basi moyo wako kwa Bwana wako, Mkale wa Siku. Tunakutaja wewe kwa ajili ya Mungu, na kutamani kwamba jina lako liweze kutukuzwa kupitia kumbukumbu yako kwa Mungu, Muumba wa dunia na mbingu.”**[52]

Kwa William I, Mfalme wa Prussia:

**“Jihadharini isije kiburi kikakuzuia kutambua Chimbuko la Ufunuo Mtakatifu, na tamaa za kidunia zikufungie nje kama kwa utando, kutoka kwa Bwana wa Kiti cha enzi juu na wa dunia chini.”**[53]

Kwa Francis-Joseph, Mfalme wa Austria:

**“Fungua macho yako, ili uweze kutazama Muono huu mtukufu, na kumtambua Yule Ambaye unamuita wakati wa mchana na katika majira ya usiku, na uangalie Mwanga ambao huwaka juu ya Upeo huu ung’aao.”**[54]

Kwa Sulṭáni ‘Abdu’l-‘Azíz wa Ufalme wa Ottoman:

**“Usiweke kando ucha Mungu, na uwe wa wale ambao hutenda kwa unyofu. Wakusanye kando yako mawaziri wale ambao kutoka kwao unaweza kuhisi manukato ya imani na ya haki, na shauriana nao, na uchague chochote kile kilicho kizuri kabisa machoni pako, na uwe wa wale ambao hutenda kwa ukarimu.”**[55]

Kwa Náṣiri’d-Dín Sháh wa Uajemi:

**“Tunaomba kwamba, kutoka ukarimu Wake — atukuzwe Yeye — Yeye atafungulia, kupitia kifungo hiki, shingo za watu kutoka minyororo na pingu, na kuwafanya wageukie kwa nyuso aminifu, kuelekea Uso Wake, Yule Ambaye ni Mwenye nguvu, Mkarimu. Yeye yuko tayari kumjibu yeyote amwitaye, na Yeye yu karibu ya wale wazungumzao Naye.”**[56]

Kwa watawala wa Amerika na Marais wa Jamhuri zake:

> **“Fungeni ninyi waliovunjwa kwa mikono ya haki, na mpondeni mdhalimu ambaye husitawi kwa fimbo ya amri za Bwana Wenu, Muamuru, Mwenye hekima kabisa.”**[57]

Kwa Papa Pius IX:

> **“Neno ambalo Mwana alilificha limedhihirishwa. Limetelemshwa katika umbile la hekalu ya mwanadamu katika siku hii. Abarikiwe Bwana Ambaye ni Baba! Yeye, kwa ukweli, amekuja kwa mataifa katika ufahari Wake mkuu kabisa.”**[58]

Kwa shirika zima la watawa wa Kanisa la Kikristo:

> **“Enyi umati wa watawa! Msijitenge wenyewe makanisani na utawani. Tokeni nje kwa ruhusa Yangu, na jishughulisheni wenyewe na kile ambacho kitanufaisha roho zenu na roho za watu.”**[59]

## SEHEMU YA 26

Miezi minne baada ya kifo cha ghafla cha Tawi Safi Kabisa, Bahá’u’lláh na wenzi Wake ililazimika waondolewe kutoka kambini kupisha vikosi vya jeshi. Yeye na familia Yake walihamishiwa katika nyumba kadhaa kwa vipindi vifupi vifupi na hatimaye walihamia katika nyumba ijulikanayo leo kama Nyumba ya ‘Abbúd. Waliendelea kuwa chini ya ulinzi na walizungukwa na watu ambao, wakishawishika na amri za Sulṭáni, hawakuwa rafiki na waliwaonesha uhasama kwao.

Kadiri muda ulivyopita, watu wa ‘Akká walikuja kutambua utovu wa hatia wa kikundi hiki kidogo cha wahamishwa kutoka Uajemi, na hali za kifungo chao zililegezwa. Sehemu kubwa ya mabadiliko ilisababishwa na ‘Abdu’l-Bahá, ambaye alikuwa akiwasiliana sana na wakazi wa mji huo na aliweza kuwaonesha nia ya kweli ya Wabahá’i na moyo wa mafundisho ya Baba Yake. Hatimaye, Bahá’u’lláh angeweza kutoka mji wa ‘Akká na kuzitembelea sehemu jirani. Baada ya kufungwa kwa muda mrefu mno ndani ya kuta za mji wenye ukiwa, Bahá’u’lláh sasa angeweza kutumia wakati huko mashambani na kufurahia uzuri na hali ya kijani ya mimea ya kiasili ambayo Aliipenda mno.

Miaka ya mwisho ya maisha ya Bahá’u’lláh ilitumiwa ndani ya Jumba la Bahjí, nje kidogo tu ya ‘Akká. Lilijengwa Yeye alipokuwa amefungwa ndani ya kuta za mji huo, liliachwa na mwenyewe wakati wa mlipuko wa magonjwa katika eneo hilo. ‘Abdu’l-Bahá aliweza kulipata kwa ajili ya Baba Yake mpendwa, kwanza kwa kulikodi na baadaye kulinunua moja kwa moja.

Hadi hadi mwelekeo wa watu siyo tu wa ‘Akká bali pia sehemu jirani za Syria na Lebanon mwelekeo wao kwa Bahá’u’lláh na wafuasi Wake ulikuwa umebadilika kabisa. Ingawa amri ya Sulṭáni bado ilikuwa haijaondolewa, na kwa nje Yeye alikuwa mfungwa katika kifungo cha masharti makali, kwa uhalisi, Yeye alikuwa akistahiwa na kuheshimiwa kama mfalme. Hata maafisa wa sehemu hiyo wangekuja kupata ushauri Wake na mawaidha. Hivyo ndivyo ilivyo nguvu ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh wa kubadilisha mioyo ya watu.

Katika miaka hiyo huko ‘Akká na Bahjí, Bahá’u’lláh alifunua vitabu vingi vya mwongozo ambao utaiwezesha jamii ya wanadamu kuujenga ustaarabu mtukufu wa ulimwengu. Kitabu chenye nguvu kabisa kati ya kazi Zake zilizotiririka kutoka kwenye kalamu Yake kilikuwa ni Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Kitakatifu Kabisa cha Kipindi Chake Kitakatifu, kilichofunuliwa katika Nyumba ya ‘Abbúd mnamo mwaka 1873 hivi. Shoghi Effendi, akirejea kwenye Maandiko ya Bahá’u’lláh katika Nchi Takatifu, anaeleza:

> **“Maandiko ya Bahá’u’lláh katika kipindi hiki, kama tukiangalia uwanda mkubwa ambao yanaukumbatia, huonekana kuwa yanaangukia katika aina tatu tofauti. Ya kwanza hujumuisha maandiko ambayo hufanya mfuatano kwa utangazaji wa Dhima Yake huko Adrianople. Ya pili hujumuisha sheria na amri za Kipindi Chake Kitakatifu, ambazo, kwa sehemu kubwa, zimeandikwa katika Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa. Ile aina ya tatu sharti ipewe zile Nyaraka ambazo kwa sehemu hutamka wazi na kwa sehemu huthibitisha yale mafundisho ya kimsingi na kanuni ambavyo hufanya msingi wa Kipindi Kitakatifu hicho.”**[60]

Upanuzi mkubwa wa Imani ya Bahá’u’lláh katika ulimwengu wa Magharibi haukuanza wakati wa uhai Wake yeye mwenyewe, upanuzi huu ilibidi ungojee kipindi cha Utumishi wa ‘Abdu’l-Bahá.Mafundisho Yake, walakini, yalikuwa yametambulishwa katika nchi za Magharibi, na watu wachache huko walikuwa wakifahamu juu ya Mfungwa wa ‘Akká Ambaye alikuwa na mvuto wa ajabu juu ya wale ambao alikutana nao. Katika kipindi cha majira ya kuchipua ya mwaka 1890, kuelekea mwisho wa maisha ya Bahá’u’lláh, Edward Granville Browne, mwanazuoni maarufu kutoka Cambridge, Uingereza, alikuja kukutana Naye. Vifungu vifuatavyo hutoka kwenye kumbukumbu yake ya mahojiano hayo ya kihistoria:

> “. . . mtu aliyekuwa ananiongoza alisita kidogo wakati navua viatu vyangu. Ndipo, upesi kwa mkono, aliondoa pazia, na kurudi nyuma, mara nilipopita yeye alilirudisha pazia; na mimi nilijikuta ndani ya chumba kikubwa, ambamo kwenye upande wa juu ukutani kulikuwa kochi lisilo na egemeo, ambapo mkabala na mlango viliwekwa viti viwili ama vitatu. Ingawa nilihisi kwa mbali ni wapi nilikokuwa nakwenda na ni nani ningemuona (nilikuwa sijapewa maelezo yoyote dhahiri) sekunde moja au mbili zilipita, ndipo kwa mshangao na kicho, kwa uhakika nilitambua kuwa humo chumbani alikuwepo mtu mwingine. Pembeni, ambapo kochi lilikutana na ukuta, lilikuwa limekaa umbo la ajabu na adhama, alikuwa amevaa kofia ya kitambaa laini, iitwayo *táji* na madarweshi (lakini yenye urefu na muundo usio wa kawaida), kwenye sehemu ya chini yake ilikuwa imezungushiwa kilemba kidogo cheupe. Uso wa yule ambaye nilimtazama kamwe siwezi kuusahau, ingawa siwezi kuuelezea. Macho yake makali yalionekana kusoma roho yenyewe ya mtu; uwezo na mamlaka vilikaa juu ya paji pana la uso wake; wakati ile mistari iliyochimba ndani ya paji la uso na uso vilimaanisha umri mkubwa ambao ulikanushwa na zile nywele nyeusi sana na ndevu zilizoshuka chini katika usitawi usioweza kuelezeka hadi kufika kiunoni. Hakuna haja ya kuuliza nilisimama mbele ya nani, nilipoinama mbele ya yule ambaye ndiye kusudi la moyo wa ibada na upendo ambavyo wafalme wangevihusudu na watawala wangevitamani bila kuvipata ng’o!
>
> “Sauti pole na yenye heshima ilinikaribisha nikae, na halafu ikaendelea: — **‘Sifa iwe kwa Mungu kwamba umefikia! . . . Umekuja kumuona mfungwa na mhamishwa. . . . Tunatamani tu mema ya ulimwengu na furaha ya mataifa; walakini wao wanatudhania sisi ni wachochezi wa ugomvi na maasi astahiliye kifungo na uhamisho . . . Kwamba mataifa yote yawe taifa moja katika imani na**

**watu wote wawe kama ndugu; kwamba mafundo ya upendo na umoja miongoni mwa wanadamu yaimarishwe; kwamba tofauti za dini zikome, na tofauti za kimbari zifutwe — kuna madhara gani katika jambo hili? . . . Walakini hivyo ndivyo itakavyokuwa; ugomvi huu usio na faida; vita hivi viharibifu vitakwisha, na 'Amani Kuu Kabisa' itafika. . . . Je, ninyi huko Ulaya hamhitaji hili pia? Siyo hiki ambacho Kristo alikitabiri? . . . Walakini tunawaona wafalme wenu na watawala wakitoa hazina zao kwa wingi mno na kwa uhuru zaidi juu ya njia za uteketezaji wa jamii ya wanadamu kuliko kile ambacho kingesaidia kuleta furaha ya wanadamu. . . . Taabu hizi na umwagaji damu huu na mafarakano sharti vikome, na watu wote kuwa kama jamaa moja na familia moja. . . . Acha mtu asijuvune katika hili, kwamba yeye huipenda nchi yake; bali muache ajivunie katika hili, kwamba yeye huipenda aina yake. . . .'"[61]**

1. Ni katika mazingira gani Bahá'u'lláh na wenzi Wake waliondolewa kutoka kwenye yale makambi? ________________________________________

2. Ni lipi jina la ile nyumba huko 'Akká ambamo Bahá'u'lláh na familia Yake hatimaye walihamia? ________________________________________

3. Hali ya maisha yao huko 'Akká ilibadilikaje? ____________________________

   ________________________________________________________

4. Kitu gani kilisababisha mabadiliko haya? ______________________________

   ________________________________________________________

   ________________________________________________________

5. Ni lipi jina la lile jumba ambamo Bahá'u'lláh aliishi miaka ya mwisho wa maisha Yake? ________________________________________________

6. 'Abdu'l-Bahá alilipata Jumba la Bahjí katika mazingira gani? ______________

   ________________________________________________________

7. Ni kazi (maandiko) gani muhimu kabisa iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh katika miaka Aliyokuwa huko 'Akká? ________________________________________

   ________________________________________________________

8. Kazi hiyo ilifunuliwa wapi na lini? __________________________________

   ________________________________________________________

9. Ni zipi aina tatu ambamo, kama ilivyoelezwa na Shoghi Effendi, Maandiko ya Bahá'u'lláh ya kipindi hiki zinaangukia?

a. ______________________________

______________________________

______________________________

b. ______________________________

______________________________

______________________________

c. ______________________________

______________________________

______________________________

10. Ni zipi baadhi ya sheria za Kipindi Kitakatifu cha Bahá'u'lláh? ____________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

11. Ni yapi baadhi ya mafundisho na kanuni za Kipindi Kitakatifu Chake? ________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

12. Edward Granville Browne alikuwa nani? ____________________

______________________________

13. Edward Granville Browne anatumia maneno yapi kueleza hisia alizopata, alipokuwa anainama mbele ya Bahá'u'lláh, alijihisi vipi mbele Yake? ______________

______________________________

______________________________

14. Kufuatana na maneno yaliyoandikwa na Edward Granville Browne:

– Bahá'u'lláh Alisema angependa nini? ____________________

______________________________

– Alisema angependa mataifa yote yaweje? ____________________

______________________________

– Angependa kitu gani kiimarishwe? ________________________________________

________________________________________________________________________

– Alitaka kitu gani kikomeshwe? ________________________________________

– Aliitisha kitu gani kifutwe? ________________________________________

– Yeye anabashiri kuwa kitu gani kitakuja kutokea? __________________________

________________________________________________________________________

– Bahá'u'lláh anasema kitu gani tusijivunie? ______________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 27

Kitáb-i-Aqdas siyo kitabu kikubwa; kina vifungu 190 tu. Ndani mwake, walakini, zimo sheria na kanuni za msingi kwa ajili ya ustaarabu wa ulimwengu wa siku za mbele. Shoghi Effendi anakiita Kitabu Mama cha Kipindi Kitakatifu cha Bahá'u'lláh na Katiba ya Utaratibu Wake Mpya wa Ulimwengu. Mtasoma mafungu kutoka Kitáb-i-Aqdas tena na tena katika maisha yako yote mtakapokuwa mnajitahidi kufungamanisha fikra zenu na vitendo kulingana na amri za Mungu. Kwa hivi sasa, inapendekezwa kwamba mkariri vifungu vitano vya mwanzo.

> **"Wajibu wa kwanza ulioariwa na Mungu kwa watumishi Wake ni utambuzi wa Yule Ambaye ni Chimbuko la Ufunuo Wake na Chemchemi ya Sheria Zake, Ambaye huwakilisha Uungu katika Ufalme wa Hoja Yake na ulimwengu wa muumbo pia. Yeyote atimizaye wajibu huu amefikia mema yote; na yeyote ambaye amenyimwa jambo hilo amepotea, ingawa awe mwanzilishi wa kila tendo jema. Imempasa kila mmoja afikiaye daraja hili bora kabisa, kilele hiki cha utukufu mkuu kupita, kutii kila amri ya Yeye Ambaye ni Haja ya ulimwengu. Wajibu hizi pacha hazitenganiki. Moja haikubaliki bila nyingine. Hivyo ndivyo ilivyoamriwa na Yeye Ambaye ni chanzo cha mvuto Mtakatifu.**

> **"Wale ambao Mungu amewajalia umaizi watatambua upesi kuwa mafundisho yaliyowekwa na Mungu hufanya njia bora kabisa kwa udumishaji wa utaratibu katika ulimwengu na usalama wa watu wake. Yeyote ambaye huyapa kisogo huhesabiwa miongoni mwa watu duni na wajinga.Sisi, kwa kweli, tumewaamuru kukataa misukumo ya shauku zenu ovu na tamaa mbaya, na msivuke mipaka ambayo Kalamu ya Aliye Juu Kabisa imeiweka, kwa kuwa hizi ndizo pumzi za uzima kwa vitu vyote vilivyoumbwa. Bahari za Hekima Takatifu na Kauli Takatifu zimeumuka kwa pumzi ya upepo mwanana wa Mwenye Rehema Kabisa. Harakieni kunywa funda yenu, Enyi watu wenye ufahamu! Wale ambao wamevunja Agano la Mungu kwa kuvunja Amri Zake, na wamegeuka na kuondoka ghafla, hawa wamekosa vya kuhuzunisha mbele ya macho ya Mungu, Mwenye vyote, Aliye Juu kabisa.**


**“Enyi watu wa ulimwengu! Jueni kwa uhakika kuwa amri Zangu ni taa za Majaaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za Rehema Yangu kwa viumbe Wangu.Hivyo ndivyo ilivyotelemshwa kutoka mbingu ya Mapenzi ya Bwana wako, Bwana wa Ufunuo. Kama mtu yeyote angeonja utamu wa maneno ambayo midomo ya Mwenye Rehema Kabisa imekusudia kuyatamka, ingawa hazina zote za dunia ziwe kwenye milki Yake, yeye angezikataa moja na zote ili aweze kuthibitisha ukweli wa japo moja ya amri Zake, ziking’aa juu ya Chimbuko la matunzo Yake ya fadhila na wema wa upendo.**

**“Sema: kutoka Sheria Zangu harufu nzuri ya vazi Langu inaweza kunuswa, na kwa msaada wake bendera za Ushindi zitasimikwa juu ya vilele vya juu kabisa. Ulimi wa Uwezo Wangu kutoka mbingu ya Utukufu Wangu wenye enzi kuu, umewaambia viumbe Wangu maneno haya: ‘Tiini amri Zangu, kwa ajili ya upendo wa uzuri Wangu.’ Ni mwenye furaha mpenzi ambaye amevuta pumzi ya manukato matakatifu ya Mpendwa wake Kabisa kutoka maneno haya, yaliyojaa marashi ya neema ambayo hakuna ulimi uwezao kuelezea. Kwa Uhai Wangu! Yeye ambaye amekunywa mvinyo bora wa haki mikono kutoka mikono ya fadhili Yangu ya ukarimu atazungukia amri Zangu ambazo hung’aa juu ya Chimbuko la muumbo Wangu.**

**“Msifikirie kuwa Tumewafunulia tu orodha ya sheria. La, bali, Tumefungua Mvinyo bora kwa vidole vyenye uwezo na nguvu. Kwa hili hushuhudia kile ambacho Kalamu ya Ufunuo imefunua. Tafakari juu ya hili, Enyi watu wenye umaizi!”[62]**

## SEHEMU YA 28

Uhamisho wa mfululizo wa Bahá’u’lláh, ingawa inavyoonekana ulifanywa kwa amri za nguvu za wadhalimu wawili kwa kushirikiana na maofisa fisadi wa kidini, kiuhalisi ulielekezwa na Mkono wa Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Nguvu za kiroho zilizoachiliwa kadri Mdhihirishaji wa Mungu alivyokuwa anahamishwa kutoka mahali hadi mahali — kutoka nchi Yake ya asili hadi kwenye fuko za ‘Akká ambapo katika ujirani wake yangesimamishwa makao makuu ya kiroho na ya kiutawala ya Imani Yake, haziwezi kupimika. Ramani iliyopo hapo chini inaonyesha njia za uhamisho Wake mbalimbali, mnaifahamu ramani hii kutoka masomo yenu ya Kitabu cha 2. Kufuatana na umaizi mliopata katika kitengo hiki, chukua muda kidogo kutafakari juu ya maana za kiroho za yale yaliyotokea katika kila sehemu muhimu. Na wakati mnatafakari matukio lukuki yanayohusu maisha Yake na kupata kianga zaidi juu ya ukuu Wake na utukufu, uwezo na ufahari Wake vinakumbusha maneno Yake: “Yule Ambaye amefichwa daima kutoka macho ya watu kamwe hawezi kujulikana isipokuwa kupitia Mdhihirishaji Wake, na Mdhihirishaji Wake hawezi kutoa ushahidi mkubwa zaidi wa ukweli wa Dhima Yake kuliko ushahidi wa Nafsi Yake Mwenyewe.”




## SEHEMU YA 29

Katika kipindi cha miaka ambamo Mdhihirishaji wa Mungu anatembea miongoni mwetu nguvu Zake zisizo za kawaida huenea ulimwenguni pote, zikisababisha mabadiliko makubwa katika uhalisi wa vitu vyote vilivyoumbwa. Katika Siku hii Tukufu, Bahá'u'lláh alifunua Neno la Mungu kwa jamii ya wanadamu kwa takriban miaka arobaini, akiujalia ulimwengu wa uwepo nguvu ambazo hazijadhihiri zisizo na mwisho, ambazo kujitokeza kwake kutasababisha ustaarabu wa uzuri usiowazika. Miongo hii minne ya Ufunuo mtakatifu uendeleao ilifikia mwisho mnamo tarehe 29 Mei 1892.

Miezi tisa kabla ya kupaa kwake, Bahá'u'lláh alionyesha shauku Yake ya kuondoka kutoka ulimwengu huu. Tangu wakati huo na kuendelea, ilizidi kuwa wazi kutokana na namna ya maneno aliyokuwa akiyasema kwamba mwisho wa maisha Yake katika uso huu wa kidunia ulikuwa unakaribia. Usiku wa tarehe 8 Mei, alipata homa kidogo. Homa iliongezeka siku iliyofuata, lakini halafu ilionekana kutoweka. Aliendelea kuwaruhusu baadhi ya marafiki na mahujaji kukutana Naye. Lakini punde tu ilidhihirika kwamba alikuwa anaumwa. Homa Yake ilirudi, wakati huu kwa nguvu zaidi kuliko mwanzoni, na hali Yake iliendelea kuwa mbaya. Kwenye saa ya alfajiri tarehe 29 Mei, katika mwaka wa 75 wa maisha Yake, roho Yake ilipaa kutoka ulimwengu huu.

Siku sita kabla hajafariki, aliwaita mbele Yake wote waliokusanyika kwenye Jumba la Bahjí, kwa ule ambao ungekuwa mkutano wa mwisho pamoja Naye. Akiwa amepumzika kitandani, akisaidiwa na mmoja kati ya watoto Wake wa kiume, Yeye aliwaambia.

“Nimeridhishwa nanyi nyote,” alisema. “Mmefanya huduma nyingi, mmekuwa makini sana katika kazi zenu. Mmekuja hapa kila asubuhi na kila jioni. Mungu awasaidie kubakia wamoja. Yeye awasaidie kuitukuza Hoja ya Bwana wa uzima.”[63] Machozi yalimiminika kutoka macho ya wale waliokusanyika kando Yake.

Habari za kufariki Kwake mara tu zilipelekwa kwa Sulṭáni kwa simu ya maandishi. Ujumbe ulianza kwa maneno haya “Jua la Bahá limetua” na uliendelea kumuarifu Sulṭáni juu ya mipango ya kuzika mabaki matakatifu karibu na lile Jumba. Chumba kidogo ndani ya nyumba jirani upande wa magharibi wa Jumba hilo kilichaguliwa, na muda mfupi baada ya jua kutua siku hiyo hiyo ya kupaa Kwake, Mwili Wake ulizikwa. Nabíl huelezea uchungu wa siku hizo katika maneno haya: “Mimi ninafikiri, ghasia ya kiroho iliyosababishwa katika ulimwengu wa vumbi imesababisha malimwengu yote ya Mungu kutetemeka. . . . Ulimi wangu wa ndani na wa nje havina uwezo wa kueleza hali ambayo tulikuwemo. . . . Katikati ya vurugu iliyoenea umati wa wakazi wa ‘Akká na wa vijiji jirani, waliosongamana mashambani kuzunguka lile Jumba, waliweza kuonekana wakilia, wakipiga vichwa vyao, na wakionesha huzuni yao kwa sauti.”[64]

Kwa juma moja zima, mfululizo endelevu wa waombolezaji, walikuja kuonesha huzuni yao kwa familia ya Bahá’u’lláh.Watu mashuhuri kutoka kila tabaka za jamii, wakiwemo Waislamu, Wakristo na Wayahudi, washairi, makasisi na maafisa wa serikali, waliunganika katika kusikitikia kifo Chake na katika kusifia wema Wake na ukuu. Wengi wao hata walitoa heshima Kwake kwa maandishi. Heshima kama hizo zilipokelewa kutoka miji ya eneo hilo lote, zote ziliwasilishwa kwa ‘Abdu’l-Bahá, ambaye sasa aliwakilisha Hoja ya Bahá’u’lláh. Walakini, onesho hilo la huzuni, katika maneno ya Mlinzi lilikuwa, “tone tu likilinganishwa na bahari kuu ya huzuni na ushuhuda mwingi wa moyo wa ibada usio na kikomo ambao, wakati wa kutua Jua la Ukweli, ulimwagika kutoka mioyo ya maelfu yasiyohesabika ambao walijiunga na Hoja Yake, na walidhamiria kuiinua juu beramu yake huko Uajemi, India, Urusi, ‘Iráq, Uturuki, Palestina, Misri na Syria.”

Sasa, baada ya kutafakari kwa muda mfupi juu ya vifungu vilivyopo hapo juu, unda vikundi vya watu wawili wawili katika kikundi chako na kwa zamu kila mtu na mwenzake simulia tukio la kupaa kwa Bahá’u’lláh katika maneno yako mwenyewe.

## SEHEMU YA 30

Baada ya kufariki Bahá’u’lláh, Nabíl alichaguliwa na ‘Abdu’l-Bahá kuchagua vile vifungu ambavyo hufanya maandiko ya Waraka wa Kuzuru. Waraka huu hutongolewa katika Makaburi Matakatifu ya Bahá’u’lláh na Báb. Hutumiwa mara kwa mara pia katika kuadhimisha kumbukizi Zao. Kupaa kwa Bahá’u’lláh huadhimishwa katika saa za mapema alfajiri tarehe 29 Mei. Kadri utavyoshiriki katika mikusanyiko kama hii katika jumuiya yako, utapata uzoefu mzuri wa maneno ya Waraka huu mzuri kabisa, kama bado hujafanya hivyo. Inafaa kwa hiyo, tunapomaliza kozi hii juu ya maisha ya Bahá’u’lláh, kuwa wewe usome na kutafakari juu ya Waraka huo:

> **“Sifa ambayo imepambazuka kutoka Nafsi Yako tukufu, na utukufu ambao umeng’aa nje kutoka uzuri Wako mwangavu kabisa, viwe juu Yako, Ewe uliye udhihirisho wa Ufahari, na Mfalme wa Umilele, na Bwana wa wote walio mbinguni na duniani! Nashuhudia kwamba kwa kupitia Kwako mamlaka ya**

**Mungu na milki, na ukuu wa Mungu na ufahari Wake, vilifunuliwa, na Nyota za mchana za utukufu wa kale zimetawanya wangavu wao katika mbingu ya amri Yako isiyobatilika, na Uzuri wa Yule Asiyeonekana umeng'aa kutokea juu kwenye upeo wa muumbo. Nashuhudia zaidi kwamba kwa mjongeo wa Kalamu Yako amri Yako 'Uwe' imetimizwa na Siri ya Mungu iliyofichika imefunuliwa, na viumbe vyote vimeumbwa na Ufunuo wote umetelemshwa.**

**"Nashuhudia zaidi, kwamba kupitia uzuri Wako uzuri wa Yule Mwabudiwa umefunuliwa na kupitia uso Wako uso wa Yule Atamaniwaye umeng'aa kote, na kwamba kupitia neno kutoka Kwako Wewe umeamua kati ya viumbe vyote, na kuwafanya wale waliojidhatiti Kwako kupanda kwenye kilele cha utukufu, na makafiri kuanguka katika shimo kubwa lenye kina kirefu kabisa.**

**"Nashuhudia kwamba yeye Ambaye amekujua Wewe amemjua Mungu, na yeye ambaye amefika mbele yako amefika mbele ya Mungu. Ni nyingi, kwa hiyo, baraka ya yule ambaye amekuamini Wewe, na ishara Zako, na amenyenyekea mwenyewe mbele ya enzi Yako, na ameheshimika kwa kukutana Nawe, na amepata ridhaa njema ya Mapenzi Yako, na kukuzungukia Wewe, na kusimama mbele ya kiti Chako cha enzi. Ole wake yule aliyekukosea Wewe, na amekukana Wewe, na kukataa ishara Zako, na kukaidi enzi Yako, na ameinuka dhidi Yako, na kufanya kiburi mbele ya uso Wako, na kupinga ushuhuda Wako, na kukimbia kutoka utawala Wako, na milki Yako, na kuhesabiwa pamoja na makafiri ambao majina yao yameandikwa kwa vidole vya amri Yako juu ya Nyaraka Zako takatifu.**

**"Nipeperushie, basi, juu yangu, Ee Mungu wangu na Mpendwa wangu, kutoka mkono wa kuume wa rehema Yako na Wema Wako wa upendo, pumzi takatifu za fadhili Zako, ili ziniondoe mbali kutoka nafsi yangu mwenyewe na kutoka ulimwengu hadi kwenye viwanja vya ukaribu Wako na mbele Yako. Wewe u mwenye nguvu kufanya kile kikupendezacho. Wewe, kwa kweli, umekuwa mkuu kabisa juu ya vitu vyote.**

**"Kumbukumbu ya Mungu na sifa Yake, na utukufu wa Mungu na fahari Yake, viwe juu Yako, Ewe uliye Uzuri wake! Nashuhudia kwamba jicho la muumbo halijapata kamwe kuona aliyedhulumiwa kama Wewe. Wewe ulizamishwa siku zote za maisha Yako chini ya bahari ya mateso. Kwa wakati mmoja ulikuwa katika minyororo na pingu; kwa wakati mwingine ulitishwa kwa upanga wa maadui Zako. Walakini, licha ya yote haya, Wewe uliwausia watu wote kutii yale yaliyoamriwa Kwako na Yeye ambaye Yu Ajuaye-yote Mwenye Hekima Kabisa.**

**"Roho yangu iwe dhabihu kwa maovu uliyovumilia, na roho yangu iwe fidia kwa taabu ulizostahimili. Ninamsihi Mungu kwa Wewe na kwa wale ambao nyuso zao zimeangaziwa kwa utukufu wa nuru ya uso Wako, na ambao, kwa ajili ya upendo Wako, wametii yote yale waliyoamriwa, kuondoa utando uliyopo kati Yako na viumbe Wako, na kunijalia mema ya ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Wewe, kwa kweli, u Mwenye enzi, Aliye-tukuka kabisa, Mtukufu kabisa, Msamehevu daima, Mwenye Huruma kabisa.**

**"Ubariki, Ee Bwana Mungu wangu, Mti Mtakatifu wa Lote na majani yake, na matawi yake, na vijitawi vyake na mashina yake, na vichipukizi vyake, kadiri**

**majina Yako bora kabisa yatakavyodumu na Sifa Zako tukufu kabisa zitakavyoendelea. Ulinde, basi, kutoka madhara ya mshari na majeshi ya mdhalimu. Wewe, kwa kweli u Mwenye enzi, Mwenye nguvu kabisa. Wabariki pia, Ee Bwana Mungu wangu, watumishi wako na vijakazi wako ambao wamekufikia Wewe. Wewe, kwa kweli, u Mkarimu-kabisa, Ambaye neema Yako haina kikomo. Hakuna Mungu aliyepo ila Wewe, Msamehevu-daima, Mkarimu-Kabisa."**[65]

## SEHEMU YA 31


Kutokana na uzoefu wako mwenyewe, unajua kwamba utapata nafasi nyingi katika miaka ijayo kusimulia hadithi ya maisha ya Bahá'u'lláh. Wewe bila shaka umeshiri hadithi hiyo mara nyiungi tangu ulipomaliza Kitabu cha 2, ambacho kimekupa maelezo mafupi lakini yaliyokamilika ya maisha Yake, kama mojawapo ya mada za kujiimarisha kwa kuzichunguza pamoja na marafiki na majirani wakati wa mfuatano wa matembezi kwenye kaya zao. Kisa ambacho wewe umesoma hivi punde, kina tondoti nyingi zaidi kuliko ilivyo katika Kitabu cha 2, na utaweza kuleta katika maongezi yenu kuhusu uwepo wa Bahá'u'lláh ujuzi mpya ambao umeupata, kuhusu matukio ya maisha Yake, kadri hali inavyoruhusu. Muhimu zaidi hata hivyo, utakuwa ule umaizi ambao umeupata kutoka matukio hayo, kuhusu asili ya Ufunuo Wake, sifa bainifu za Dhima Yake, ukubwa wa nguvu zilizoachiliwa na ujio Wake, na umuhimu kipindi hiki katika historia ya wanadamu. Yoyote iwayo hali — kama ni maongezi mafupi pamoja na mtu ambaye ni mpya kwa Imani, au uwasilishaji unaofanywa wakati wa matembezi ya nyumbani katika kijiji chako au ujirani — ni umaizi huu ambao hatimaye, utaathiri jinsi unavyoongea kuhusu Nafsi ya Bahá'u'lláh kile unachomwambia msikilizaji. Hakika, zitakuwepo nyakati ambapo uwasilishaji wa kawaida tu utahitajika, na kurasa zifuatazo zitaweza kukusaidia katika suala hili.

# Bahá’u’lláh

## *Utukufu wa Mungu*




**Bahá'u'lláh alizaliwa tarehe 12 Novemba 1817 huko Ṭihrán, mji mkuu wa Iran. Kutoka utoto, Wake alionyesha dalili za ukuu. Alipata kiasi kidogo cha mafunzo nyumbani, lakini hakuhitajikwenda shule, kwa kuwa alikuwa amejaliwa na Mungu elimu ya kiasili.**



**Usiku mmoja, baba Yake alipata ndoto ambapo alimuona Bahá’u’lláh akiogelea kwenye bahari. Nuru ambayo ilitoka katika mwili Wake iliangaza kwenye maji. Nywele zake ndefu nyeusi zilielea katika kila pembe na kundi kubwa la samaki lilimfuata, kila mmoja akishikilia kwenye ncha ya unywele. Alikwenda kwa uhuru na bila kuzuiliwa. Ndoto hii ilikuwa mojawapo kati ya ishara nyingi za hatima kuu ambayo ilikuwa ikimsubili Bahá’u’lláh.**



**Baadaye alipokuwa kijana, alipewa nafasi ya juu katika baraza la mfalme lakini aliikataa. Alitaka kutumia muda Wake katika kuwasaidia wanyonge, wangonjwa na maskini, na kutetea hoja ya haki.**



**Alipokuwa na umri wa miaka 27, Bahá'u'lláh alipokea hati ya Maandiko kutoka kwa Báb, Mjumbe mpya wa Mungu, Ambaye alikuwa akiwatayarisha watu kwa ajili ya kuja kwa Mwahidiwa wa Wakati Wote. Bahá'u'lláh aliukubali Ujumbe wa Báb na kuwa mmoja wa wasaidizi Wake wenye nguvu kabisa.**



**Watu wa mamlaka, kwa kutotaka Ukweli uliotajwa na Báb, walianza kuwakamata wale waliomuamini Báb, na hapo ndipo mateso ya Bahá'u'lláh yalipoanza. Katika mwaka 1852, alikamatwa na kufungwa minyororo kwenye moja kati ya magereza mabaya ya Ṭihrán.**



**Katika gereza hili, Mungu alimfunulia Bahá'u'lláh kuwa alikuwa Yule aliyehahidiwa na Báb na Mitume wote waliopita. Kutoka katika shimo hili la giza Jua la Ukweli lilichomoza, likiangazia ulimwengu na kuanzisha Siku mpya katika maisha ya jamii ya wanadamu.**



**Baada ya miezi minne ya kifungo, serikali ilimuhamisha Bahá’u’lláh kutoka nchi aliyozaliwa. Kwenye majira ya baridi kali, Bahá’u’lláh na familia Yake walifanya safari ndefu kutoka Ṭihrán hadi Ba<u>gh</u>dád.**



**Huko Ba<u>gh</u>dád, umashuhuri wa hekima ya Bahá'u'lláh ulienea pande zote. Watu wa kila tabaka walisongamana kwenye nyumba Yake, wakitafuta msaada Wake na ushauri. Serikali, ambayo ilikuwa ikiogopa uwezo wa Bahá'u'lláh, iliamua kumuhamisha hata mbali zaidi na kutoka nyumbani Kwake.**



# Bustan ya Riḍván
## Aprili 1863

**Kabla ya kuondoka Ba<u>gh</u>dád, Bahá’u’lláh alitumia siku kumi na mbili katika bustani nje ya mji, ambapo msururu wa wageni walikuja kumuaga. Katika bustani hii, Bahá’u’lláh Alitangaza kuwa Alikuwa Mdhihirishaji wa Mungu wa Siku hii. Kwa karne zijazo, kipindi hiki cha siku kumi na mbili za mwezi Aprili zitasherehekewa kama Sikukuu za Riḍván, kumbukumbu ya Tangazo la Dhima ya Bahá’u’lláh ikumbatiayo ulimwengu mzima.**



Sulṭáni ‘Abdu’l-‘Azíz
wa Ufalme wa Ottoman



Nicolaevitch Alexander II
Czar wa Urusi



Francis-Joseph,
Mfalme wa Austria



Mfalme wa Wafaransa,
Napoleon III




Náṣiri’d-Dín Sháh
wa Uajemi



Papa Pius IX




Malkia Victoria
wa Uingereza



William I, Mfalme
wa Prussia

**Uhamisho wa Bahá’u’lláh uliofuata ulikuwa ni Constantinople na baadaye, Adrianople, miji yote miwili iko Uturuki ya siku hizi. Kutoka Adrianople, Bahá’u’lláh, mfungwa na mhamishwa, Aliandika barua kwa wafalme na watawala wa dunia akiwaamuru kuwa wenye haki na kutumia uwezo wao kukomesha taabu na vita.**



**Akiwa Adrianople, kama hapo kabla umashuhuri wa Bahá'u'lláh ulisambaa kwa wakazi wa ukanda huo na serikali iliamua kumhamisha tena mbali Zaidi kwenye mji-gereza wa 'Akká. Hili lilikuwa gereza ambapo waharifu wabaya kabisa na wachochea maasi wa nchi walipokuwa wakipelekwa ili uwe mwisho wao.**



**Hali za gerezani zilikuwa kali kupindukia. Baadhi ya wafuasi wa Bahá'u'lláh walitembea safari ndefu hadi 'Akká lakini hawakuruhusiwa kufika mbele Yake. Wangeona tu kidogo umbo Lake akiwapungia akiwa ndani kwenye dirisha dogo la chumba Chake cha gereza.**



**Taratibu mashariti ya kifungo yalilegezwa kadri idadi iliyoongezeka ya watu katika eneo hilo walivyotambua uwezo na ukuu wa Bahá’u’lláh. Katika kipindi cha miaka ya mwisho ya maisha Yake, Aliishi kwenye Jumba la Bahjí nje kidogo ya kuta za gereza. Akiwa ‘Akká, Bahá’u’lláh Alifunua vitabu vya mwongozo kwa binadamu kikiwemo Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Chake Kitukufu Kabisa.**



**Mnamo Mei 1892, Bahá'u'lláh Alifariki. Mapumziko Yake huko Bahjí, sasa pakizungukwa na bustani nzuri ni Mahali Patakatifu Kabisa duniani. Kila mwaka maelfu ya watu kutoka sehemu zote za dunia hutembelea mahali hapo kutoa heshima zao na kufanya sala na taamuli katika mazingira yenye utulivu.**

# MAREJEO


1. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 18 Aprili 1912, imechapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa Safari Zake kitengo hiki Anatamka na Canad katika 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2012), aya. 2, uk. 34.

2. *Wito wa Bwana wa Majeshi: Nyaraka za Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006), na. 3.14–15, uk. 248.

3. Kama hapo juu., na. 3.16–17, ku. 248–49.

4. *Wana Mapambazuko: Simulizi ya Nabil ya siku za mwanzoni wa Ufunuo was Kibahá’í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1932, 2018 kuchapisha), uk. 119.

5. Kama hapo juu., ku. 119–20.

6. Bahá’u’lláh, *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, 2016 kuchapisha), uk. 11.

7. *‘Abdu’l- Bahá juu ya Falsafa Tukufu* (Boston: Shirika la Uchapishaji la Tudor, 1918), uk. 53.

8. *Wana Mapambazuko*, uk. 96.

9. Kama hapo juu., uk. 104.

10. Kama hapo juu., ku. 104–5.

11. Kama hapo juu., ku. 105–6.

12. Kama hapo juu., uk. 106.

13. Kama hapo juu., uk. 107.

14. Kama hapo juu.

15. Kama hapo juu., ku. 107–8.

16. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Báb* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006, 2014 kuchapisha), na. 3:8.1, ku. 106–7.

17. Kama hapo juu., na. 3:27.1, ku. 126–27.

18. Kama hapo juu., na. 5:21.3, uk. 193.

19. *Wana Mapambazuko*, uk. 113.

20. Kama hapo juu., uk. 116.

21. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í1983, 2017), CXXIX, aya. 1–2, ku. 316–17.

22. Kutoka hotuba iliyotlewa na 'Abdu'l-Bahá juu ya 22 Mei 1912, uliochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 6, ku. 193–94.

23. *Wana Mapambazuko,* ku. 607–8.

24. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1988, 2005), na. 4.22, uk. 40.

25. Kama hapo juu., na. 7.40, uk. 96.

26. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, ku. 20–21.

27. *Wana Mapambazuko*, ku. 632.

28. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, uk. 21.

29. Kama hapo juu., uk. 22.

30. *Wito wa Bwana wa Majeshi*, na. 1.6, ku. 6–7.

31. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XXIX, aya. 5, uk. 80.

32. Kutoka barua ya tarehe 24 Juni 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, katika "Misukosuko na Ushindi: Mateuzi kutoka Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í", iliyokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, iliyochapishwa katika *Makusanyo ya Mateuzi* (Maryborough: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 1991), juz. 1, na. 287, uk. 148.

33. H. M. Balyuzi, *Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu* (Oxford: George Ronald, 1991, 2018 kuchapisha), uk. 106.

34. Bahá'u'lláh, ikinukuliwa na Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, 2019 kuchapisha), ku. 169–70.

35. Bahá'u'lláh, *Kitáb-i-Íqán: Kitabu cha Yakini* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2018 kuchapisha), aya. 278, uk. 231.

36. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, ku. 178–79.

37. Nabíl-i-A'zam, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, ku. 215–16.

38. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, uk. 22.

39. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, uk. 226.

40. *Kitáb-i-Íqán*, aya. 1, uk. 3.

41. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2003, 2012 kuchapisha), uk. 3.

42. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, uk. 147.

43. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1993, 2013 kuchapisha), aya. 75, uk. 48.

44. Nabíl-i-A'zam, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, ku. 240–41.

45. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XIV, aya. 1, 4–5, 11–12, ku. 29–34.

46. *Mungu Yu Nasi*, uk. 252.

47. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa ndani ya *Mungu Yu Nasi*, ku. 292–93.

48. H. M. Balyuzi, *Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu*, ku. 317–19.

49. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, uk. 292.

50. Tangazo la *Bahá'u'lláh kwa Wafalme na Viongozi wa Ulimwengu* (Haifa: Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá'í, 1967, 1972 kuchapisha), uk. 17.

51. Kama hapo juu., uk. 28.

52. Kama hapo juu., uk. 33.

53. Kama hapo juu., uk. 39.

54. Kama hapo juu., uk. 43.

55. Kama hapo juu., uk. 47.

56. Kama hapo juu., uk. 60.

57. Kama hapo juu., uk. 63.

58. Kama hapo juu., uk. 84.

59. Kama hapo juu., uk. 95.

60. *Mungu Yu Nasi*, uk. 325.

61. Edward Granville Browne, akirekodi maneno ya Bahá'u'lláh, ilinukuliwa na H. M. Balyuzi, *Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu*, ku. 378–80.

62. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas*, aya. 1–5, ku. 21–23.

63. Bahá'u'lláh, ikinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 350–51.

64. Nabíl-i-A‘zam, ikinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 351–52.

65. Bahá’u’lláh, katika *Sala za Kibahá’í: Uteuzi wa Sala na Dua zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2002, 2017 kuchapisha), ku. 323–27.